

**Mafundisho Ya Msingi  
Wa  
Kikristo**

**Na Andrew Connally**

## **YALIYOMO**

### **Milango ya Kitabu:**

1. Mungu-Kuwako kwake na hali yake
2. Huyo Kristo-Nafsi yake na kazi yake
3. Maandiko Matakatifu ni yenye pumzi ya Mungu
4. Mamlaka na Kufaa Biblia Zisiwe Zenye Mashaka:
5. Roho Mtakatifu
6. Kazi ya Roho Mtakatifu
7. Vipawa vya Miujiza vya Roho Mtakatifu
8. Ubatizo wa Roho Mtakatifu
9. Kipawa cha kueneza pote cha Roho Mtakatifu
10. Mafundisho juu ya Roho Mtakatifu Yasiyo Sawa
11. Asili na Hali ya Mwanadamu
12. Hali ya Sheria
13. Asili Na Hali Ya Dhambi
14. Hali ya Yale Maagano Mawili
15. Hali ya Injili
16. Hali ya Imani
17. Hali ya Utii
18. Hali ya Wokovu

### **Ukurasa:**

- 03
- 12
- 22
- 26
- 32
- 34
- 38
- 41
- 44
- 47
- 50
- 55
- 61
- 71
- 79
- 83
- 87
- 90

## **MUNGU - KUWAKO KWAKE NA HALI YAKE**

INGIZO:

A. Imani ya mwanadamu iliyo ya zamani kabisa na iliyo ya maana kubwa mno ni imani yake kwa Mungu. Bila ya imani ya aina hiyo maisha ya mwanadamu hayastahili kuwako, yaani hayana maana. Lakini ufahamu wa kweli unahitajika vile vile.

B. Nia yake mwanadamu juu ya Mungu hudhihirisha kadiri na aina ya ibada na utumishi wake. Ni kama kutufinyanga kweli maisha na matendo yetu. Mwanadamu ni matokeo ya imani yake.

C. Kusudi la masomo hayo ni kukupangia imani kwa Mungu iendayo ndani zaidi, na kukupa ufahamu wa Mungu ulio saw a na wa kukuwezesha kuishi kwa ajili yake na kukataa imani juu yake yenze ukosefu.

### **I. JINA LA "MUNGU".**

- A. Neno hila "Mungu" latokea mara 4067 katika Biblia.
- B. Mungu alikuwako kabla ya Biblia. Mwa. 1:1, Yn. 1:8.
- C. Kuwa kwake kwa milele, kuwako kwake, na kuwapo kwake huhakikishwa katika Biblia.
- D. Ni "mpumbavu" tu asemaye kwamba hakuna Mungu, Zab. 14:1.
  - 1. Nyakati zote watu fulani walijaribu kumkanusha Mungu. Lakini walimthibitisha tu.
  - 2. Katika mji wa Oxford, nchi ya Uingereza, mtu fulani aliwahutubia wasikilizaji wengi akisema, Nitathibitisha kwamba hakuna Mungu nikimbisha mpaka ataniua; akasema, "Hakuna Mungu". Msikilizaji mmoja aliyekaa nyuma akamwambia, "Namna' gani, wewe uduvi mdogo, Mungu hatapoteza mud a wake akimwua uduvi mdogo kama wewe."
- E. Majina ya Mungu.
  - 1. Jina liitwalo "Elohim" - Mara nyingine hutumika pamoja na "definite article", mara nyingine bila yake. Hutokea mara 2555 katika A.K.; mara 2310 kati yake hutaja Mungu yule mmoja wa pekee kwenye uhai, lakini mara 245 hutumika kwa njia nyingine isiyo ya maana kubwa kama ile. Labda "Elohim" alikuwa kama "Yule Mmoja wa, pekee aliyejifunua mbele ya mwanadamu kama mwumbaji, mtawala na Bwana". Lilikuwa jina lake la kipekee ambalo lisitumike kwa mwengine. "Mungu (EMhim, katika wingi) aliziumba (kat. umoja) mbingu na nchi."

Shetani aliingiza uzushi wa kwanza, Mwa. 3:5, alipowaeleza wengine watajulikana kwa jina hilo. Ibada ya Elohim ilikuwal imechafuka, watu wakitaja cho chote kwa jina hilo. Mwa. 35:1, 24. Hapa Elohim lilikuwa kama hirizi au sanamu. Mwa. 31:19 (toraphim) mst. 30 Elohim. Kut. 12:12; Law. 19:4; Kut. 32:3-5. Yatofautishwa kati ya Jehovah na Elohim

zote, Kut. 18:11; Kut. 20:3; 23:13; Kum. 4:39. Bwana alijitahidi kuwafundisha Waisraeli kwamba jina la Elohim ni jina lake peke yake.

2. Jina la Elohim na Utatu. Elohim, likiwa neno katika wingi, hairidhii wingi wa miungu (polytheism); lakini yatupasa tuufikirie uwezekano wa wingi katika Uungu; Mwa. 1:26. Rapo neno katika wingi latumika, ikiwa Mwa. 1:1 neno katika umoja Iaonekana. Waebrainia walipendelea kutoa maneno yaliyo katika hali ya wingi ili kwa maneno hayo maana maalum na ya mtindo ionekane; ling. Damu, Maji, Hekima, Wokovu, Maisha, n.k. Yaani hali{ya umoja ya maneno hayo haikutosha kueleza yote ambayo mwandishi aliyakusudia. Majina mengine ya Mungu ni katika hali ya wingi, Mhu. 12:1 (Waumbaji, kat. wingi).

3. Matumizi mengine ya jina hilo "Elohim" Kut. 4:16, hapo maana yake ni kuwa mjambe wake, siyo kuwa sawa naye, ling. Zek. 12:8. Hapo jina la Mungu lilitumika kwa mtu aliyekuwa mjambe wake, Kut. 7:1. Hayo yalielezwa wazi na Yesu katika Yn. 10:34-36 (Zab. 82; Kut. 22:8-9). Kama wale walikuwa wajumbe wa Mungu, Yesu alikuwa mjambe wake zaidi. Mara nyingine waamuzi walikuwa wametajwa Elohim, Kut. 21:6. Hapo maana yake siyo kwamba watu watajwao Elohim wastahili kuabudiwa, bali watu hao ni jamii ya mahakimu watajwao jina hila kwa sababu watenda kazi badala ya yu1e Elohim mmoja na wa kweli, 19:17.

4. Utumiaji wa jina la Elohim kwa malaika. Zab. 8, "Malaika kwa Kiebrania ni Elohim".

5. Mwenyezi - Shaddai. Jina hilo kwa kweli humkumbusha msomaji Mwebrania utajiri na neema ya Mungu. Mpaji wa kila kitu, Mwa. 35:11; 43:14; Mwa. 49:25 (Ezi ya Mungu ya El - Shaddi - Uzuri wake).

6. Bwana - Adonai - Jina hilo limetoka kwa neno lile Adon ambalo maana yake ni Mungu, au kwa lugha ya Kiyunani ni Kyrios - Bwana; ling. Mwa. 43:24; Mwa. 24:9. Jina hila laweka wazi ukweli ule kwamba kila mwanachama wa jamii nzima ya kibinadamu ni mali ya Mungu, na kwa hiyo Mungu anataka utii kamili wa wote. Jina hilo lilitumika mara ya kwanza kwa Mungu katika Mwa. 15:2; 15:8; 18:3. Mwa. 15:2 yasemwa hasa, "Bwana wangu Jehovah". Kum. 10:17 "Bwana wa Mabwana", au hasa, "Mkuu wa Wakuu", m.y. Mungu Mkuu wa wote walio na mamlaka ya kuyashika mikononi mwao. Jinsi matakwa ya Mungu kwa utumishi wa mwanadamu yaonekanavyokwa jina hila Adoni, yajulikana katika Mal. 1:6.

7. Aliye Juu - Elion - Jina hilo lilitumika mara ya kwanza katika Mwa. 14:18-22, Hes. 24:16; Kum. 32:8; Mdo. 17:26. Katika Zab. 89:27, jina hilo latumika kwa Masihi. Neno hila halitokei katika matumizi ya lugha ya dini tu, ling. Mwa. 40: 17; 1 Fa! 9: 8; Neh. 3:25, n.k.

8. Jehovah. Jina hila latokea mara 5,500 katika A.K. Mara nyingi neno lile "Bwana" limeandikwa badala yake. Katika tafsiri nyingi za lugha nyingine "Jehovah" hutafsiriwa kwa "Aliye wa milele". Kama neno laweza kujulisha wazi maana yake nini, ni neno hilo. Yafahamika kwamba Jehovah ni jil1a la binafsi ambalo hutumika kwa Mungu, yaani kwa Mungu tu. Fikirie Kut. 3:14; 6:1-3, "Mistari hii miwili ikitazamiwa pamoja yafafanua mambo hayo yafuatayo:

Kwanza, hata kama jina la Jehovah lilitumika sana kama jina la Elohim wa Mababa Wakuu wa A.K., hat a hivyo maana yake iliyo kamili haikufunuliwa mbele yao; Pili, jina hila lilihusika hasa na utimilizo wa agano na ahadi ya Mungu ili sasa baada ya kame nyingi zilizopita maana ya kweli ya jina hilo iwekwe wazi kwa ufunuo wa Yule binafsi mwenye uhai, akifanya kazi kwa ajili ya Waisraeli ili ahadi ile iliyofanyika kwa Mababa ittimizwe. Hivyo ndivyo, fikra ile adhimu juu ya Mungu wa milele asiyebadilika akikaa kuwa mwaminifu katika neno lake kwa muda wa vizazi vingi, ilivyanza kufahamika katika mawazo ya Waisraeli, na yale yaliyotumainiwa na kutiwa muhuri wa jina hila nyakati za Mababa Wakuu, yalianza kujifunua yenyewe kuwa katika hali ya ukweli. Kuwako kwa Mungu binafsi, jinsi aendeleavyo kufanya kazi pamoja na wanadamu, jinsi ahadi zake zisivyobadilika, na ufunuo kamili wa neema yake ikomboayo, hayo yote yakusanyika katika jina hilo Jehovah. Siyo "Elohim asema hivi", bali ndiyo "Jehovah asema hivi", ambalo ndilo ingizo 1a kawaida 1a taarifa za manabii. Akiwa Jehovah, ndiyo Mungu amekuwa Mwokozi wa Waisraeli, na kama Jehovah akomboa ulimwengu; na huo ndio ukweli uliowekwa ndani ya jina la Yesu, ambalo maana yake ndiyo JehovahMwokozi hasa."

Katika Mwa. 9:26 Jehovah ni MU11gu wa Shemu; Mwa. 14:22 yadhaniwa kuwa sawa na E1-Elion "Mungu aliye Juu". Katika Mwa. 15:1 "neno la Jehovah ----" Jehovah mwenyewe hasa. Aliye mhukumu, Mwa. 18:25. Mababa Wakuu walishauriana na Jehovah, Mwa. 18:1-2; 28:13-17; 32:24. Musa alizungumza naye uso kwa uso, Kut. 33:9-11. Ufunuo ulifanyika na Jehovah, Kut. 34:6-7. "Hapo twaona maana kamili ya Jehovah - neema yake na nafsi yake ya hukumu; yaani kama jina la Elohim huweka wazi nguvu ya Mungu aliye mwumbaji na mfululizaji, Jina la Shaddai likionyesha uzuri wake, na jina hilo la Jehovah ambalo hufunua tabia zake maalum zisizogeuka, yaani tabia zake za neema na hukumu, akionekana kuwa Baba, Rafiki na Mtawala mwenye adili.

9. Bwana wa majeshi (jina "Jehovah" latumiwa) au Bwana wa Sabbato, jina lile 1a kwanza likiwa utafsiri wa lile la pili. 1 Sam. 1:3, Rum. 9:29; Yak. 5:4 na vv. Kut. 12:41; Waisraeli ni "majeshi ya Bwana", maana yake kwamba Jehovah ni akida au mlinzi wao. Wengine hutaja "Mwenye mbingu". Labda Myahudi alifahamu maana yake hivi kwamba Mungu

ana vyama vyote vya ulimwengu na vya dhamira chin'i ya mam1aka na madaraka yake akivisimamia jinsi atakavyo. Taz. Zab. 147:4; Isa. 40:26.

10. Malaika wa Bwana, jina la Jehovah latumika tena. Mwa. 32:1-3; "Malaika afahamika kuwa Jehovah mwenyewe. Mwa. 16:7-13; Zek. 3:2, "Malaika wa Bwana, - Bwana na akukemee". Wengine waona kwamba ni Kristo; lakini hakuna hakika; taz. Mt. 2:13. Katika Zek. 1:12 Jehovah na Malaika ni tofauti, kwa sababu Malaika amsihi Jehovah. Malaika yule ali-kuwa wakili wake Jehovah akiyaimarisha na kuyatimiliza mapenzi ya Jehovah.

## II. USHUHUDA WA KUWAKO KWA MUNGU

- A. Ushuhuda wa Kihistoria: Kuwako kwake kwa kihistoria hakuna mashaka.
  1. Mungu alimwumba mwanadamu. (Kama mwanadamu alimwumba Mungu, ni nani aliyemwumba mwanadamu?)
  2. Katika fikra za mwanadamu kutoka zamani sana ni imani yake kwa Kitu maalum cha Juu.
  3. "Hata taifa ambalo hali yake ni ya kishenzi kabisa, na hata watu wale wasiostaarabika, hata wao wamwamini Mungu," alisema Cicero.
  4. Shuhuda za kihistoria zimekuwa za dunia nzima kutoka mwanzo wa wakati na wa mwanadamu.
- B. Ushuhuda zihusuzo ulimwengu ulivyo (cosmological evidence):
  1. Kutoka mwanzo wa wakati wanadamu walikuwa wameishi katika ulimwengu mzuri mno wenye utaratibu.
  2. Juu ya uzuri wa ulimwengu amba mwanadamu huishi ndani yake, mmoja alisema, "Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu, na anga laitangaza kazi ya mikono yake." (Zab. 19:1).
  3. Mbingu na dunia hazikuwa zimetokea kwa bahati, 2 Pet. 3:5.
  4. Hapa duniani twapata ushuhuda jinsi Mungu alivyouumba kwa mikono yake.
    - a. Paulo alisema, "Kwa sababu mambo yake yasivyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, ..." Rum. 1:20.
    - b. Moyo wa mwanadamu huona mambo ambayo akili yake haiwezi kuyaona.
    - c. Mwasi mmoja wa Kifaransa aliwaambia wakulima fulani, "Nitaubomoa mnara wa kanisa lenu ili msiwe na kitu cha kuwakumbusha imani yenu ya usihiri tena." Wakulima wakajibu, "Huwezi kubomoa nyota".
- C. Ushuhuda unaomgusa mwanadamu ndani ya moyo wake (intuitive):
  1. "Mwanadamu alikuwa am eon a kwa moyo wake kwanza, kabla hajaanza kufikiri kwa akili yake."
  2. Kisa juu ya bata Bukini wawili wa shamba huko Amerika ya Kusini. Wakati wa uhamaji hao wawili walifanya ya ajabu. Yule dumeakiwa mbele akienda moja kwa moja, yule jike alikwenda kuelekea kusini ya mashariki. Yule dume alianza kuruka na kumwita yule jike kwa wito wa

kumsihi sana. Baada ya muda mfupi tu dume aliona kwamba yule jike alikuwa, amevunja ubawa wake. Lakini hata hivyo dume hakumwacha. Hali hii ya kusihi ni kitu cha msingi ndani ya mwanadaamu.

3. Ushuhuda unaomgusa mwanadamu ndani ya moyo wake si njozi iliyo tupu, bali ni kitu muhimu kweli.

4. Augustino alisema, "Miyo yetu haiwezi kupata raha mpaka itapumzika ndani ya Mungu."

5. Siku fulani kijana mmoja alikuwa amerusha tiara yake. Mtu mmoja akamjia akamwuliza afallyaje? Yule kijana akajibu, "Ninarusha tiara yangu." Yule mtu akasema, "Siwezi kuiona". Kijana huyo akajibu, 'Hata mimi siwezi kuiona, lakini najua kwamba ipo sababu inavuta."

D. Ushuhuda wa mambo tupatayo kuyafahamu kwa njia ya kidini:

1. Kama wale waliofariki tangu wakati wa Kaini wangeweza kufufuka na kusema, tungepata kufaharnu kutoka kwao kwarnba Mungu yupo.

2. Twajua kutoka kwa mambo mbalimbali ya maisha yetu kwamba Mungu wa ulimwengu huu yupo.

3. Labda mwengine ana ujuzi mkubwa zaidi katika mambo ya saiansi n.k. kuliko sisi, na kutoka kwa ujuzi wake 1abda atajaribu kutoa hoja kwamba hakuna Mungu. Lakini "futi sita za udongo zafanya watu wote kuwa sawa"; mfuasi wa Mungu ana mbingu, walakin yule asiyemwamini Mungu, ana jehanum.

E. Ushuhuda wa Biblia.

### III. TABIA ZA MUNGU - HALI YAKE

A. Utawala na nguvu zote (Omnipotence) za Mungu.

1. Mungu aliumba kila kitu kwa neno la nguvu yake. Alisema, na vitu vyote vilikuwa 'vimetokea (Uumbaji). Mwa, 1:3.

2. Paulo alisema, "Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa neno la Mungu," Ebr. 11 :3.

3. Mungu ana uwezo kuharibu roho na mwili katika Jehanum. Mt. 10:28.

4. Kwa nguvu yake Mungu kuta za Yeriko, zilibomolewa, jua lilikuwa limesimama, waliofariki walikuwa wamefufuliwa, viwete waliponywa, viziwi walifumbuliwa masikio yao, kaburi Yesu lilifunguliwa, na Kristo alikuwa amefufuka.

5. Kwa nini mti mwengine huzaa matunda merna na mwengine huzaa matunda yenye sumu? Kwa nini wanyama wengine huonekana kuwa na akili zaidi kuliko wengine? Kwa nini mimea mii1gine huzaa matunda mara nyingi ki1a mwaka na mingine huzaa mara moja tu kwa mwaka? Jibu la pekee kwa maswali hayo ni Utawala wa Murigu katika yote. Zab. 135:6.

6. "Kama Mungu ana nguvu zote, kwa nini basi kuna vita, maovu n.k.?", swalii hilo huulizwa na watu wengi.

a. Jibu kwa swalii hila lapatikana Yn. 18:36, "Ufalme wangu sio wa ulimwengu huu, Mt. 6:10, "Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni. "

b. Lk. 2, Malaika hawakuwatangazia Makuhani Wakuu habari za Kuzaliwa kwa Yesu, ingawa wale walikuwa viongozi wa dini wa sikuzile. Hata hivyo malaika waliwaendea wachungaji tu waliokaa peke yao.

c. Mara nyingi Mungu hayatimizi mambo kwa jinsi ile wanadamu watakavyo ayatimize; Lakini hata hivyo Mungu ana nguvu zote.

d. Amani ni kitu cha binafsi. Imo miyoni mwa wale wafanyao mapenzi ya Mungu.

e. Kaisari Napoleoni Bonaparte alikuwa amemwaga damu za watu wengi katika nchi nyirtgi akijaribu kushika ufalme wake kwa nguvu. Kabla hajafa akikaa katika kisiwa cha St. Helena, aliungama kwamba upo ufalme mmoja tu udumuo milele yaani ufalme wa Kristo uliokuwa umeanzishwa na kudurnishwa kwa upendo.

B. Kujua yote (Omniscience) na Hekima ya Mungu:

1. Mungu alijua kila kitu kabla ya wakati, ataendelea kujua yote baada ya wakati.
2. Kila kituni wazi na tupu mbele ya Mungu. Ebr. 4:13.
3. Paulo alieleza hekima ya Mungu katika 1 Kor. 1:20-25.
4. Kuanzia na mwanamke yule wa kwanza Hawa mpaka siku hizi, wanadamu wamejiona wenye kuwa na hekima kubwa zaidi kuliko Mungu, lakini baadaye wameonekana kuwa wapumbavu.
5. Isa. 55:8-9, Ukiujumlisha hekima zote za watu wote wenye ujuzi, utapata kastabini tu ya hekima ile aliyo nayo Mungu.

C. Kuwako kwa Mungu mahali po pote (Omnipresence):

1. Mungu yupo ndani ya ulimwengu huu na nje ya ulimwengu huu vilevile. Utukufu wake upo po pate.
2. Mungu yupo pamoja na wale wanaoona uchungu hapa na po pote. Yupo nchini pa wale waliofariki hapa na po pote. Yupo pamoja na wale wahubiri na wamissionari wengi - nchini hapa na katika dunia nzima.
3. Mungu hayupo po pote katika maisha hayo tu, bali ye ye ndiye peke yake vilevile ambaye anaweza kwenda pamoja na wapendwa wetu "katil ya bonde la uvuli wa mauti," Zab. 23:4.
4. Habari za mume na mkewe walioishi pamoja kwa muda wa miaka hamsini. Hawakutengana katika maisha yao hata kidogo. Wakati yule mke alipokuwa karibu na kufa, alimwambia mumewe, "Jim, mimi nipo karibu na bonde la mauti. Nenda pamoja nami." Akamshika mkono wake kwa nguvu kubwa zaidi kidogo. Yule mume akamjibu, "Mary, ningependa kwenda pamoja nawe, lakini ni Kristo peke yake ambaye anaweza kwenda pamoja nawe sasa". Hiyo ndiyo maana ya Kuwako kwa Mungu mahali po pote.

#### IV. MAFUNDISHO JUU YA MUNGU NA HALI YAKE YASIYO KWELI

Tangazo: Katika masomo mafupi kama hayo hatuwezi kueleza lo lote kwa urefu, lakini twawezakuorodhesha makosa machache yatokeayo tena na tena katika Dini mbalimbali zilizo ulimwenguni.

A. Dini ya Umormoni (Mormonism): Joseph Smith alikuwa amefundisha wingi wa miungu mbalimbali. Tangu mwaka 1844, Joseph Smith alikuwa akidharau kabisa mafundisho ya Kitabu cha Mormoni, yaani alieleza kwamba Mungu ni mwanadamu tualiyeinuliwa juu, na hata wanadamu waweza kuwa kama miungu.

Angalia:

1. "Kwanza, Mungu mwenyewe akaaye akitawazwa huko mbinguni ni mwanadamu kama mmojawenu, hii ndiyo siri iliyo kuu .... Mungu mwenyewe ambaye ni baba wa sisi sote alikuwa amekaa duniani kama Yesu Kristo mwenyewe alivyofanya .... Ni lazima mjifunze kuwa kama miungu wenyewe. Hakuna mtu awezaye kuwafundisha ninyi zaidi kuliko mimi niliwaeleza". (Times and Seasons, Kit. 5, uk. 613-614). Mtume wa Kimormoni, Orson Pratt, alitoa fundisho hilo lifuatalo juu ya wingi wa Miungu.
2. "Hiyo ndiyo ilezayo siri. Kama tungeshika millioni moja ya dunia mbalimbali kama dunia hii, na kama tungejumlisha vipande vyao vyote, basi tungeona kwamba katika dunia hizo kuna miungu mingi zaidi kuliko vipande vile" (Journal of Discourses, Kit 2, uk. 345).
3. Kanisa la Kimormoni lafundisha kwamba Mungu mwenyewe alikuwa na baba yake, na baba huyo alikuwa na baba vilevile, n.k. (Ni kama kusema kwamba wewe u babu yako mwenyewe!! A. M. C.) Brigam Young alisema, "Ndugu Kimbell alipasha usemi wa Nabii Yosefu kwamba asingemwabudu Mungu yule ambayc hanababa; na mimi sijui kwamba angefanya hivyo kama asingekuwa na mama; neno lile moja ni la upuzi kama lile lingine" (Journal of Discourses, Kit. 9, uk. 286).
4. Herbert C. Kimbell aliyekuwa mmojawao Wakuu wa Wakati wa Kwanza, alisema "... halafu tutamrudia Baba yetu yaani Mungu aliyekuwa ameunganishwa na mmoja ambaye alikuwa amekaa kabla yake; na baba huyo alikuwa ameunganishwa na mmoja vilevile ambaye alikuwa amekaa kabla yake tena, na kadhalika", (Journal of Discourses, Kit. 5, uk. 19), n.k. Ad-Nauseam! (= mpaka kupuzia).

B. Dini ya Uhindi - "Kuna Kitu kimoja cha asili chenye ukweli, ambacho ni cha juu kuliko vyote, kisichochanganyika na kitu kingine, ambacho kinaitwa Brahman. Brahman ni kama utulivu. Hakuna maneno yavezayo . kuueleza; hakuna wazo ila kibinadainu ·liwezalo kuchungua tabia yake; hakuna filosofia iwezayo kueleza maana yake.Ni zaidi na nje ya yote yaliyowekwa chini ya nguvu ya mauti na maisha. Ni zaidi ya ufahamu wa yule ajuaye na yale y:mayofahamika. Ni zaidi kuliko maelezo yote yanayoelezwa kuwa yakupendeza au ya kutokupe-ndeza katika maisha yetu yenye mwisho wake. Maana yake haina mwisho. Haiwezi kushikwa ndani ya mipaka yo yote. Kutokana na hayo ni ile Halisi hasa isiyohusika na ulimwengu huu, tena isiyowekwa chini ya vitendo vyote

walachini ya matokeo yake. Kwa hiyo tabia kamili ya ile Brahman haiwezi kujulikana wazi, lakini hata hivi ni yule "Mimi' wa kweli." (Introducing Hinduism, na Malcolm Pitt, uk. 17-18).

C. Dini ya Uislamu - "Tendo lile moja kubwa kabisa la nabii Muhammed lilikuwa lile la kuanzisha dini ile ambayo inashika karibu kwa ushupavu kwamba Mungu ni mmoja ... Nguvu yake na mamlaka yake juu ya viumbe vyote, hiyo ndiyo inayodhihirishwa mno katika Uislamu kiasi hiki kwamba ni vigumu kwa Mwislamu kumwita Mungu kuwa Mungu wa upendo au kumtaja Baba. Utakatifu na haki yake Mungu hazidhihirishwi kuwa msingi wa matendo yote, kama zilivyo katika Agano la Kale. Allah ajulikana kuwa 'Bwana wa dunia zote, au 'Mtawala wa ulimwengu' na kama 'Bwana wa Siku ya Hukumu' .... Kufuatana na mafundisho ya Kiislamu, nguvu na kutokubalika kwa Allah zamfanya kuwa mwumbaji wa vitu vyote, yaani wa vitu vyema na vitu vibaya vile vile; fundisho hilo huelezwa katika sehemu nyingi za Kurani.

"Kuna orodha ya majina mazuri tisini na tisa ya Mungu yanayo julikana kwa Waislamu. Yasemeka kwamba ni ngamia tu ajuaye jina lile la mia moja, na hiyo ndiyo inayompa ngamia tabia yake ya heshima. Tasbihi ya kawaida ya Kiislamu ina shanga tisini na tisa, au vifungu vitatu vya shanga thelathini na tatu; na kila ushanga umewekwa badala ya jina moja la yale 'majina mazuri' ya Allah.

"Dr. Paul Harrison ambaye ni mmissionari wa miaka mingi katika nchi ya Arabia asema kwamba hawajui watu wengine amba wanamfikiri Mungu kuwa juu kabisa kama Waislamu, hata hivyo imani hii haigusi sana adilifu ya maisha yao ya kawaida." (Alama zime wekwa na mwandishi A. M. C.) Introducing Islam, na J. Christy Wilson, uk. 19, 20, 21.

D. Dini ya Uanismi - Maelezo yake: "Pundisho liIe la zamani ipo nguvu fulani (Anima Mundi, nafsi ya ulimwengu) ambayo haina sura yenewe, lakini haiwezi kutengwa na vitu, tena yatia vitu sura na mwendo wao; ni kama kutia roho au nafsi katika vitu visivyo na nafsi bado." Educational Book of Essential Knowledge, uk. 34.

1. Uanismi hupatikana sana katika dini zote za zamani, lakini kwa kawaida Uanismi hupatikana hata katika dini zile maalum kama Ukristo, k.m. (viapo, dalili, ustahifu wa utajiri, nguzo zenye rangi, n.k. - Mkune Mwamerika, utapata mpagani vilevile!)
2. "Mwanismi kwa kawaida humwamini "Mungu mmoja aliye juu" - yaani Mungu ambaye kwa maneno afanana kidogo na Mungu wa Ukristo, lakini kwa vitendo nitofauti sana" Ingawa wafuasi wake wasema kwamba aliuumba ulimwengu, lakini mara nyingi haonekani kuwa na nguvu nyingi. Yeye ni kama Mungu wa kwanza tu mionganoni mwa miungu mingi ambayo ni sawa naye. Kwa kawaida ametengwa akikaa mbali na wanadamu, pia haabudiwi kwenye madhabahu yo yote wala haheshimiwi kwa kupewa zawadi zo zote." Introducing: Animism, na Eugene A. Nida, Will A. Smalley, uk. 15.

3. Katika Uanismi kuabudiwa kwa majadi kuna maana kubwa katika imani hii. Yanayohusu ufahamu, hofu na imani yao, mara nyingi ni vigumu sana kutofautisha kati ya ibada yao kwa majadi na ibada yao kwa miungu. Mungu kama Jehovah ni Mungu wa kigeni sana mbele yao ambaye hajulikani kwa wafuasi wa dini ile; lakini hata hivyo mara nyingi wapo tayari kujifunza jinsi ya kumtambua vema.

4. "Msingi mkubwa wa dini ya Uanismi ni hofu hasa. Mwanismi huishi katika hofu kucha kutwa akiogopa pepo mbalimbali ambazo, kufuatana na imani yake, zamzunguka kila mahali. Ni zile pepo zilizo na madaraka na wajibu juu ya kila kitu kinachotokea. hakuna sababu nyingine za kawaida. Maisha yote katika kila jambo yamejaa hofu ya pepo. Nyakati zote kama zile za kuzaliwa kwa mtoto, arusi, kujenga nyumba, kupanda mimea au wakati wa mavuno, lazima pepo ziheshimiwe. Wanaoishi wanateswa na hofu kwa yule ambaye amekufa, wakifikiri kwamba pepo zake huzunguka kijiji chao kukisumbua. Sadaka hutolewa kwa njia ya madhabihu, ili pepo za yule aJiyefariki zitoke kwenda mahali pao. Hudhaniwa kwamba pepo hukaa kwenye mahali pa pekee, kama kwenye miamba ya mtindo, miti mitakatifu, maporomoko ya majiau chemchemi zenye maji yanayotumika kama dawa." Religions in a changing world, na Haward F. Vas, mtengenezaji, uk. 25.

AZIMIO:

Mtu mwaminifu hawezi kuwa na mashaka juu ya kuwako kwa Mungu. Kama akitoa mashaka ni kwa sababu amekataa ushuhuda uliopo po pote juu ya Mungu. Hali tukufu ya Mungu ni hivi kwamba Mungu aweza kufanya 10 late. Lakini tabia zake hazimruhusu Mungu kufanya zaidi kwa ajili ya mwanadamu kuliko amekwisha fanya. Hekima yake yamfanya Mungu alijue limfaalo mwanadamu zaidi, na kuwako kwake mahali po pote kwamwezesha kuwapo kila mahali wakati wo wote. Hivya ndivyo Mungu alivyopanga kila kitu vizuri. Kweli, Mungu ni Mungu Mkuu! Je, wataka kumtumikia?

## HUYO KRISTO - NAFSI YAKE NA KAZI YAKE

INGIZO:

- A. Kusudi la somo hila ndiyo kuchungua Yesu Krista Bwana wetu alivyo na kazi yake katika Agano Jipyा.
- B. Baada ya Mungu, ni Kristo ambaye ni wa maana kubwa katika Biblia na katika historia nzima.
1. Agano Jipyा hueleza juu ya nafsi ya mmoja. Hueleza juu ya tokeo moja ambalo Yesu Kristo ni katikati yake.
  2. Katika Kristo, Mungu amekuja, Yn. 1:4. Yeye ndiye Neno aliyefanyika mwili; Yeye ndiye Imanueli, yaani Mungu pamoja nasi, Mt. 1:23.
  3. Ukristo haurudii tu mpaka usharika ule wa kwanza wa wanafunzi, bali msingi wake ni ndani ya Yesu wa Nazareti.
- C. Injili zina msingi wao ndani ya Kristo.
1. Marko huijulisha injili yake kama "Injili ya Kristo," Mk. 1:1.
  2. Kusudi la Luka ni hasa kuzungumzia "mambo yale yaliyotimizwa katikati yetu." Lk. 1:1; Mdo. 1:1.
  3. Mathayo, injiji yake ni juu ya "ukoo wa Yesu Kristo, mwana wa Daudi." Mt. 1:1.
  4. Yohana, injili yake ni juu ya "Nena alifanyika mwili" Yn. 1:14.
  5. Bila Yesu, yaani nafsi yake, mafundisho yake na kazi yake, Injili hizo Nne hazingekuwa kitu.
- D. Usawa wa Agano Jipyा una msingi wake ndani ya Krista vilevile.
1. Paulo alisema kwamba haazimu kujua lolote ila Kristo, I Kor. 2:2.
  2. Uumbaji, ukombozi na ufunuo zafuatishwa katika Yesu, Yn. 1:1-2; Efe. 1:1-8; Gal. 1:15-16.
  3. Kwa Petro, Kristo ndiye "jiwe lililo hai," 1 Pet. 2:4. Ndani yake tunalo "tumaini lenye uzima." I Pet. 1:3.
  4. Kitabu eha Ufunuo ndio "Ufunuo wa Yesu Kristo," Ufu. 1:1.

### I. CHEO KINACHOSHIKWA NA YESU KRISTO.

- A. Yesu ndiye ashikaye cheo ambaeho mwingine hakushika wakati wo wote.
1. Charles Lamb alikuwa akihudhuria nafasi ya chakula eha adhuhuri, pamoja na watu wengi waliokuwa watukufu sana; Walikuwa wakizungumzia juu ya "Mtu ambaye ningependa sana kumwona kuliko mtu yeyote mwingine." Wengine walisema, Shakespeare, Milton, Bunyan, Lamb alisema, Kama ye yote wa wale angeingia hapa sasa, sisi tungeinama; lakini kama Yesu angeingia hapa sasa, sisi tungepiga magoti tungelia kama Tomaso alivyolia akisema, "Bwana wangu na Mungu wangu." Yn. 20:28.
  2. Mt. 16:13, Yesu aliwaauliza wanafunzi wake, "Kristo ni nani?" Vilevile aliwaauliza Mafarisayo, "Mwaonaje katika habari za Kristo?" Mt. 22:42.

- B. Vitabu vingi vimeandikwa juu ya watu waliokuwa wakuu na muhimu, lakini mamillioni ya vitabu vimeandikwa na waandishi waaina mbalimbali juu ya Kristo.
- C. Mistari mikuu ya nyakati zote imepigwa ikizungukia hori ya Yesu.
- D. Karibu kila mtu ajua juu ya Yesu. (Wale waliosoma na wale wasiosoma vilevile, n.k)
- E. Mara nyingi watu hawashindani na Kristo, bali hushindana na wajumbe na wafuasi wake katika udhaifu wao, Mt. 5:6.

## II. MAFUNDISHO YA AGANO JIPYA JUU YA YESU KRISTO:

- A. Kutoka mwanzo mpaka mwisho Agano Jipyä huzungumza juu ya Kristo, Mt. 1:18-25; Yn. 1:29.
- B. Watu wengi wanajulikana sana leo kwa sababu ya Kristo.
  - 1. Kama Pilato asingaliongea na Kristo, waehaehe tu wangalilija jina la Pilato baadaye.
  - 2. Ndiye Paulo ambaye ndiye juu ya Nero, na vilevile ndiye Kristo aliye juu ya Pilato.
  - 3. Siyo jinsi sisi tumwonavyo Kristo, baJindiyo jinsi Kristo atuonavyo sisi.
- C. Agano Jipyä hufundisha kwamba Kristo alikuwako kutoka ,hapo mwanzo.
  - 1. Je, alikuwa kama wanadamu wengine? Je, alikuwa mwanzoni?
    - a. Yeye hakuzaa. bali alikuwaamejalia; siyo kwamba yeye amezaa, bali ametia nguvu yake.
    - b. Mvuto wake ulikuwa mkubwa kuliko watu walivyoweza kuufanyiza wenyewe.
  - 2. "Haiwezekani kwamba yeye aliye katikati ya makuu ya historia hana mahali pa kutokea," Crumout.
  - 3. Akili na maarifa hufundisha kwamba Kristo alikuwako kutoka hapo mwanzo.
  - 4. Maandiko Matakatifu hufundisha kwamba alikuwako hapo mwanzo.
    - a. Yn. 1:1-2. Si kitu cha maana. mwanzo ulikuwa lini. Kufuatana na hati fulani za nasaba. wan adamu walianza kuishi hapa duniani miaka elfu sita mpaka elfu nane iliyopita. Hii inayategemea mawazo mengi mbalimbali.
    - b. "Wala hakuna mtu aliyepaa mbinguni. ila yeye aliyeshuka kutoka mbinguni. yaani Mwana wa Adamu." Yn. 3:13.
    - c. "Wala sikuja kwa nafsi yangu, bali yeye ndiye aliyenituma." Yn. 8:42.
    - d. "Yesu akawaambia, Amin, amin, nawaambia, Yeye Ibrahimu asijakuwako, mimi niko." Yn. 8:58.
    - e. "Na sasa, Baba, unitukuze mimi pamojanawe, kwa utukufu ule niliokuwa nao pamoja nawe kabla ya ulimwengu kuwako." Yn. 17:5.
    - f. "Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho ..." Flp. 2:5-6.

D. Kristo hakuwa hapo mwanzo tu, bali alikuwako hapo mwanzo pamoja na Mungu.

1. Yeye ndiye mmoja na Mungu, Yn. 10:30, 14:9. (Mmoja katika "nafsi wa kuwako kwake", Ebr. 1:3), 2 Kor. 4:4; Kol. 1:15; Flp. 2:6.
2. Hakuna mume wala mke ambaye ni mmoja zaidi na mwenzake, kuliko Yesu ni mmoja na Mungu. Hakuna mtoto ambaye ni mmoja zaidi na mamake hat a wakati wa kuchukua mimba, kuliko Yesu ni mmoja na Mungu.

E. Yesu alikuwa mwumbaji pamoja na Mungu.

1. "Alikuwako ulimwenguni, hata kwa yeye ulimwengu ulipata kuwako," Yn.1:10.
2. "Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa," Kol. 1:16.
3. "Aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu." Ebr. 1:2.
4. "Umestahili wewe, Bwana wetu na Mungu wetu, kuupokea utukufu na heshima na uweza; kwa kuwa wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote ..." Ufu. 4: 11.
5. Sahihi ya Kristo imeandikwa katika mwezi aliouweka katika bustani ya nyota.

F. Yesu Kristo ni Mungu.

1. Mungu wa Utatu, Mwa. 1 :26; kwa sababu hakuna Mungu mwingine ila Jehovah, (Isa. 43:10), lazima pawe na "umoja" katika wingi na katika nafsi yake, au mstari ule hauna maana. Hii yahu Mwa. 11: 7 vilevile.
2. "Mamlaka yote mbinguni na duniani" ni ya Kristo. Mt. 28:18. Ama ana "yote" au alikuwa akidanganya.
3. Kristo anadai heshima yote, kama vile wanadamu wanavyomheshimu Baba, Yn. 5:23.
4. Amefunuliwa kama Jehovah - Mungu katika sura ya mwanadamu, Isa. 9:6; Mik. 5:2; Yn. 1:1; 8:58; Ebr. 1:3; Flp. 2:11; Kol. 2:9; Ufu. 1:8; 1:17-18. Uungu wa Yesu Kristo ni jiwe la pemberi katika Ukristo, na ikiwa ndivyo ilikuwa imeshtakiwa zaidi katika muda wa kame nyingi, kuliko fundisho 10 lote lingine la Imani ya Kikristo. ("Isa. 9:6 katika Biblia ya Kiebrania ni mstari wenye nguvu kabisa katika AX.; mstari huu unahakikisha Uungu wa Yesu Kristo na kuthibitisha pasipo shaka kwamba Jehovah mwenyewe ameweka mpango atokee katika sura ya mwanadamu. Mamlaka yote yatakuwa mkononi mwake, na nafsi yake inafunuliwa katika maneno yale yale yanayotumika kueleza tabia zake - tabia hizo zote zikiwa za Mungu peke yake.")

G. Jina la Kristo:

1. Kristo - Christos - "Mtiwa mafuta", Masihi katika Septuaginta - neno lililotumika kwa ye yote aliyetiwa mafuta matakifu, hasa Kuhani Mkuu, Law, 4:3; 4:5, 16. Lategemezwa na Dan. 9:25, Zab. 2:2 latumika kumtaja Mwokozi angojewaye kama Mtiwa mafuta wa Mungu awe Mfalme na Mkombozi wa watu wake, Lk. 23:8, 35, 37. (Kama cheo chake cha Mfalme chaeleza uhusiano wake na watu, na aina yake ya kutawala, hivyo ndivyo jina hila la Krista lielezavya asili ya cheo chake cha Kimungu.)

Ho-Christos - (likiwa na nena kama "Yule") - katika vitabu vya Injili na Matenda ya Mitume: Yule Mtiwa mafuta, Yule Krista, Yule Masihi.

"Katika lugha ya Kiyunani nena hila "Yule" ladhihirisha zaidi jamba fulani lililapa kweli .. Kufuatana na sarufi ya lugha hiya nena lile limtajala huya anenwaye lafuatwa na 'Yule', lakini lile lizungumzwala tu halina nena lile 'Yule'. Mara nyingi latakea katika Nyaraka - likimtaja Kristo, Yule wa kiraha, Kile Kichwa, Ule Mwili." Mt. 1:1; 2:4; 2:11; 2:16.

2. Yesu - Easous - kwa lugha ya Kiebrania ni lile lile kama Jashua, au Jehashua, katika LXX (Septuaginta) na A. J. nena hila likiwa Yesu. Nena lile la Kiebrania "Joshua" lajumlisha manena mawili: Jeh. (Jehsual) na "Kuakaa", nena la Jehovah maana yake ikiwa Mwokozi. Latumika kwa Kristo, sababu ye ye ndiye Mungu awezaye "kuwaakaa wanadamu kutaka kwa dhambi zao." Yesu ni jina la unyenyekevu wake; ni jina la mtu wa huzuni - alikufa akainuliwa tena Kristo limekuwa jina la kuwa yule aliyeinuliwa "juu ya yate". Kwa hiyo yamesemwa kwamba tumo "ndani ya Kristo", siyo "ndani ya Yesu".

"Yule Kristo"- (pamaja na nena 'lile "Yule"), ni jina rasmi la yule aliyetalewa mbele ya Waisraeli akiwa tayari kuwabariki. Katika Injili (ziliza na habari za "maisha" ya Yesu hapa duniani) neno lile "Yesu" latokea mara 566, neno la "Krista" likitokea mara 36. Katitka kitabu cha Matendo ya Mitume na vitabu vifuatavyo, neno lile "Kristo" latokea mara 217, neno la "Yesu" likitakea mara 29 tu (yaani mara 16 katika kitabu cha Matendo ya Mitume, likiwa ushuhuda wa Yesu pamoja na Kristo).

Manena hayo mawili yanayaungwa pamoja "Yesu Kristo" yaanekana kudhihirisha kwamba Yesu alikuwa amenyenyekewa lakini sasa ametukuzwa; jina la "Kristo Yesu" likidhihirishwa kwamba sasa ametukuzwa lakini zamani alikuwa amenyenyekewa. Manena haya "Bwana Yesu Kristo" yataja mamlaka na nguvu yake kama Bwana (Mdo. 2:36).

3. Mwana - wios, kumweleza ye yate habari za asili na hali yake zilivyo, yaani mambo yale yakinishaya mtinda na tabia zake.

Mwana wa Mungu - (bila "yule") jina hila latumika kwa Kristo na kwa watu vilevile kwa kuanyesha uhusiano kati ya Mungu akiwa na upenda wa kuchagua, na mwanadamu. Maisha na tabia zimetakana na yule Mjengaji Mkuu-Mungu. Jina hila likimtaja Kristo, lahusika na tendo lile la Mungu la kumweka Kristo katika uhusiana huo, yaani kuzaliwa kwake, Lk. 1:35; Mdo. 13:33; Rum. 1:4, Mdo. 2:32, 36.

4. "Yule Mwana wa Mungu-(pamoja na "yule"), ni uhusiana wa pekee ambaa mwanadamu hawezi kuusimika. Yamta Kristo kuwa Masihi ambaye uhusiana wetu kama "wana wa Mungu" wamtegemea.

5. Mwana wa Adamu-jina hili laanyesha utu wake, yaani mamba yale yanayamhusu mwanadamu hasa. Wanafunzi hawakutumia jina hila mpaka Mdo. 7:56. Kwa jina hila Yesu alikuwa ametalewa kutaka kwa jamii ile ya kawaida ya

- "wana wa wanadamu", akatiwa katika milki ya Kimasihi, Yesu akijiweka mwe-nyewe mionganini mwa wana wa Adamu (kama uzaa wa ahadi wa Mwanamke).
6. Mwana wa Baba - jina la heshima litajalo umoja ule unaofurahiwa na Kristo pamoja na Baba katika uungu wao.
  7. Mwana wa Yule aliye Juu - cheo cha mamlaka ya Mungu kinachoelekeza mfalme aliyetiwa mafuta, 2 Sam. 7:14; Zab. 2:7; 89:28; Mk. 5:7.
  8. Mwana wa Mtukufu - jina hila lilitumika kwa njia ya unafiki ili kuonyesha kwamba Yesu alitoa kufuru ya Mungu alipokubali kudai jina hila - Mtukufu. Mk. 14:61.
  9. Mwana wa Daudi - Yesu ndiye aliyerithi kitii cha enzi cha Daudi na kuwa mrithi wa ahadi zile Daudi alizopewa, Lk. 1:32.
  10. Bwana - Kyrios --- Mkuu, mtawala (mwenye haki au au mwenye nguvu). Jina hilo latumika kwa mtu mwenyewe, Mkuu; katika Injili Jina hila "Bwana" kwa kawaida hutumika kwa Jehovah, lakini katika Nyaraka hutumika kwa Kristo, liileza cheo chake cha kuwa Mkuu wa watu wake, kumiliki na mamlaka yake, Kol. 3:16.

Bwana - despotace - "Mmoja aliye na utawala mkubwa kabisa, mamlaka makuu, na nguvu kamili, zitokazo kutoka kwa kumiliki kwake; au ni Mkuu aliye ni tofauti sana na mtumishi, 1 Tim. 6:1-2; Ufu. 6:10; 2 Pet. 2:1; Mdo. 4:24.

Bwana - Rabbini - ni ya hesshima kubwa zaidi kuliko Rabbi, maana yake ni Mkuu wangu kabisa (Watu wale saba wa shule ya Hillel walipewa jina hilo rasmi, ni la utukufu mkuu), Mk. 10:51.

Kuna zaidi ya majina 150 ya Yesu Kristo - (Hii ingekuwa somo lingine la pekee.)

### III. YESU ALIKUJA DUNIANI - KUFANYIKA KWAKE . MWILI: Yoh. 1:14

A. Yosefu alikuwa akiongoza pundakutoka Nazareti mpaka Bethlehemu ambaye Mariamu alikuwa amepanda juu yake akiwa na mimba.

1. Hapakuwa na nafasi katika nyumba ya wageni. Kama Yosefu angalikuwa liwali, n.k. pangalikuwa na nafasi. Lakini alikmva seremala.
2. Wakati fulani wa usiku Mungu alishuka akamzalisha Mariamu. Akamzaa mwana asiyekuwa na baba. Mwana alikuwa mzee kuliko mama. Mwana alichukua sura ya mwanadamu akawa mwanadamu duniani ambaye hakuwa katika ufalme wa milele.

B. Yesu alikuja katika utimilifu wa wakati. Gal. 4:4.

1. Wakati wa kituo katika vita; wakati watu wa mji wa Athene walipokuwa wameelewa uzito wa filosofia yao iliyojaa mashaka (skepticism).
2. Wakati watu wa nchi ya Uhindi walipoota ndoto ya Buddha, na wakati alama ya masongo ya mazishi ilipokuwa imewekwa juu ya nchi ya Uajemi.
3. Wakati mji wa Rumi ulipokuwa umeandaa ulimwengu katika mambo ya kimwili, maadili, utawala na utaratibu - YESU ALIKUJA.

C. Yesu alikuwa Ufunuo wa Mungu. Yn. 1:8. "Mwana wa pekee amemtangaza baba ...." Yn. 14:9 "Aliyeniona mimi - amemwona Baba."

1. Kumjua Kristo ni kumjua Mungu. "Yeye ndiye aliye kuwa akili ya Mungu akiwa akifikiri; moyo wa Mungu akipumia; mikono ya Mungu akitoa; macho ya Mungu akiona."
2. Sisi tungependa kujua ulimwengu unakwendapi, lakini yatupasa kuhubiri nani aliye akiujia ulimwengu.

D. Wengi hawakumpokea, kwa sababu alikuwa tofauti na matumaini yao.

1. Kama Naamini walikuwa WAMEFIKIRI.
2. Wayahudi walidhani kwamba wamekwisha fikiria. Walifikiri kwamba atakuwa Masihi wa kisiasa. Wengine walifikiri kwamba atakuwa "Masihiwa kieskatologia." (Kuja kwake kungeleta mwisho wa ulimwengu).
3. Yesu alikuwa tofauti.
4. Yesu mara nyangi ni tofauti na matumaini yetu tuliyio nayo juu yake - "Nilikuja kutumika," Mt. 20:28.

#### IV. YESU ALIKUWA MTUMISHI:

- A. "Kwa maana Mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi." Mk. 10:45.
- B. Hatukufahamu wazo hilo la kuwa mtumishi; ujiulize, "Je, mimi ni mtumishi?" Yn. 13.
- C. Katika Kanisa la Charlotte Ave. katika mji wa Nashville kulikuwa na mukutano mkubwa wa wasikilizaji wengi. Uchaguzi wa mhubiri ulikuwa kati ya wawili - Bw. Clay Pullias na Bw. N. B. Hardeman. Bw. Hardeman alikuwa ametakwa zaidi, lakini Bw. Pullias alitakwa kuongoza nyimbo. Pullias akajibu: "Kwa ajili ya faida ya mukutano huu ningekuwa tayari hata kufagia chumbs; hiki."
- D. Yesu ni mtumishi na MWOKOZI. Cheo kile cha "Bwana" ni kikuu kati ya vyeo vyote vyta kidini. Utendaji wa ukombozi wa Mungu ulionyeshwa wazi kabisa katika Yesu na katika kanisa lililoumbwa naye.

#### V. YESU ALIKUFA AKAFUFUKA:

A. Ufufuo wa Yesu Kristo mwenyewe huelezwa mara 104 au zaidi katika A. J. "Kama Kristo hakufufuka - Y ote yangalipotea!"

1. R. A. Torrey alielekeai kusema, "Kama ufufuo wa mwili wa Yesu Kristo ni jiwe la pembedi la mafundisho ya Kikristo, ni vilevile kama Gibraltar ya ushuhuda wa Kikristo, na ni Waterloo ya kutokuwa na imani na kufuata akili za binadamu tu.
2. "Kama Kristo hakufufuka," 1 Kor. 15:12-19, basi:
  - a. "Kuhubiri kwetu ni bure," 1 Kor. 15:1-4.
  - b. "Tumepata mashahidi wa uongo wa Mungu," Mdo. 2:24; 2:32; 3:13-15; 4:33; 17:30, 31.
  - c. "Imani yenu ni bure," Mt. 12:38-40, Rum. 5:1-2.
  - d. "Mngalimo katika dhambi zenu," Mt. 26:28.
  - e. "Na hapo wao nao waliolala katika Kristo wamepotea," Ebr. 11:1; 1 Pet. 1:20-21.

## B. Ushuhuda wa Ufufuo.

Nguvu ya ushuhuda wa watu hutegemea mambo matatu : wao; ustadi wao; idadi yao.

### 1. Tuufikirie uaminifu wao.

- a. Usemi wao. Wasema bila kupendelea.
- b. Uadilifu wao. Hawaogopi kutaja mambo mengi ambayo ni aibu yao wenyewe.
- c. Mateso yao. Walivumilia matokeo ya maneno yao.
- d. Nia zao. Woga, tamaa za mali, wala tamaa za cheo haziwezi kuwa nia za watu hawa.

Kwa hiyo twaona kwamba mashahidi walikuwa waminifu.

### 2. Tuufikirie ustadi wao. Huu wategemea nafasi zao za kupata ujuzi na uwezo wao wa akili wa kukumbuka mambo.

- a. Walikuwa pamoja na Yesu tangu ubatizo wake, Mdo. 1:21-22.
- b. Walikuwa wenye ustadi. Miiongoni mwao walikuwa watu kama watoza ushuru, mtaalamu mmoja, mganga mmoja na wafanyakazi. Hawakutaja mambo madogo madogo kwa wingi, ling. Yn. 20:7. Hawakuwa wepesi kwa kuamini, Mk. 9:30-32; Lk. 24:25; Mk. 16:9.

### 3. Idadi yao. Mashahidi wawili wana nguvu zaidi kuliko mmoja, watatu kuliko wawili n.k. Lakini ipo idadi fulani ambayo hatuna haja ya kuwa na zaidi. 1 Kof. 15:6 yasemekana kwamba Kristo aliwatokea "ndugu zaidi ya mia tano pamoja."

C. "Wanafunzi waliokuwa wamebadilika" wa ushuhuda wa Ufufuo. Yn. 21:3, "Naenda kuvua samaki", lakini baada ya ufufuo ilikuwa ya tofauti. Mdo. 2:14; 3:13-15; 4:8-13; 5:28~32. Maelezo ya Petro, ufufuo wa Kristo. 1 Pet. 1:3-5.

### D. Mashahidi wa mambo mbalimbali ya Kikristo.

1. Kanisa lipo! - lakini lasimama juu ya Uungu wa Kristo, Mt. 12:39-40; 16:13-20.
2. Biblia ipo! Kristo, Kanisa, baadaye Kitabu. Kitabu hicho ni mazao ya Kanisa ambalo ni mazao ya Ufufuo. Utungaji wa kitabu kama hicho ambacho kisingekuwa na ukweli ungekuwa ajabu kubwa kuliko Ufufuo.
3. Siku ya Bwana ipo! Lakini siku hii ina maana tu kama Kristo amefufuka! Mdo. 20:7, Ufu. 1:10.
4. Chakula cha Bwana kipo! Lakini chafahamika tu katika nuru ya Ufufuo. 1 Kor. 11:26.
5. Ubatizo wa Kikristo upo! Hata huu umetiwa nanga ndani ya Ufufuo. Rum. 6:3-4. Ulikuwa ushuhuda wa Ufufuo uliowafanyiza watu elfu wabatizwe siku ile ya kwanza ambayo Injili ilikuwa imehubiriwa, Mdo. 2:41.

Neno la kuangaliwa: Kwa hiyo twaona kwamba Yesu Kristo amefufuka kutoka kwa wafu; alikuwa Mwana wa Mungu, jinsi alivyosema.

## VI. MAFUNDISHO YA UONGO JUU YA KRISTO, MWANA WA MUNGU, NA UFUFUO WAKE

### A. Mafundisho ya Mashahidi wa Jehovah (Jehovah Witness)

1. "Wakati ule (kabla ya kufanyika mwili) na nyakati zilizofuata, yeye (Kristo) pengine alijulikana kuwa "mungu fulani" - mwenye nguvu ..... Kwa sababu yeye (Kristo) alikuwa kiumbe cha juu cha viumbe vyote vya Jehovah, alikuwa kiumbe cha kwanza cha Mungu vilevile, kiumbe cha pekee; na baadaye yeye (Kristo) akishika mahali pa Jehovah, akitumia mamlaka ya Jehovah, na katika jina lake, alivumba vitu vyote ... " (Maneno katika vifungo yametiwa na mwandishi, AM.C.). Studies in the Scriptures, Chas. Taze Russell, Kit. V, uk. 84.
2. Yesu ni mungu fulani, lakini siyo Mungu kama Jehovah; taz. kitabu kile kile uk. 55, 84, 134.
3. Kama Jehovah na Kristo mfu wangalikuwa mmoja katika nafsi yao, ufuluko haungaliwezekana. Taz Let God Be True, .. uk. 91-92.
4. Kwa hiyo yaonekana wazi kwamba Shetani ndiye aliyeunda "Mafundisho ya Utatu," taz: kitabu kile kile, uk. 82.
5. Kama Yesu angekuwa Mungu, basi wakati Yesu alikuwa amekufa, Mungu angalikufa, angalikuwa katika kaburi; taz. kitabu kile kile, uk. 91.
6. Yesu alikufa 'kama mwanadamu, lakini amefufuka kutoka kwa wafu kama roho, akiwa katika cheo cha juu cha hali cha kiungu .... Yesu kama mwanadamu amekufa, amekufa kwa milele. Studies in the, Scriptures, uk. 453, 454.
7. Hakuna mtu ajuaye, kwamba ule (mwili wa Yesu, AM.C.) umeyeyushwa kuwa hewa ya aina fulani, au kwamba bado unashikwa mahali fulani kuwa kumbukumbu kuu la upendo wa Mungu, utii wa Yesu, na ukombozi. Kitabu kile kile, uk. 127.
8. "Fidia ya wote" iliyotolewa na "Kristo Yesu kama mwanadamu" haitoi wala haihakikishi maisha ya milele wala mbaraka kwa mtu ye yote; lakini huhakikisha kwa kila mtu nafasi na jaribio la maisha ya milele. The Harp of God, J. F. Rutherford, uk. 170.

B. Umormoni - "Joseph Smith alifundisha kwamba kuna dhambi fulani kubwa mno kiasi hiki kwamba zitamweka yule aliyezifanya nje ya Uweza na Upatanisho wa Kristo. Kama dhambi za aina hiyo zimefanyika, damu ya Kristo haitawasafisha wale kutoka kwa dhambi zao, hata kama wakitubu; kwa hiyo tumaini lao la pekee ndilo hilo kwamba damu zao zimwagike kuwa malipo ya ukosefu, jinsi iwezekanavyo kwa ajili yao wenywewe .....

1. "Kwa ajili ya makosa fulani, lazima watu walipie ukosefu wao jinsi wanavyoweza, kwa sababu warnejiwcka nje ya uweza wa upatanisho wa damu ya Kristo." Doctrines of Salvation, Kit. I, uk. 135-136.
2. Brigham Young, Rais wa pili wa Kanisa la Kimormoni alisema: "Kuna dhambi fulani zifanyikazo na watu ambazo watu hawawezi kupewa msamaha kwa dhambi hizo katika ulimwengu huu wala katika ulimwengu ujao, na kama watu hao wakifumbua macho kuona hali yao ilivyo kweli,

wangekuwa tayari kabisa damu zao zimwagike ardhini, ili moshi wake upande mbinguni, kama malipo ya dhambi zao; na uvumba wa moshi huu ulipie makosa yao, "Journal of Discourses, Kit. 4, uk. 53-54.

3. Joseph Fielding Smith Jr. alisema: "Kuzaliwa kwake Mwokozi kulikuwa tokeo la kimwili tu bila cheo cho chote cha kidini, na Baba Mungu alikuwa mzazi has a Yesu kwa njia ya kimwili na ya kiroho." Religious Truths Defined, uk. 44.

4. Tena, "Kristo alizaliwa kutoka kwa Mungu, hakuzaliwa bila msaada wa mtu, na mtu huyu alikuwa Mungu." kitabu kile kile, I, uk. 18.

5. Brigham Young alisema, "Jinsi tujuavyo, yule mtu Yosefu, mume wake Mariamu, hakuwa na zaidi ya mke mmoja, lakini Mariamu, mke wake Yosefu, alikuwa na mume mwengine," The Desert News, Okt. 10, 1966.

6. Tena Brigham Young alieleza: "Kuzaliwa kwake Mwokozi kulikuwa jambo la kimwili kama kuzaliwa kwa watoto wetu; kulikuwa tokeo la kitendo cha kimwili; Yesu alishiriki mwili na damu - alizaliwa kutoka kwa Baba yake, kama sisi tumezaliwa kutoka kwa baba zetu." Journal of Discourses, Kit. 8, uk. 115.

**Neno la kuangaliwa:** Uchunguzi maalum wa maneno ya hapo juu utaonyesha kwa kila mtu kwamba maneno hayo yakana kabisa mafundisho ya Biblia, ten a ni maneno ya upagani zaidi kuliko ya Ukristo.

C. Ukatoliki - "K wa njia ya kubarikiwa kwa mkate na divai, tabia nzima ya mkate hubadilika kuwa tabia ya Mwili wa Kristo risto Bwaa wetu, na tabia nzima ya divai hubadilika kuwa damu yake: Kanisa Takatifu Katoliki huita mabadiliko hayo kuwa Kugeuka kwa asili (transubstantiation) .

"Kwa maneno hayo Mkutano wa Halmashauri ililaumu fundisho la Kilutheri la Tabia zilizo Pamoja (consubstantion), kwamba tabia ya mkate na ile ya Mwili wa Kristo zikae pamoja (Grisar, Luther; 1, 162; 111, 320; 111, 380; mst. 463; fundisho la Kicalvinistic la kuwako kwa kweli na kwa uwezo, mwili na damu za Kristo zikishirikiwa kutoka kwa mbinguni na nafsi za wale waliochaguliwa (Instit., IV., 27); na fundisho la Kizwingli kwamba Chakula cha Bwana ni ukumbusho tu (Opera, 111, 240).

"Maneno ya kuanzisha, 'Huu ndio mwili wangu', maana yao ndiyo kwamba kile ambacho Kristo alikuwa nacho mikononi mwake kimekoma kuwa mkate, bali kimekuwa mwili. Kwa sababu hakuwa na mabadiliko ya tabia wala ya sura za mkate na divai, lazima mabadiliko yalikuwa yale ambayo Kanisa lataja Kugeuka kwa asili (transubstantiation).

"Mt. Cyril aliandika: 'Ikiwa ni sakramenti itoayo uhai, tunayo Mwili mtukufu wa Kristo na Damu yake ya thamani katika sura za mkate na divai'" (Katitka Luc. XXII, 19). "Ambayo yaonekana kuwa mkate, siyo mkate, baJi mwili wa Kristo; ambayo yaonekana kuwa divai, siyo divai, bali damu ya Kristo." (Cath. IV. 9).

"Liturgia zote za zamani, zile za Mashariki na zile za Magharibi pia, hufundisha kule Kugeuka kwa asili. Sala ifuatayo ni kutoka liturgia ya Mt. Basil: 'Fanya mkate huu kuwa Mwili wa thamani wa Bwana wetu na Mungu na Mwokozi Yesu Kristo, na kikombe hiki kuwa damu ya Bwana wetu na Mungu na Mwokozi Yesu Kristo, iliyomwagika kwa ajili ya uhai wa ulimwengu' (Phole, The Sacraments, 11, 22). The Question Box, na Bertrand L. Conway, C. S.P. (Andiko rasmi la Kanisa la Kirumi la Kikatoliki, likiwa na dibaji ilioandikwa na Kardinale Gibbons).

#### AZIMIO:

Yesu Kristo ndiye Mkuu kabisa katika historia ya wanadamu. "Hapo pana mtu aliyezaliwa katika kijiji kisicho julkana sana, tena kilikuwa kimedharauliwa. Alifanya kazi katika duka la seremala kwa muda wa miaka thelathini, baadaye akawa mhubiri mtembezi kwa mud a wa miaka mitatu. Hakuandika kitabu cho chote. Hakushika afisi yo yote. Hakuwa mwenye nyumba. Hakuwa na mke wala watoto. Hakusoma shule ya juu. Hakuingia mji wo wote uliokuwa mkubwa sana. Hakusafiri zaidi ya maili 200 kutoka mahali pa kuzaliwa kwake, isipokuwa wakati alipokuwa mtoto mchanga. Hakuwa na cheo cho chote, isipokuwa nafsi yake mwenyewe.

"Wakati alipokuwa mtu mzima, maoni ya watu yalikuwa yakipambana naye. Rafiki zake walikimbia. Mmojawapo alimsaliti. Alitiwa katika mikono ya maadui wake. Aliwekwa chini ya mzaha wa hukumu. Alipigiliwa misumari msalabani kati ya wezi wawili. Wanyongaji wake waliipigia kura mati yake ya pekee aliyokuwa nayo duniani, yaani kanzu yake isiyoshonwa. Alipokuwa amekufa, ameondolewa kutoka msalabani akawekwa ndani ya kaburi lililokuwa limekopeshwa kwa ukarimu wa rafiki mmoja. Kame 19 zimekuja zikaenda, na lea Yesu yupo katikati has a ya ujamaa wa wanadamu wote, tena ni kiongozi wa maendeleo yote ya binadamu.

"Siongezi sifa kupita kiasi nikisema kwamba majeshi yote ya maaskari yaliyokuwapo mpaka sasa, vyombo vyote vya bahari vilivyojengwa kwa vita, mabunge yote yaliyokutana, na wafalme wote waliotawala wakati wo wote, hao wote wakiwekwa pamoa hawakugeuza maisha ya wanadamu duniani kiasi hicho kama Yule mmoja wa pekee ameyageuza.

"Nyakati zote hunesabiwa kufuatana na kuzaliwa kwake, tena haiwezekani kufahamu wala kueleza maendeleo yajamii ya watu katika taifa 10 lote la dunia bila maongozi yake. Katika mwenendo wa nyakati watu wameanza kufahamu polepole kwamba haja ya kwanza katika ulimwengu huu siyo maji, chuma, dhahabu, chakula, nguo, wala mawe ya kuchimbiliwa chini ya nchi, bali Kristo aliywekwa ndani ya mioyo, mawazo, na nia za wanadamu."

Mwandishi hajulikani

## **MAANDIKO MATAKATIFU NI YENYE "PUMZI YA MUNGU"**

INGIZO:

A. Neno lile "kuvuta pumzi" limeondolewa kutoka kwa tafsiri mpya za Biblia. Katika K.J.V. (King James Version) lilikuwa limetokea mara mbili, yaani Ayu. 32:8; 2 Tim. 3:16. Katika Revised Version lilitokea mara moja tu, yaani katika mstari ule wa pili.

1. Neno la asili ni "theopneustos", na maana yake ndiyo "lenye pumzi ya Mungu," jinsi tusemavyo kwa kawaida.
2. Maana yake hasa ni, "limetoka kwa pumzi ya Mungu." Kwa maneno mengine, ni mazao ya kiungu zaidi kuliko Mungu alikivutia pumzi kitu fulani ambacho kilikuwa kimekwisha kuwapo. Maandiko ni matokeo ya "pumzi ya Mungu". Taz. Zab. 33:6, ambapo "mbingu zilifanyika kwa pumzi ya kinywa chake Mungu."
3. Kwa sababu Maandiko ni matokeo ya mvuto wa Mungu kutoka juu uliotiliwa ndani ya waandishi wa Biblia, kwa hiyo ni yenyewe uaminifu wa kiungu, taz. 2 Pet. 1:19-20.

B. Kama neno 10 lote lingekatwa kutoka kwa yale yaliyosemwa hapo juu, Maandiko yanepoteza uaminifu wao usio na makosa, na Mkristo asingeweza kuyategemea tena Maandiko kama kiongozi wake kamili katika mambo ya kidini.

I. HAKI YA BIBLIA KUHUSU UPUZIO WA KILA NENO:

Neno la kuangaliwa:

Kwa muda wa karne zote zilizopita watu fulani walijaribu kubadilisha wazo lile la Upuzio kamili wa kila neno katika Biblia. Lakini ubadilisho wo wote hukatazwa kwa akili halisi na kwa Maandiko yenyewe. Kama Shetani akiweza kuiharibu imani yetu kwa maneno hasa, ushindi mkuu umekwisha patikana! "Upuzio kamili", maana yake ndiyo kwamba yote yamewekwa sawa katika Biblia chini ya uongozi wa Mungu, ama kwa ufufuo mpya au kwa kutiwa ndani (kama hati ya nasaba, n.k.). Upuzio wa kila neno ndio njia ile moja hasa iwezekanayo - kwa njia ya maneno twajua mawazo." The New Smiths Bible Dictionary, uk. 158.

A. Maandiko yanadai kuitwa "yenye pumzi ya Mungu" mazao ya kiungu.

1. 2 Tim. 3:16

Mst. 15 huzungumza juu ya "maandiko matakatifu". Neno hilo ni neno la pekee lisilotokea tena katika A. J. Lakini katika maandiko ya Josephus na Philo, neno hilo limetumika kutaja jumla ya maandiko rasmi yaliyokuwa Sheria za Kiyahudi. Maana yake hapa ndiyo hiyo kwamba, "kila andiko, lenye 'pumzi ya Mungu', lafaa." Tafsiri za baadaye zae1eza zaidi wazo lile lile. Paulo ameweka maandiko yake kati ya 'maandiko matakatifu, yenyewe pumzi ya Mungu.'

2. 2 Pet. 1:19-20

Mistari hii ni yenye nguvu sana katika yote yahusuyo Neno la Mungu ikionyesha haki ya upuzio wa kila neno. Mistari hii yae1eza wazi zaidi kwamba Neno la Mungu haliku1etwa "kwa mapenzi ya mwanadamu", wala halipati "kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani", bali "wanadamu walinenya yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu." Hiyo ndiyo sababu kwamba "neno" ni "imara". "Imara", maana yake ni "thabit", aminifu, ya hakika; tunalo neno la unabii kama kitu ambacho twaweza kukitegemea." uk. 137, Greek English Lexicon of The N. T., Arndt na Gingrich. Un. of Chicago Press.

Ushuhuda imara zaidi kutoka kwa neno hauhitajiki. Swali moja lingine ambalo lazima mwanadamu alijibu, ndilo hilo - Je waamini kwamba Maandiko ni yenye uaminifu?

3. Yn. 10:34-35

Yesu alichagua neno kutoka Zab. 82:6. Neno hilo halitoki Vitabu vile vitano vya mwanzo wa Biblia (Pentateuch) wala kitabu cho chote kingine cha Torati. Hata hivyo alisema, "Je! haikuandikwa katika torati yenu"; hii yaonyesha kwamba Yesu alihesabia Maandiko yote madaraka ya kisheria (Torati). Paulo a1ifanya vivyo hivyo 1 Kor. 14:21 na Rum. 3.19, aki-chagua neno kutoka Isaya na Zaburi. Yesu alisema pia, "maandiko hayawezi kutanguka," maana yake, "kubatilishwa, kufutwa, kuondolewa," Kitabu kile kile, uk. 485. Kwa hiyo madaraka yake hayawezi kukatazwa wala kukanushwa.

"Ni lazima ifahamike kwamba Mt. Yohana aliandika juu ya A. K. lenye maana ya kudumu ... " The Gospel According to St. John, na B. F. Westcott, uk. 160. Jinsi nijuavyo, hii ndiyo maana ya mistari hiyo.

4. Maneno yaliyosemwa na watu mashuhuri :

" .... tusifikiri kwamba lugha ya watu wale wenye pumzi ya Mungu yatangulia, bali ni Neno la Kiungu liwaongozalo." Justin Martyr.

"Lo lote Maandiko ya Kiungu yasemalo, ndilo sauti ya Roho Mtakatifu". Gregory wa Nyasa.

"Kwa hiyo twaungama na kuyakubali madaraka ya Maandiko Matakatifu ambayo hayawezi kudanganywa wala kudanganya." Augustino.

5. Waandishi wa A. J. wasema juu ya Maandiko kwa namna ile ile kama Kristo alivyosema. Mk. 1:2 "Ilivyoandikwa". Taz. Mt. 4:4; 4:7; 4:10; Lk. 24:44; tena, 1 Kor. 15:3-4; Mdo. 8:35; 17:3; 26:22; Rum. 1:17; 3:4; 3:10.

#### AZIMIO:

Kristo na waandishi wa A. J. vilevile wa1ifundisha kwamba Maandiko ni ya kushurutisha na yenye madaraka. Waliwaamsha watuwayachunguze maandiko, Yn. 5:39; Mdo. 17:11, wakaamini kwamba 1azima yote yatimizwe, Mk. 14:49; Yn. 13:18, 17:12, na kwamba

lazima mambo fulani yatokee, "kwa kuwa imeandikwa", Mt. 26:31; Mk. 14:27. Sababu yake ndiyo ya kuwa waliamini kwamba Maandiko ni Nena Tukufu la Mungu.

## II. UPULIZO WA KILA NENO HURUHUSU UTUMI WA BINADAMU:

A. Mara nyingi Maandiko yenyewe hudhihirisha kwamba Mungu ametumia watu kwa kupasha ujumbe wake kwa wanadamu.

1. 2 Pet. 1:21 "wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu .... "
2. Mk. 12:36 "Daudi mwenyewe alisema .... "
3. Mdo. 1:16 "kwa kinywa cha Daudi .... "

B. Ingawa la utumi wa binadamu, utawala wa Roho Mtakatifu hukubaliwa:

1. 2 Pet. 1:21 "wakiongozwana Roho Mtakatifu".
2. Mk. 12:36 Daudi alisema, "kwa uweza wa Roho Mtakatifu."
3. Mdo. 1:16 "Alilolinena Roho Mtakatifu zamani kwa kinywa cha Daudi." Kwa hiyo utawala wa Roho Mtakatifu ulikuwa mkubwa, kamili na mtimilifu kiasi hiki kwamba haukuwaruhusu waandishi wa binadamu kushawishi kwa njia yo yote ubora wala sura yao ya mwisho. Neno la "imla" halifai kuwasilisha vizuri wazo lile Ia Upuzio wa Biblia.

C. Maneno halisi ya Maandiko yamefahamika kuwa yametoka kwa Mungu. Utumiaji wa maneno halisi huonyesha kwamba utumiaji huo una maana. Taz. Gal. 3:16. Haja kubwa kutoka kwa idadi ya jina la kitu fulani; taz. "mmea" na "mmea". Tazama hoja itokeayo kwa hali ya wakati wa neno fulani, Mt. 22:32. Tazama hoja itokeayo kwa neno moja la pekee, Mt. 22:43. Kama ukikana wazo lile kwamba Mungu ametia pumzi yake kwa kila neno la Maandiko, basi huwezi. kuamini kwa kweli lolote lilosemekana katika Biblia! Yaani ni maneno yawasilishayo mawazo. Upuzio wa mawazo hauwezi kuwa bila upuzio wa maneno.

D. Maneno yaliyosemwa na watu mashuhuri:

"Hatuwezi kusema juu ya Maandiko ya Roho Mtakatifu kwamba lo lote ni bure au halifai, hata kama yanaonekana yakijificha na wengine." Origen.

"Maandiko yote jinsi tulivyopewa na Mungu yanaonekana yakipatana." Irenalus.

E. Majaliwa na Upuzio. Wengi waona kwamba mafundisho hayo (A. B. na C.) ya upuzio hayatoi nafasi kwa utumi wa wanadamu. Lakini hiyo siyo, kwa sababu kuna tofauti ya binadarilU katika waandishi mbalimbali. Mungu aliwaandaa watu hao kwa kusudi i1i watumike hivyo. Soma kwa uangalifu, Gal. 1:15-16. Mungu hakuuandaa wakati tu kwa ufunuo wa Yesu Kristo, bali Mungu aliwaandaa wanadamu vilevile! Na yote aliyatumia kwa kusudi lake. Jina la Bwana lisifiwe!

"Twaambiwa kwamba, kama nuru ile ipitayo kioo cha rangi katika dirisha kanisani, ndiyo nuru kutoka mbinguni ikitiwa rangi ya kioo ambacho yapita, hivyo ndivyo kila neno la Mungu lipitishwalo akili na nafsi ya mwanadamu latoka lenye rangi nyingine kufuatana na nafsi ile iliyopitishwa, na kiasi hiki limepunguka kuwa neno kamili la Mungu. Lakini kama nafsi hiyo yenyewe imeumbwa na Mungu kuwa nafsi hiyo hiyo, kwa kusudi has a ishirikiane na neno

lile rangi ile ile ambayo limetiwa? Au, kama rangi za dirisha lile lenye kioo zimerekebishwa na mjengaji kwa kusudi hasa ziivishe nuru ile iliyojaa kanisani hali na tabia ile ile itiwayo nazo? Au, kama Neno la Mungu, linalowakaribia wanadamu, limetungwa kuwa neno liIe lile la Mungu lililo, likitungwa na Mungu kwa njia ya tabia za wanadamu, kwa kusudi hasa ambalo limetolewa kwalo?" Benjamin B.. Warfield, uk. 64, Thy Word Is Truth, na Ed. J. Young.

### III. UHAFIFU W A SIKU HUDHOOFISHA FUNDISHO LA BIBLIA LA UPUZIO:

A. Uhafifu wa siku hizi na upuzio. Uhafifu wa Biblia wa siku hizi, ambao idadi na namna zake ni nyingi mno, hujaribu kutahayarisha wazo lile la Biblia la upuzio.  
B. Mara nyingi hujaribu kutenga Kristo na Mitume katika mafundisho yao. Kristo alifaundisha waandisho wa A. J. tu, na Mitme walisema kwa mamlaka yake. Taz. Yn. 13:20. Tena, Yn. 14:16-20; 16:13-15. Ye yote asomaye mistari hiyo amefahamu kwamba watu hawa walisema jinsi Mungu alivyowaongoza kwa Roho Mtakatifu. Hakuna maelezo mengine yaliyo yamefuata Biblia.  
C. Uhafifu wa siku hizi hujaribu kutllhayarisha andiko lenyewe ili watuharibu imani yetu tuliyo nayo na uaminifu wake. Wataalamu wa kweli, waliotolea maisha yao yote kwa uchunguzi, husema, "kadiri ya maneno, yakubaliwayo na wote ikiwa hayana mashaka, ni kubwa sana; yaani kadiri hii siyo chini ya sehemu saba kwa nane. Sehemu ile ya nane inayobaki, ikiwa na mabadiliko wa utaratibu na mambo mengine madogo madogo tu, ndiyo ambayo inashughulikiwa na uhafifu wa siku hizi ... kadiri yenye tofauti za maana yo yote ... siyo zaidi ya sehemu moja kwa elfu moja katika andiko zima." Dr. F. J. A. Hart, The N. T. in the Original Greek, uk. 2. Maana yake ndiyokwamba ni chini ya nusu ya ukurasa mmoja katika A. J. lako ambayo huleta mashaka kidogo. Mungu ndiye mwenye nguvu kweli! Kwa hiyo twaweza kusema pamoja na Sir Frederic Kenyon, "Mkristo aweza kushika Biblia nzima mkononi mwake akisema bila woga na wasiwasi ya kwamba ashika ndani yake Neno la kweli la Mungu lililokabidhiwa bila hasara yenye maana, kizazi kwa kizazi kwa kame nyingi zilizopita." uk. 23, Our Bible and the Ancient Manuscripts. Lililosemwa juu ya A. J., ndilo lenye ukweli katika A. K. vilevile. Hati zile ndefu zenye maandiko zilizoonekana juzi tu huko kwenye Bahari ya Chumvi zimesaidia sana kuhakikisha uaminifu wa Maandiko ya Biblia tuliyo nayo mpaka leo. Mungu tena na tena huthibitisha nia ya Wakristo wake, akiifanya sepeto ya mtaalamu wa mambo ya kale ifunue mahakikisho zaidi katika wakati mwema wa Baba.

## **MAMLAKA NA KUFAA BIBLIA ZISIWE ZENYE MASHAKA:**

SOMO: Mt. 21:23-27; 15:1-9

INGIZO :

A. Swali lile lihusulo mamlaka ndilo lenye msingi mahali po pote - hata katika mambo ya dini.

1. Jaribu kufikiria Kampuni ya General Motors Corporation bila mfano ule kamili wa mamlaka.
2. Jaribu kufikiria Jeshi la Anga la Amerika bila mfano ule kamili wa mamlaka.
3. Jaribu kufikiria Serikali yetu ya Mambo ya Ndani bila mfano ule kamili wa mamlaka.
  - a. Katika mambo ya Kutunga Sheria.
  - b. Katika mambo ya Hukumu.
  - c. Katika mambo ya Utawala.

B. Umoja kati ya Wakristo waaminifu kwa kweli ndio shabaha ambayo yastahili tuilenge.

1. Yesu aliuombea - Yn. 17.
2. Paulo aliushika sana akiulaumu mgawanyiko - 1 Kor. 1:10-13.
3. Paulo pia alieleza jinsi umoja huo unavyopatikana.
4. Lakini umoja huo haupatikani isipokuwa wote wakubali mamlaka yale yale yenye ukweli.

### **I. MAMLAKA NI NINI? TUYAELEZAJE?**

- A. Webster: "" .. haki ya kutoa amri na kutenda
- B. Niongeze hapa kidogo nikisema: "Haki ya kutoa amri na kufikiria utii." au: "Hayo yanayopelekewa maombi ya kupatiwa haki ya kuamini na kutenda kwa njia fulani ya pekee."
- C. Kuna namna mbalimbali za mgawanyo zihuuso "mamlaka", lakini nafikiri ya kwamba maelezo ya hapo juu yatatosha kwa kusudi letu la leo.
- D. Mfano mmoja: Chuo cha Juu - mkataba wa malipo ya serikali - Halmashauri yaamua maongozi - yamwajiri Katibu Mkuu - Katibu Mkuu awaaajiri wasaidizi wake (Angalia : Mkataba na sheri a zake hutoa idhini ya vitendo vya hatua zote za juu na za chini ofisini na matumizi yake.)

### **II. JE, KUNA JAMBO KAMA LILE LA MAMLAKA KATIKA DINI?**

- A. Maelezo ya H. N. Wieman juu ya ukweli: "Madhumuni yale yafafanuayo sawa mambo yaliyopo." (Mambo yaliyopo - katika hali ya kuwa kweli)
- B. Je, lipo hasa jambo fulani kama lile la "ukweli" ushindao juu ya mashaka upande wa mambo ya Maarifa? Kama haupo, ingekuwa ya busara wataalamu wote waache uchunguzi wao wa kupeleleza ukweli ulivyo.
- C. Je, kuna jambo kama lile la ukweli ndani ya mambo ya dini? Je, kuna lolote katika dini litakalo - tena lina haki ya kufanya hivyo-wanadamu watende na kufikiria kwa nia fulani ya pekee? Je, kuna mtu, kiumbe, kundi la watu au viumbi, jamii, kanuni, au hati zo zote zilizo na haki ya kuamuru imani na vitendo vya kidini? Na pia kumwahidi haraka yule akubaliye na hizo kwa uaminifu. na kumtisha adhabu yule azikatazaye hizo asizitii?

Kama hii siyo, basi thamani ya dini yo yote ni nini? Twajuaje ya kwamba dini ina thamani yo yote? Twajuaje ya kwamba tumeifikia dini yenye thamani yo yote?

Kama hakuna ukweli, au kama ukweli upo, lakini haupatikani. au kama hakuna mamlaka. basi sisi (wenye dini) twatafuta njia pumbavu sana.

D. Kama kila mwanadamu ni mamlaka yake mwenyewe. basi hakuna ukweli wala mamlaka - au iwayo yote - wala mamlaka hazina thamani yo yote.

E. Lakini kama mamlaka yako katika dini ... na mamlaka hayo ni sauti ya Mungu ... basi lazima kila mmojawetu aangalie sana:

1. Ili tusikataze sauti yake, wala ....
2. Ili tusiikosee sauti ya mwanadamu kuwa sauti ya Mungu.

### III. MAANA KUBWA YA SWALI HILO YAFAHAMWIWA NA YESU:

A. Mt. 21:23-27 ... Kufuatana na mistari hii yaonekana kwamba Yesu alimfikiri mwanadamu kuwa na vyimbuko viwili vya mamlaka kwa hali yake katika mambo ya dini : (kama wale waliozungumza naye wangalijua juu ya kingine, kwa nini hawakujiondoa wenyewe katika shida walizo nazo wakikitaja kile kingine?)

1. Kutoka mbinguni ... hii ndiyo, kutoka kwa Mungu.
2. Kutoka kwa wanadamu.

B. Mt. 15:1-9 .... haiwezekani kuangalia hukumu ya bina.. damu tu.

C. Yesu alitoa sala ili wafuasi wake wawe mmoja .... akilifahamu Neno la Mungu kuwa chombo kile ambacho kitautayarisha umoja huo amba o aliuombea. Yn. 17:17-21.

Kwa hiyo lazima tuliangalie jambo lilivyo: Ama limetoka kwa mbinguni au kwa wanadamu?

### IV. "MAMLAKA" FULANI AMBAYO NAYAKATAZA KUWA "KUTOKA KWA WANADAMU"

A. "Mamlaka" yafahamikavyo na yule asiyeamini (Agnostic) (Bertrand Russell)

1. Haamini "mamlaka" yo yote kama namna ile jinsi watu wa dini waaminivyo ....
2. Kila mtu hufikiria maongozi ya mwenendo wake mwenyewe tu.
3. Hakuna mamlaka, na kwa hiyo hakuna "dhambi" ... kuna mwenendo wa "kupendeza" au wa "kutopendeza" tu. (Lakini. wataamuaje?)

Kila mwanadamu ana mamlaka yake mwenyewe.

B. Mamlaka yafahamikavyo na Waunitari (Unitarians) (Karl M. Chworowsky)

1. Wayafikia yale waaminiyo kwa bidii ya akili na kazi ya roho na moyo.
2. Wakataa Biblia kuwa na mamlaka "wakidumisha sharti za uzuri wa manufaa ya ufahamu unaohusika sana na uhuru wa dhamiri."

Hii yakadiria yale yale: Kila mwanadamu ni mamlaka yake mwenyewe.

C. Mamlaka yafahamikavyo na yule aangaliaye hali ya nje ya ulimwengu  
(Naturalist) H. N. Wieman)

1. "Muumbo" ... mabadilishano katika muumbo.
2. Wazo lile la kwamba Yesu alisaidia "kumwokoa" mwanadamu siyo fundisho la kanuni ... lafikiriwa kuwa la kweli tu kama uchunguzi wa kihistoria waonyesha kwamba tendo hila la mabadilishano limetoka kwa Yesu. (Lingeweza kutoka kwa ye yote mwingine).

Kila mwanadamu na "uchurrguzi wa kihistoria" ni "mamlaka".

D. Mamlaka yafahamikavyo na Wakatoliki wa Kiroma:

1. Kutokuweza kukosa kwa Kanisa ....
  - a. Papa akisema "akikaa kitini mwake".
  - b. Kanisa likiwa katika hali ya Baraza Kuu.
2. Maelekeo mawili ya "ufunuo".
  - a. Biblia
  - b. Mafundisho yatokeayo katika mwenendo wa nyakati.

E. Mamlaka yafahamikavyo na Mamormoni.

1. "Mafunuo" ya Joseph Smith - Kitabu cha Mormoni, Doctrine and Covenant, Pearl of Great Price.
2. Biblia ... siyo hasa.

F. Sayansi ya Kikristo (Christian Science) ... Sayansi na afya.

G. Quakers ... "Bado sauti ndogo".

H. Liberalism ya Kiprotestanti.

## V. NINI NIPOKEAYO KAMA MAMLAKA KATIKA DINI

- A. Mamlaka yote yakaa ndani ya Mungu .... Rum. 9:14-23; Yer. 18:4-6.
- B. Mungu alitoa mamlaka yote kwa Kristo. Mwanawe, Mt. 28:18-20.
- C. Kristo alikabidhi mamlaka kwa Mtume akaahidi ya kwamba atamtuma Roho Mtakatifu awaongoze katika kweli yote ... Yn. 14:26; 16:13.
- D. Aliwapa Mitume mamlaka wafunue Neno lake ... Mt. 16:18; 18:18 mwandishi halisi wa Biblia ni Roho Mtakatifu ... 2 Pet. 1:20, 21. Siyo mchanganyiko wa mamlaka, kama yanakabidhiwa au kama yanaandikwa.
- E. Mitume (pamoja na manabii ambao wameweka mikono yao juu yao) walifunua IMANI, NENO, INJILI.
  1. Kwa muda fulani ilikuwa imetokea kwa midomo tu.
  2. Baadaye ilianza kuwa kwa maandiko ... kisehemu ilikuwa kwa midomo, kisehemu ilikuwa kwa maandiko.
  3. Mwishowe yote yalikuwa kwa maandiko ... 1 Kor. 13:8-10; Yud. 1:3.

## VI. KIWEKO HICHO CHA IMANI KILIFAHAMIKA NA WAANDISHI WA AGANO JIPYA KUWACHENYE MAMLAKA.

- A. Kilifikiririwa kuwa chenye "pumzi ya Mungu" ... 2 Tim. 3:16, 17.
- B. Kilifikiriwa kumkamilisha mwanadamu apate kutenda kila tendo jema ... mistari ile ile ya hapo juu.
  1. Mambo yote ya lazima Yesu aliyoyafanya .. Yn. 20:30, 31.

2. Mambo yote ya lazima Yesu aliyoyafundisha .....Mdo. 1:1, 2.
  3. Hakika ya matendo na mafundisho ya Yesu, Lk. 1:3, 4.
  4. Kumwamini Yesu kuwa Kristo, Mwana wa Mungu, Yn. 20:30, 31.
  5. Uzima kwa jina la Yesu ... pale pale.
  6. Ushirika pamoja na Mitume ... 1 Yoh. 1:3.
  7. Sharti za wokovu Mdo.2:22-38, 39-47.
  8. Ondoleo la dhambi Mdo. 2:38.
  9. Kuwa Katika Kristo, Rum. 6:3.
  10. Kuwa katika mwili au kanisa la Kristo, 1 Kor. 12:13.
  11. Kila tendo jema, 2 Tim. 3:16, 17.
  12. Kuwa kamili ... pale pa1e.
  13. Ulinzi kwa dhambi, 1Yoh. 2:1.
  14. Furaha inayotimizwa, 1 Yoh. 1:4.
  15. Kushirikiana na Watakatifu waMungu, 1 Yoh. 1:7.
  16. Kuyakumbuka yale Mitume waliyohubiri, 2 Pet. 1:15.
  17. Kanuni ya kumtambua nabii wa kweli, 2 Yoh. 1:10; Mdo. 17:11, n.k.,

C. 1 Tim. 4 n.k. asiondoke kwa imani.

D. 2 Tim. 4:1-5 "neno" ni kitu halisi hasa.

E. Gal. 1:7-9 ... Injili ni halisi ya kutosha kiasi hiki, kama ye yote akihubiri kitu kingine alaaniwe.

F. 1 The. 5:21 ... lazima kujaribu mambo yote, lishike lililo jema.

G. Ebr. 2: 1.... lazima tuangalie tusikose wokovu mkuu ..,huu ndio Neno lililofunuliwa katika A.J.

H. 1 Yoh. 4:1 ... ni lazima tuzijaribu zile roho, kwa sababu kuna manabii wa uongo wengi.

I. 2 Yoh. 1:9-11 ... lazima tudumu katika mafunidisho ya Kristo kama tunataka kuwa na Mungu.

J. Rum. 1:16 ... KUOKOLEWA KWA INJILI. 1 Kor. 15:1, 2 ... kuokolewa kwa Injili.

K. 2 The. 1:7-9 ... wataadhibiwa kama hawaamini wala kutii Injili.

L. 1 Kor. 4:6 ... lazima tupate kujifunza kutokupita yale yaliyoandikwa.

M. Ufu. 22:18, 19 ... lazima tusiliongeze wala kuondoa lolote.

N. Yn. 12:48 ... maneno yatahukumu.

O. Yud. 1:3, ... kuishindania "imani" kwa bidii.

## VII. MAWAZO MACHACHE JUU YA MATUMIZI YA JAMBD HILO.

- A. Ile "Sheria ya kitu cha Tatu Kikataliwaeho" ifikiriwe katika jambo hilo. Kuhusu madhumuni sheria hiyo yasema, "Madhumuni fulani kama P, ndiyo kweli au uongo."

ndiyo B (1) Kama Bw. X akisema, A ndiyo B.  
A (2) Kama Bw. Y. akisema, A siyo B.  
siyo B (3) Ingekuwa ya upumbavu, kama Bw. Z. angesema  
kwamba wote wawili sio sawa au wote wawili wakosa.

B. Jinsi ninavyofikiri kulikuwa na mawazo mengi yasiyo halisi juu ya mistari hii katika nehi ya Amerika.

C. Jinsi ninavyofikiri, kulikuwa na mawazo mengi yasiyo halisi juu ya mistatri hii katika nchi ya Amerika.

1. Tunao urithi wenyewe thamani wa uhuru wa dini .... lakini pengine tumeufahamu huo kuwa uhuru KUTOKA dini au UHURU KATIKA dini. Wengine waonekana kufikiri kwamba unyofu watosha tu, ... kwamba si neno, ni nini mtu anayoamini au anayotenda.

2. Lakini Yesu alisema kamba KWELI Y A WEKA HURU ... Yn. 8:32, na Paulo alisema kwamba UONGO HUMLAUMU MTU ... 2 The. 2:8-10.

D. Haja kubwa ya leo siyo kuwa na Kristo mkubwa zaidi, au Mitume - au vitabu vingi zaidi, bali ni haja ya kuwa na watu wengi zaidi wamwaminio Kristo, Mitume na Biblia.

E. Nawatajieni Efe. 4:4-6 ... ndiyo taarifa iliya rahisi sana.

Taarifa ya Paulo kwamba kuna Mungu mmoja ndiyo taarifa iliyo kweli.

Taarifa ya Paulo kwamba kuna Mungu mmoja Siyo taarifa iliyo kweli.

Taarifa ya Paulo kwamba kuna Bwana mmoja ndiyo taarifa iliyo kweli.

Taarifa ya Paulo kwamba kuna Bwana mmoja Siyo taarifa iliyo kweli.

Taarifa ya Paulo kwamba kuna imani moja ndiyo taarifa iliyo kweli.

Taarifa ya Paulo kwamba kuna imani moja Siyo taarifa iliyo kweli.

Taarifa ya Paulo kwamba kuna ubatizo mmoja ndiyo taarifa iliyo kweli.

Taarifa ya Paulo kwamba kuna ubatizo mmoja Siyo taarifa iliyo kweli.

Taarifa ya Paulo kwamba kuna mwili mmoja (kanisa) ndiyo taarifa iliyo kweli.

Taarifa ya Paulo kwamba kuna mwili mmoja (kanisa) Siyo taarifa iliyo kweli.

Fundisho la Petro juu ya wale waaminio, watubu wakabatitzwe wapate ondoleo la dhambi, ndiyo fundisho lililo kweli.

Fundisho la Petro juu ya wale waaminio, watubu wakabatitzwe wapate ondoleo la dhambi, Siyo fundisho lililo kweli.

F. Nawatajieni Mdo. 20:7.

### **La kuangaliwa:**

Taarifa ya Luka kwamba Chakula cha Bwana kilikuwa kimetumika siku ya kwanza ya juma ndiyo taarifa iliyo kweli.

Taarifa ya Luka kwamba Chakula cha Bwana kilikuwa kimetumika siku ya kwanza ya juma Siyo taarifa iliyo kweli.

G. Nawatajieni Efe. 5:19.

Taarifa ya Paulo juu ya muziki ya midomo tu bila kutumia vyombo, ndiyo taarifa iliyo kweli.

Taarifa ya Paulo juu ya muziki ya midomo tu bila kutumia vyombo, Siyo taarifa iliyo kweli.

AZIMIO :

1. Yesu alifundisha kwa maneno rahisi sana ... chachu, wavu, n.k. - angalia tabia ya neno lile la mbegu. Mbegu ni Neno la Mungu - po pote zinapopandwa katika moyo mwema na mwaminifu, tokeo lake kila mara ni mtoto wa Mungu ... ambaye ataamini umoja.
2. Kuna maelekezo fulani katika kila wakati kukataza mamlaka. Wakati wetu siyo tofauti. Shetani alikuwa amekana maneno ya Mungu tangu wakati wa bustani ya Edeni, yaani "Hakika hamtakufa." Lazima tuyakinge maneno kama hayo ili tusiamini uongo, tusipatee, 2 The. 2:10. Bwana atusaidie kila wakati.

### **ILANI YA PEKEE:**

Napasiwa kumshukuru ndugu Thomas B. Warren, Mkuu wa Idara ya Biblia ya Chuo cha Freed Hardeman, Henderson, Tenn., kwa mistari ya maelezo ya hapo juu. A. M. C.

### **V. MAFUNDISHO YASIYO SAW A JUU YA MAANDIKO "YENYE PUMZI YA MUNGU".**

- A. Uhafifu halisi: "Hatuamini upuzio hasa; hatupokei upuzio wa kila neno, hatukubali upuzio wa sentensi, lakini twapokea upuzio wa mawazo."
- B. Ukatoliki wa Kiroma: "Biblia ni yenyepumzi ya Mungu, lakini Papa tu akisema akikaa katika Kiti chake ('ExCathedra') ana uweza wa kuyaeleza Maandiko .. Mafundisho ya Kanisa yanatia sharti sawa na Maandiko."
- C. Wamormoni: "Joseph Smith asema kama nabii wa Mungu na maneno yake ni sawa na Maandiko."
- D. Sayansi ya Kikristo (Christian Science): "Pokea Mary Baker Eddy mwenye mamlaka yale yale kama Biblia."
- E. Quakers: "tambua sauti ile ndogo tulivu kutoka ndani."
- F. Waprotestanti: "Poke a 'mawazo', 'nia', 'maongozi' ya Roho Mtakatifu, uone kwamba unyofu una mamlaka sawa na Maandiko."
- G. Wote wasiomwamini Mungu (Atheists), wasioamini lolote (Agnostics), waangaliao hali ya nje tu (Naturalists) na Waunitari (Unitarians) hukataza Maandiko wakikubali neno lile kwamba kila mwanadamu amekuwa sheria yake mwenyewe.

### **AZIMIO:**

Ingawa kuna mashambulio mengi na watu wengi wasioamml tangu zamani hadi siku hizi, hata hivyo Maandiko yenyepumzi ya Mungu yaendelea kuongoza wanadamu kutoka giza mpaka nuru, kutoka mauti mpaka uzima. Biblia yaendelea kuwa kitabu kitawanyikacho nyakati zote, na hii iwe siku zote! Labda hakukmva na wakati wenye maana kubwa zaidi katika mwenendo wa historia, ambao yawapasa watu wa Mungu kuyaamini, kuyatii na kuyafundisha mamlaka ya Maandiko yenyepumzi ya Mungu". Hii ndiyo ambayo wokovu wa ulimwengu na wokovu wetu vilevile waitegemea. Mungu akusaidie kuwa mlinzi wa imani wakati wote Mungu anapokuruhusu kuishi

## **ROHO MTAKATIFU**

INGIZO:

- A. Watu wachache sana uhumfikiria Roho Mtakatifu kuwa na nguvu ile ile sawa na Mungu na Yesu Kristo. Wengi wamehesabia Roho Mtakatifu kuwa kama "Kitu" tu. Wengi waamini kwamba Roho Mtakatifu ni jinsi ya "kuona moyoni" tu. Kwa hiyo baada yawongofu, Roho Mtakatifu huangaliwa kuwa kama "mvuto" au kama "kitu kinachoonekana moyoni zaidi kuliko katika maneno." Hiyo ndiyo inayoleta tatanisho kubwa la mafundisho yenye fumbo (mysticism), ujuzi wa ghafula (intuitions), na maongozi ambayo yategemea maono ya moyoni ya mtu tu yanayohusu mamlaka na asili ya vitu.
- B. Roho Mtakatifu ni nafsi, nafsi ya kiungu, sehemu ya Utatu.
- C. Kufafanua ushuhuda waakili na Maandiko kwamba Roho Mtakatifu ndiye nafsi hasa. Kuonyesha kwamba ndiye sehemu ya Uungu. Kueleza majinana tabia fulani za Roho Mtakatifu.

### **I. ROHO MTAKATIFU NDIYE NAFSI:**

- A. Roho Mtakatifu ndiye nafsi akiwa na hali ya binafsi.
1. Fafanusi juu ya nafsi, hali ya pekee, silika, ushawishi, maisha, fikra, kwa hiyo kuwa na tabia za nafsi.
  2. Ndiye mwenye umoja katika kuwako kwake, akatajwa kuwa mmoja.
    - a. Yesu kila mara alimtaja katika hesabu ya umoja na katika jinsi ya kiume, taz. Yn. 14:26; Yn. 15:26; Yn. 16:13.
    - b. Roho Mtakatifu ana tabia za kuwa ndiye nafsi.
      1. Nia - Rum. 8:29
      2. Kusudi - Mdo. 16:7; 21:11-14
      3. Hujua na kufunua - 1 Kor. 2:10-11.
      4. Hunena - 1 Tim. 4:1
      5. Huchunguza - 1 Kor. 2: 10
      6. Husaidia - Rum. 8:26
      7. Huhuzunika - Efe. 4:30
      8. Hupenda - Rum. 15:30
- B. Roho Mtakatifu ndiye mwenye kuwako, nafsi yenye akili; kwa hiyo siyo ndiye "Kitu".

### **II. ROHO MTAKATIFU NDIYE WA KIUNGU- UMUNGU - SEHEMU YA UNGU**

- A. Roho Mtakatifu ana tabia za nafsi, lakini ana tabia za Umungu vilevile; kwa hiyo yeye ndiye nafsi ya Kiungu.
1. Roho Mtakatifu ni wa milele, Ebr. 9:14
  2. Roho Mtakatifu yupo mahali po pote, Zab. 139:7
  3. Roho Mtakatifu ajua yote, 1 Kor. 2:10
  4. Roho Mtakatifu ana nguvu yote, Mwa. 1:1-3.
- B. Roho Mtaaktifu ni Mmoja wa wale Watatu katika Uungu.

Mistari mitatu yatumia neno lile la "Uungu", nalo latoka kwa maneno matatu mbalimbali katika andiko la asili. Mistari - Mdo. 17:29; Rum. 1:20; Kol. 2:9. Kila neno la hayo matatu lina maana yake tofauti kidogo. Lakini kila moja lafahamika kwa mistari mingine kwamba maana yake ndiyo "la Kiungu", kubwa kuliko mwanadamu.

1. Maandiko yaonyesha wazi kwamba watatu waonekana kuwa wa Kiungu; Mt. 28:19; Mk. 1:9-11; Rum. 15:30; Yn. 15:26.
2. Mistari ifuatayo yataja wale nafsi watatu, na kila mmoja wao ameitwa Mungu; 1 Kor. 8:6; Yn. 1: 1; Mdo. 5:3-4. Basi ikoje kwamba kuna nafsi watatu wa Kiungu, lakini Mungu ni mmoja tu?

### III. MAJINA NA MAANA YA ROHO MTAKATIFU:

A. Majina mbalimbali kumi na manane hutumika kwa kumtaja Roho Mtakatifu katika Agano la Kale, na thelathini na tisa katika Agano Jipyä, kwa jumla ni majina mbalimbali hamsini na mawili; matano yaktumika katika A.K. na katika A. J. vilevile; taz. Roho wa Mungu, Roho wa Bwana, Roho yangu, Roho Mtakatifu, na Roho.

B. Neno lile la kuonyesha nafsi ya pekee, "Yeye", hutumika tena na tena.

### AZIMIO:

Kwa hiyo lazima tuone kwamba madhumuni yetu ni ya kweli.

Roho Mtakatifu ndiye nafsi ambaye yuko kweli. Yeye ndiye nafsi ya Kiungu, yaani Mungu. Yeye ndiye sehemu ya "Watatu" wa Uungu.

## KAZI YA ROHO MTAKATIFU

INGIZO:

A. Ulimwengu wetu una sehemu mbili, yaani ile ya kimwili na ile ya kiroho, yaani ile ya dunia hii na ile isiyo ya dunia hii. Lazima kila mwanafunzi Hhodari azione pande hizo mbili tofauti katika kuishi kwetu. Upande ule moja hauwezi kujibu badala ya ule mwingine, wala ule mmoja hauwezi kutwaa mahali pa ule mwingine.

B. Roho Mtakatifu wa Mungu alifanya kazi pan de zote za muumbo wa ulimwengu. Upande wa kimwili na upande wa kiroho vilevile.

C. Kazi ya Roho Mtakatifu ilifunika muumbo wa kimwili na ule wa kiroho vilevile.

D. Kuonyesha kazi ya Roho Mtakatifu katika muumbo wa kimwili na wa kiroho.

### I. KAZI YA ROHO MTAKATIFU KATIKA MUUMBO W A KIMWILI:

A. Uungu katika muumbo.

1. Mungu Baba alikuwa ameanzisha, akaandaa, akatawala.
  - a. Yer. 51:15 - ameumba kwa uweza wake, hekima, na ufahamu wake ... kwa hiyo alikuwa akiweza yote na akijua yote.
  - b. Zab. 29:4 - Mungu alisema, ulimwengu akawa, Mwa. 1:3.
  - c. 1 Fal. 8:27 - "Mbingu na mbingu za mbingu" hazimtoshi. Yeye ndiye aliyepo mahali pote, Zab. 139; Yer. 23:24.
2. Neno aliumba vitu vyote - Yn. 1:1-3; 1 Kor. 8:6; Kol. 1:16-17; Ebr. 1:2; Mwa. 2:3. Neno lilionenwa ndilo mtendaji wa Mungu katika muumbo.
3. Roho Mtakatifu alikuwako katika muumbo - Mwa. 1 :2. "Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu" Tohu na Bohu, 'ghasia na buruga bila mpango wala ularatibu na sehemu mbalimbali" (Katika Komentari ya Clarke).

"Ikatulia" - Meracheepheth, "Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji ... neno hilo ni kama mfano wa kuku aatamiaye akiatamia mayai au akilisha vifaranga wake." (Katika Komentari ya Clarke).

"Roho" - Ruach, katika A. J. limetafsiriwa kwa Pneuma, "Roho Upopo .." Hapa neno lile "wa" katika "wa Mungu" huonyesha kwamba ndiye mali ya Mungu na uhusiano wake pamoja na Uungu. na bila shaka huyo ndiye Nafsi ya Tatu wa Uungu, Yn. 3:8, pia Mdo. 2:2.

B. Mtakatifu aliweka utaratibu wa ulimwengu wa kiriiwili. Kuweka utaratibu, - kutengeneza au kusimamia sehemu zinazotegemeana; kupanga sehemu zisizo na utaratibu.

Neno lile la Kiingereza "Universe" ni kutoka lugha ya Kilatini: "Unus" ni kama "moja", na "vertere, versum" ni kama "kugeuka"; kwa hiyo "universe" ni kama "kugeuka kuwamoja".

1. Maneno matatu ya Kiebrania katika Mwa. 1-2: muumbo, utengenezaji, na ufanyaji katika mwanzo.

a. "Bara", "kuumbwa", "kUita katika kuwako, kufanya kuwako ambako zamani hakukuwako na kitu cho chote." (Boles) "Neno hilo hudhihirisha chanzo cha kuwako kwa kitu, . au kutokea kwa kutokuwako katika' kuwako. Maana yake ya kwanzia siyo kudumishawala kufanya upya kwa vitu vilivyokuwako zamani, kama wengine wafikirivyo, lakini ni muumbo wa asili hasa" (Katika Komentari ya Clarke) Latumika kwa muumbo wa mbiugu na nchi - Mwa. 1: 1. Latumika kwa muumbo wa viumbe vyenye uhai katika bahari na katika anga - Mwa. 1:21.

Latumika kwa muumbo wa: mwanadamu - Mwa. 1:27.

b. "Asah", "kutengeneza (vitu na vitu vya asili vilivyokuwako kutoka zamani)", Iatumika kwa muumbo wa mwanadamu, Mwa. 1:26. Sehemu za mwanadamu zilikuwa zimetengenezwa kwa vitu vilivyokuwako kabla yake, mwili wake.

c. "Yarsar", "kufanyiza, kupasha sura" - latumika kwa mwanadamu - Mwa. 2:7.

d. Webster ameeleza tofauti ya maneno hayo katika lugha ya Kiingereza (neno la "kutengeneza") "kutengeneza", ambalo ni neno litumikalo sana, halitumiki tu kwa kufanya kazi kwa mikono, vyombo, n.k., bali kwa akili, na Mungu vilevile; 'kufanyiza'; neno hila ladekeza ya kwamba kitu kile kilichofanyika kina umbo, sura, muundo wake wa pekee n.k."

2. Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu alivyovitengeneza vitu, akivipa sura, uhai, na nguvu ya kuzaa. Kutoka hali ya ukiwa na utupu, jinsi tusomavyo Mwa. 1:2, Roho Mtakatifu alivitengeneza vitu vyote kwa mpango wa utaratibu kamili.

C. Roho Mtakatifu alltoa sheria za kuendeleza ulimwengu.

1. Vitu vyote vilianzishwa kwa ajabu, kwa muumbo, lakini viliendelezwa kwa sheria ya asili. (Baadaye itaonekana jinsi ufunuo wa mapenzi ya Mungu ulinganavyo na hayo, mapenzi ya Mungu yalijulishwa kwanza kwa ajabu, kisha yakaendelezwa kwa sheria.)

a. Ayu. 26:13 - Roho Mtakatifu alizipamba mbingu. "'Kupambwa' kwa mbingu, labda maana yake ni kuweka sayari za angani mahali pao pa kufaa, na kudumisha kwake huzunguka katika miuda ya mwenendo wao angani wakati wote ikiwapo. Kazi hii hufanyika na Roho Mtakatifu, na huendelezwa na Roho vilevile." (Boles, uk. 40), Mwa. 1 :11, 22.

b. Zab. 104:30 - Roho Mtakatifu akagua jamii ya Isa. 32:15.

Kuwa mahali pote. Kwa hiyo, po pote sheria za asili zilizopo, ndipo Roho Mtakatifu yupo. Mimea na miti.

c. Zab. 139:7-10 - Roho Mtakatifu ana uwezo wa

2. Mwanadamu alikuwa ameanzishwa kwa ajabu, lakini aendelea kuzaliwa kwa sheria ya asili.

- a. Mwa. 1 :26-27 - Alifanyika, akaumbwa kwa mfano wa Mungu.
- b. Mwa. 2:7 - Mungu alimfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi.
- c. Kut. 31:3 - mwanadamu amejazwa "roho ya Mungu, katika hekima, na maarifa, na ujuzi, na mambo ya kazi ya kila aina."
- d. Ayu. 32:8 - "Lakini imo roho ndani ya mwanadamu, na pumzi ya Mwenyezi huwapa akili."
- e. Ayu. 33:4 - "Roho ya Mungu imeniumba."
- f. Mwa. 1 :28 - Mwanadamu amepewa sheria ya kuzaa, yaani kuzaa wengine kwa sura yake wenye tabia na asili hizo zile zile.

## II. KAZI YA ROHO MTAKATIFU KATIKA MUUMBO W A KIROHO:

### A. Baba katika utaratibu wa ukombozi.

1. Mungu Baba alikusudia utaratibu wa ukombozi Rum. 8:28-29; Efe. 1:3 n.k. "Kujua tangu asili," "pro-ginosko", (kwa Kiyunani) kutoka "pro" = "tangu asili", na "ginosko" = "kujua", kwa hiyo ni "kujua tangu zamani, kabla haijatokea", m.y. kujua kabla ya muumbo wa kimwili.

"Kuamuru tangu asili" = "pro-horizo" (kwa Kiyunani), kutoka "pro" = "tangu asili", na "horizo" = "kuweka mipaka", kwa hiyo ni "kuweka mipaka tangu asili", kabla ya muumbo wa kimwili.

2. Kol. 2:9 - Utimilifu wa Mungu ulikuwapo katika Kristo. Kwa hiyo, ukamilifu wa Baba ulikuwapo katika Kristo "Uungu" = "theotes" (kwa Kiyunani) = "Diety" (kwa Kilatini), m.y. "hali ya kuwa Mungu", johari ya Uungu (Thayer, uk. 288). Neno lile la "Uungu" au "Umungu" hueleza yale yale kuhusu Utatu, kama maneno yale ya "utu" na "utoto" hueleza kuhusu hali ya kuwa mtu au mtoto, yaani ni nini hasa imfanyayo mtu kuwa mtu, aumtoto kuwa mtoto.
3. Yesu amezaliwa na Mungu - Yn. 1:18; Mdo. 13:33.
4. Mungu Baba alimtuma Kristo duniani - Rum. 8:3.
5. Mungu alikuja ndani ya Kristo - 2 Kor. 5:19.

### B. Kristo alikuwa mtendaji katika kutimiliza utaratibu wa ukombozi.

1. Mt. 1:23 - Alikuwa Imanueli, "Mungu pamoja nasi". Uungu uliofanyika mwili. "Kuwakatika mwili", "kuvikwa kwa mwili, au kwa hali na sura ya kimwili; kufanyika mwili kwa sura ya binadamu" - Webster.
2. Fil. 2:6-7 - Yesu alikuja duniani kwa mapenzi yake mwenyewe.
3. Yn. 4:34 - Yesu aliwafunulia wanadamu mapenzi ya Baba.

### C. Roho Mtakatifu alitengeneza na kufunua utaratibu wa ukombozi, Yn. 14:16-18; 14:25-26; 15:26-27; 16:7-16 .

1. Lk. 1:35 - Alimfunika Mariamu kama kivuli, akishirikiana katika Kufanyika mwili.
2. Mt. 1:18, 20 - Mariamu alikuwa na mimba kwa uweza wa Roho Mtakatifu.
3. Kol. 2:9 - Utimilifu wa Uungu katika Kristo.

### D. Roho Mtakatifu alitoa Sheri a kwa Ufalme wa Kiroho.

1. Mt. 10:20; Yn. 14:26 - Alisema kwa vinywa vyatya mitume.
2. Yn. 15:26; 16:7-15 - Aliwafunulia mitume mambo fulani.

3. 1 Kor. 2:13 - Mitume walikuwa wakiandika, wakati wakiongozwa na Roho.

4. 1 Kor. 2:13 - Mitume walikuwa wakinena kwa njia ya Roho.

E. Yatokanayo na hayo: Ullinganifu wa tabia za muumbo wa kimwili na wa kiroho.

1. Nafsi zile zile upande wa kimwili na kiroho.

2. Utawala ule ule katika zote mbili.

a. Mungu Baba alianzisha na kupanga zote mbili.

b. Mungu Mwana, Kristo kama Neno, alikuwa mtendaji wa zote mbili akizitimiliza zote mbili.

c. Mungu Roho Mtakatifu alitengeneza akakamilisha na kuziendezea zote mbili .

d. Kwa hiyo, kuna upande wa kimwili na upande wa kiroho, ambazo zote mbili zimetengenezwa na Roho Mtakatifu kufuatana na mapenzi ya Baba, zikiwa zimetimilizwa na Mwana.

#### AZIMIO:

Twaona ya kwamba madhumuni yetu yamefafanuliwa wazi kwa kutosha kuwa ni kweli, yaani Roho Mtakatifu alikuwa akifanya kaz; i katika muumbo wa kimwili na kiroho vile vile.

## **VIPAWA VYA MWUJIZA VYA ROHO MTAKATIFU**

INGIZO :

- A. Vipawa vya mwujiza vya Roho Mtakatifu vilitolewa na Mungu kwa Mitume; viliweza kugawanywa katika kanisa lile la zamani kwa njia ya "Kuwekewa mikono" ya Mitume; vilikoma wakati makundi hayo mawili yalipokufa na ufunuo wa maandiko ulipokuwa tayari.
- B. Kuonyesha hali ya vipawa vya mwujiza; kuchunguza jinsi vilivyapokelewa na jinsi vilivyogawanywa; kuonyesha vipawa vya mwujiza vilidumu kwa muda gani.
- C. Katika masomo yetu mpaka sasa, tumeona ya kwamba "kipawa cha Roho Mtakatifu" katika Mdo. 2:30 kilikuwa Roho Mtakatifu mwenyewe. Tuliona vile vile kwamba kili-kuwa ahadi ya kuenea po pote kwa wote waaminio na kubatizwa wapate ondoleo la dhambi. Tuliona kwamba Ubatizo wa Roha Mtakatifu uliwafikia Mitume tu, isipokuwa Kornelio na nyu11ba yake vile vile, ili ionyeshwe wazi kwal11ba Mungu amewapokea mataifa jinsi alivyowapokea Wayahudi. Mdo. 11:17-19. Sasa tutaingia somo juu ya vipawa vya mwujiza vya Roha Mtakatifu, jinsi vitumikavya, jinsi vипатиканавыо, na jinsi vikomavyo.

### I. KULIKUWA NA "KIPAWA CHA MWUJIZA" CHA ROHO MTAKATIFU:

- A. Watu "waliowekewa mikono" ya Mitume walipokea nguvu ya mwujiza. Mdo. 6:5-6, 8; 8:6-7, 13, 17-19; 19:1-7; Rum. 1:11.
- B. Lakini wale ambao Mitume "waliweka mikono" juu yao, hawakuweza kuwagawanyia wengine kipawa hiki!
  1. Filipo alikuwa mtu wa aina hii. Mdo. 6:5-6; Mdo. 8:7, 13.
  2. Mitume walihitajika wagawanye kipawa hiki. Mdo. 8:18.
  3. Lakini hata Filipo alikuwa na uweza akawabatiza, Mdo. 8:12-13; kwa hiyo walipokea "kiwapa cha Roha Mtakatifu" kama ilivyo Mdo. 2:38.

Maangalizi:

1. Yaonekana ya kwamba "kipawa" katika Mdo. 2:38 hakikuwa cha mwujiza.
2. Wale ambao Mitume waliweka mikono juu yao, wakati walipoweza kutenda miujiza, hawakuweza kuwagawanyia wengine hiki.

### II. KIPAWA HIKI CRA MWUJIZA KWA NJIA YA "KUWEKEWA MIKONO" YA MITUME KWA WATU BINAFSI FULANI.

- A. Mitume "waliweka mikono" juu ya haa wafuatao:
  1. Wale Saba, Mdo. 6:5-6.
  2. Wale Wasamaria, Mdo. 8: 14-21.
  3. Wale Waefeso, Mdo. 19:1-7.
  4. Wale Warumi, Rum. 1:11, n.k.

B. Maonyesho ya mwujiza yalitokea.

1. Kunena kwa lugha ya mwujiza yameorodheshwa, 1 Kor. 12:1; 12:4; 12:8-11; I Kor. 12:28-31. (vipawa tisa nya mwujiza kwa jumla).

Maangalizi:

1. Roho Mtakatifu hakutolewa kwa kitendo ki1e cha kuwekea mikono ya Mitume, bali ilikuwa i1e asili ya mwujiza tu iliyogawanyika.
2. Hii haikuweza kuitishiwa kwa ye yote mwingine.
3. Miujiza ilishuhudiwa kila mara wakati Mitume walipogawanya kile kipawa cha mwujiza.
4. Roho Mtakatifu kama kipawa alikuja kwa njia ya kuitii injili; Mdo. 2:38; maonyesho ya mwujiza yalitokea kwa mikono ya Mitume tu.

### III. KILE " KIPAWA CHA MWUJIZA" LAZIMA KIMEKOMA.

A. Kama kilitokea kwa mikono ya Mitume tu basi bila shaka haiwezekani kukitazamia siku hizi - kwa hiyo siku hizi hakuna ushuhuda wa kweli wa miujiza ya Mitume na Kanisa lile la zamani.

B. Biblia yaonyesha jinsi miujiza ilivytumika, Mk 16:16-20; Ebr. 2:1-4.

1. Kuthibitisha neno lao.
2. Neno limekwisha thibitishwa.
3. Kwa hiyo hakuna haja na miujiza siku hizi.

Maangalizi:

Kwa njia hii, na kwa njia hii tu, yawezekana kujua kwamba msemaji alifundisha ukweli.

C. 1 Kor. 13:8-12, mistari hii yafundisha wazi komo la mambo ya mwujiza:

1. Unabii - lugha - maarifa - zote zitakoma. Hizo zilikuwa za mwujiza, 1 Kor. 14.
2. Ijapo ile ilio "kamili". Katika lugha ile ya asili ya Kiyunani, neno lile "kamili" lipo katika mfano wa kuonyesha kwamba ni kitu hasa, siyo mtu ..
3. Maelezo yaliyotolewa na Paulo yaonyesha kwamba ile "kamili" ndiyo ufunuo uliomalizika, mst. 12. Pia, neno lile "kamili" lina maana ya kuwa "zima" au "pevu".

Maangalizi:

1. Kama ya Mwujiza yangeweze kana au yangetokea leo, wateteaji wangevunja 1 Kor. 14 vibaya!
2. Wakati kanisa lilipokuwa katika hali ya uchanga, lilihitaji "misaada hii ya pekee" '- lakini hili siyo lazima siku hizi. Ufunuo uliomalizika watukabidhi yote tunayohitaji, Yud. 1:3; 2 Pet. 1:3.

Swali :

Nini inayohusu "mambo ya mwujiza" yashuhudiwa katika dini siku hizi?

AZIMIO:

Mungu alipowaumba mwanamume na mwanamke, hii ilikuwa imetokea kwa mwujiza; baadaye sheria ya asili ilianza kazi.

Mungu alipoliunda kanisa liwepo, aliyatumia mambo ya mwujiza ili alianzishe na kulisaidia kanisa katika uchanga wake. Mwishowe sheria iliyokuwa imefunuliwa ilianza kazi: kwa hiyo madhumuni yetu ni ya kweli.

## **UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU**

INGIZO :

- A. Mungu alitenda miujiza akauveka Ubatizo wa mwujiza wa Roho Mtakatifu.
- B. Kuonyesha Ubatizo wa mwujiza wa Roho Mtakatifu. Kuwaonyesha wale walioupokea ubatizo huo. Kuonyesha kusudi la Ubatizo wa aina hii.
- C. Kwa sababu wasiwasi na mashaka mengi yametokea katika jambo hilo, ni muhimu hasa tulizungumze swali hilo na kuyapeleleza Maandiko ili tupate ukweli katika jambo hilo.

### I. UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU:

- A. Ile "ahadi" ya Yohana, Mt. 3:11.
- B. Ile "ahadi" ya Kristo, Lk. 24:48-49.
  - 1. Iliwabidi "kungoja" katika mji wa Yerusalem.
  - 2. Iliwabidi kupokea "uwezo" utokao juu.
  - 3. Iliwabidi "kushuhudia".
- C. "Agizo" limetolewa mara ya pili, Mdo. 1:2-4.
- D. "Uwezo" umetolewa mara ya pili, Mdo. 1:5.

Maangalizi:

- 1. Kama huwezi kuyakinia kuhusu neno lile la Yohana katika Mt. 3: 11, ni nani anayesemwa, Yesu kwa "kusema maneno yake tena" na kwa "kuyaeeza" mbele ya Mitume, aeleza wazi kwamba ndio "Mitume tu" wanaohusika.
- 2. Wale waliopokea ahadi ile, waliupokea "uwezo" vile vile. Nani waliupokea "uwezo"? Mdo. 2:1-4, yaonyesha kwamba ni Mitume "tu" waliupokea "uwezo" wa kusema kwa "lughu", 2:13. Petro na wale kumi na mmoja wengine, 2:14. Pia fikiria neno lile "wao" katika Mdo. 2:1 na Mdo. 1:26. Ni wazi kwamba ndio Mitume waliohusika.
- 3. Tangu wakati u1e tu Mitume "walipoweka mikono yao" juu ya mtu, tunazo habari kwamba Mitume waliitenda miujiza, 2:43; 3:3; 3:6; 4:33; 5:12; 5:15-16; 6:6, 8.
- 4. Mitume walikuwa mashahidi wa pekee, Mdo. 1:22, pia Mdo. 1:26 "akahehsabiwa kuwa pamoja na mitume kumi na mmoja"; "sisi sote tu mashahidi wake", Mdo. 2:32; wasikilizaji waliwasihhi Mitume walipowau1iza "watendeje", Mdo. 2:37. Hiyo ndiyo itimilizayo amri ya Yesu ya kusema, "ngogeni", "pokeeni uwezo", "shuhudieni".

### II. UBATIZO WA ROHO MTAKATIFU ULITOKA MBINGUNI, NILIKUWA WA KUONEKA NA WA KISIKILIKA :

- A. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ulitoka mbinguni hasa, ukakabidhiwa kwa utumi wa binadamu.
  - 1. "Mungu amekimwaga kitu hiki".

2. "Mnaehokiona sasa".
3. Na "kukisikia," Mdo. 2:33.

Maangalizi:

1. Yalikuwa mafafanusi ya1iyosikilika, 2:2. Kitu fulani kilioneka; kwa hiyo yalikuwa mafafanusi ya1yooneka, 2:3. Kitu fulani kilitendeka; walianza kusema kwa kwa 1ugha (lughha, Mdo. 2:7-12; "lughha zetu wenyewe").
2. Hii siyo yale mathubutu yaliyo dhahiri katika "ahadi" ile ya Mdo. 2:39. Yale "ya1yoahidiwa" na Yohana na Yesu, yakapokelewa na Mitume, siyo yale "yaliyoahidiwa kwa waamini wote. Siyo wote waliokuwa na kipawa cha lughha, 1 Kor. 12:10; 12:30, kwa hiyo "ahadi" mbili tofauti zahusika, 1 Kor. 12:29-31.
3. Wote "waliobatizwa katika Roho Mtakatifu" ndio wale waliosema kwa lughha, Mdo. 2:1-4; 2:6; 2:8; 2:11; 10:44-47. Laldni kulikuwa na wengine waliosema kwa kwa 1ugha bila kubatizwa katika Roho, Mdo. 19:1-6; 1 Kor. 12. Kwa hiyo Mdo. 2:39 hauhusu Ubatizo wa Roho Mtakatifu, kwa sababu, kama ingekuwa hivyo, basi wote wangesema kwa lughha; lakini Paulo akisema, "Je, wote wanana kwa lughha?", anaonyesha wazi kwamba sio wote. Lakini wote wameahidiwa kipawa cha Roho Mtakatifu; kwa hiyo ni wazi kwamba ahadi ya Roho Mtakatifu haifuniki Ubatizo wa Roho Mtakatifu wala kipawa cha lughha.
- B. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ulikuwa "ahadi", siyo amri.
- C. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ulifuatana na miujiza na upuzio.
- D. Ubatizo wa Roho Mtakatifu haukukusudia ondoleo la dhambi wala kumweka mtu katika Kristo.

### III. KORNELIO NA NYUMBA YAKE WALIBATIZWA KATIKA ROHO MTAKATIFU:

- A. Kornelio "alibatizwa katika Roho Mtakatifu", Mdo. 11:15-16.
- B. Hii iliitwa "karama ile ile", Mdo. 11:17, lakini hii ilikuwa tofauti na yote, isipokuwa yaliyotokea "mwanzo", 11:15, na juu "yetu" (yaani "Mitume tu.").

Maangalizi :

Ni wazi kwamba hiyo "karama ile ile "haikuwa kile "kipawa cha Roho Mtakatifu" ambacho waamini wote wameahidiwa; kama ingekuwa hivyo, Je ingaliandikwa kwa urefu wa namna ile?

- C. Ubatizo wa Kornelio katika Roho Mtakatifu ultangulia wongofu wake, kwa hiyo ulikuwa kabla hajapokea ondoleo la dhambi, Mdo. 10:44. Sasa soma Mdo. 11:4, "kwa taratibu," 11:15, Roho Mtakatifu alitangulia kabla ya imani, toba au ubatizo! Lakini "kipawa cha Roho Mtakatifu" hufuata baada ya ubatizo kwa ondoleo la dhambi.

Maangalizi:

1. Kupokelewa kwa Roho Mtakatifu juu ya nyumba ya Kornelio hakukuonyesha kwamba yeze amekwisha kuwa mtoto wa Mungu.
  2. Neno lile "kipawa" linawenza kuwa na maana mbalimbali tofauti kufuatana na mistari iliyopo. Mfano: Gal. 1:1 na Fil. 2:25 (Mitume). Katika mstari wa kwanza, ni mmoja wa wale kumi na wawili; katika mstari wa pili, ni "mmoja aliyetumwa na usharika".
- D. Baada ya kupokea ile karama ya mwujiza ya Roho Mtakatifu, Kornelio na nyumba yake waliagizwa wabatizwe, Mdo. 10:48; kwa ondoleo la dhahmbi, Mdo. 2:38; wapokee kipawa cha Roho Mtakatifu, Mdo. 2:38-39.
- E. Kwa nini nyumba ya Kornelio waliupokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu?
1. Iii ionyeshwe kwamba Mungu alikuwa amepokea, mataifa vile vile na Wayahudi, Mdo. 11:17-18.
  2. Iii kanisa la Kristo liunganishwe, Mdo. 11:19-26.

Maangalizi:

Mungu alikuwa akingoja kwa muda wa miaka kama kumi, mpaka aliwaita watu wake kuwa Wakristo. Alifanya .hivyo tu, baada Wayahudi walikuwa wameyatambua mataifa kuwa warithi wa uzima pamoja nao, na baada Wayahudi na mataifa walikuwa wakisali pamoja katika usharika mmoja.

AZIMIO:

Ubatizo wa Roho Mtakatifu ulikuwa maonyesho ya Mungu ya kushangaza na yenye mwujiza! Ulikuwa mwanzo wa wakati mmoja maalum katika Ufalme wa Mungu, na kwa hiyo ndio wenye maana kwa watu wa Mungu. Matokeo yake yanaonekana hata leo, lakini hakuna mtu leo awezaye kujinenakuwa na uwezo, mathibitisho, na maonyesho ya aina hii. Lakini mtoto wa Mungu mpaka leo hupata kipawa cha "kuenea pote" cha Roho Mtakatifu.

## **KIPAWA CHA KUENEA POTE CHA ROHO MTAKATIFU**

INGIZO:

- A. "Kipawa cha Roho Mtakatifu" ni Roho Mtakatifu mwenyewe anayetolewa kwa kila mtu aliyebatizwa akiwa mwamini atubuye.
- B. Kuonyesha kwamba kipawa cha Roho Mtakatifu ni Roho Mtakatifu mwenyewe, tena ni kipawa cha kuenea pote kwa watoto wa Mungu.
- C. Roho Mtakatifu ameahidiwa kwa njia ya Iipuzio kwa watoto wote wa Mungu; kwa hiyo aweza kuitwa "kipawa cha kuenea pote".

### **I. "KIPAWA CHA ROHO MTAKATIFU" KATIKA Mdo. 2:38 NI NINI?**

- A. "Kipawa ndicho Roho Mtakatifu (jinsi ya kujulisha mwenyewe)" A. T. Robertson, Word Pictures of Greek New Testament.
- B. "Jinsi ya kujulisha kitu", N. Turner, Grammar of New Testament Greek. Kipawa kilikuwa Roho Mtakatifu.
- C. Mara nyingi Mungu hayasemi yale ambayo "mimi" nataka ayaseme, lakini hata hivyo nina wajibu wa kujifunza na kuyapokea yale aliyoyasema.

### **II. AHADI ILIKUWA YA KUENEA POTE:**

- A."Ahadi ni kwa ajili ya Wayahudi, na kwa watoto wao, na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Mungu." Mdo. 2:39. Kwa hiyo, kwa ajili ya Wayahudi na mataifa - kwa watu wote, ling. Efe. 2:11-13 (na mengine).
- B. Wote "walioitwa". Mungu aitaje? Mdo. 2:37 "wakachomwa mioyo yao," Mdo. 2:38 wafanye nini, Mdo. 2:40 wamc:onywa kufanya hivyo, Mdo. 2:41 walilipokea neno lake wakabatizwa, Mdo. 2:47 "wakiokolewa"; kwa hiyo wote walioyapokea masharti, wameahidiwa Roho. Wakati wote wanadamu waweza kusikia injili na kuitii, Mungu ataitimiza ahadi yake ya kipawa cha Roho Mtakatifu.

### **III. WOKOVU - JE, HUO NDIO KIPAWA CHA ROHO MTAKATIFU?**

- A. SIYO! Hakusema, "tubuni mkabatizwe kwa ondoleo la dhambi mtaokolewa." Wokovu limo ndani ya ondoleo la dhambi. Ni lingine lililoahidiwa. Ni nini?
- B. Roho Mtakatifu mwenyewe!

### **IV. NENO - JE, HILO NDILO KIPAWA CHA ROHO MTAKATIFU?**

- SIYO! Sababu "neno" halie1ezwi hivyo. Walilipokea neno kabla hawajabatizwa, kwa sababu walikuwa "wamekatwa". "Maneno" yaliwaambia wafanye nini. Wote walioyatenda walilipokea. "neno"; hata hivyo bade kitu kingine kilielezwa. Neno na roho siyo kitu kimoja. "Kipawa" kilikuwa kimeahidiwa, wakati waliokuwa wamekwisha pokea neno na kubatizwa; kwa hiyo kile' "kipawa" siyo "neno la Mungu .. " Efe. 6:17.

### **V. MISTARI MINGINE IHUSUYO WAKRISTO WAKIPOKEA KIPAWA CHA ROHO MTAKATIFU:**

A. Mdo. 5:32, mstari huu wasema kwamba Roho Mtakatifu hutolewa kwa wale watiiro. Roho Mtalcatifu alikuwa ameahidiwa kwa wale waitiiro injili, Mdo. 2:38. Watiiro watajwa katika mistari yote miwili; jinsi gani twaweza lcuepuka, tusidhani kwamba Roho Mtalcatifu mwenyewe ametajwa katika mistari hiyo miwili?

B. Mdo. 6:3, watu hawa walikuwa "wenye kujawa na Roho Mtakatifu". Bila shaka, hao ndio wale wale wa Mdo. 2:38 na 5:32. Lakini, hata kama ikawa hivyo walikuwa tofauti na wale wanafunzi wengine kwa aina fulani.

Sababu wote walikuwa na kile kipawa, bila shaka walikuwa wamejitolea maisha yao kwa Roho na kwa Mungu, zidi kuliko wengine walifanya. Miujiza haihusiki wala haitajwi hapo.

C. Rum. 8, Roho, Roho wa Mungu, na Roho wa Kristo hukaa ndani ya Wakristo, Rum. 8:9. Katika 8:11, neno lile "kukaa" latoka kwa neno "nyumba au makao". Neno hila halihusiki na mahali pa kusimamia kwa mud a tu, bali lahusika na mahali pa kuishia kwa kudumu. Lahuksika na kukaa kwa kudumu. Roho Mtakatifu siyo mgeni wa siku moja tu, bali ni mkazi wa kudumu.

1. "Anakaa" ndani yako hasa. Nini inayoufanya mstari huo kuwa kama mfano?
2. Hautaji wala hauhusiki na mfano wa kitu kingine. "Kila neno linenwalo, lazima lifahamike kufuatana na maana yake ya kawaida, isipokuwa jambo Ienyewe linenwalo au maneno mengine yanayotangulia na kufuata yanaikataza kwa jinsi maalum. Sheria hii yahusu maneno yote, tena ni sheria iliyo lazima." J. D. Bales, The Holy Spirit and Christians, uk. 10.

D. Gal. 4:4-6, siyo kwa maoni yetu wala Kwa upuzio, bali ni kwa Roho kwamba twalia, "Aba, yaani, Baba"" Roho yupi anakaa ndani yetu? Kwa hiyo tunaye shahidi (Rum. 8:16) pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu.

E. 1 Kor. 6:19-20, Paulo adhihirisha, kwa nini Wakristo wasitende uasherati. Paulo asema juu ya mwili wa mwanadamu uonekanao. Mwili huo ndio hekalu la Mungu, ambalo Mungu anakaa ndani yake kwa Roho Mtakatifu. Asema wazi juu ya "Roho aliye ndani yenu". Labda hiyo ndiyo sababu kwamba kanisa au mwili wa Kristo huitwa hekalu la Roho Mtakatifu, 1 Kor. 3:16.

Maangalizi:

1. Mistari hii yaonyesha wazi kabisa kwamba Roho Mtakatifu akaa ndani ya watu wa Mungu.
2. Anakaa ndani ya mtu zaidi ya mmoja, wakati ule ule.
3. Tena hakuna lolote lililo kinyume cha akili, uwezekano, au maandiko, kuhusu kukaa kwa Roho Mtakatifu ndani ya mwili wa kibinadamu.

## VI. ROHO MTAKATIFU AKIKAA "NDANI YA NENO TU":

A. Kuna ndugu wanyofu wengi wenye akili waammlO kwamba Roho Mtakatifu anakaa ndani ya Wakristo kwa njia ya neno tu. Lakini sisi hatuamini hayo. Ndugu hao waingia matatizo magumu ambayo hawawezi kuyashinda kwa akili wala kwa maandiko.

1. Hakuna mstari hata mmoja usemao kwamba hivyo ndivyo Roho Mtakatifu akaavyo ndani yetu.
2. Hakuna mstari hata mmoja usemao kwamba Kristo na Mungu wakaa ndani yetu kwa njia ya neno tu, Efe. 2:22.
3. Kupokelewa kwa Roho Mtakatifu (ahadi yake katika Mdo. 2:38) kulikuwa baada ya kulisikia na kulitii neno.
4. Tumetiwa muhuri na Roho Mtakatifu katika Kristo, Efe. 1:13, lakini kwanza mmebatizwa katika Kristo, Gal. 3:27.

B. Kwa hiyo tumefahamu ya kwamba Roho Mtakatifu anakaa ndani ya Mkristo binafsi, na siyo kwa maneno ya Roho tu, wakati maneno hayo yakipokelewa.

## VII. ROHO MTAKATIFU ATAKAA NDANI YA MKRISTO KWA MUDA GANI?

- A. Lini na kwa sababu gani Roho Mtakatifu anamwacha mtoto wa Mungu? Swali hilo ni lile lile Ia kuuliza, lini yule mtoto wa Mungu anaanguka katika neema asiirudie tena?
- B. Kanisa la Korintho lilikuwa usharika uliokuwa na ukosefu wa dhambi nyingi; hata hivyo kanisa lilikuwa hekalu la Roho Mtakatifu, 1 Kor. 3:16; na washarika hawakuwa mali yao wenyewe, maana "Roho Mtakatifu anakaa ndani yenu". 1 Kor. 6:19.
- C. Roho Mtakatifu hatafuti udhuru wa kutuacha, bali anahamu kubwa ya kuwa msaidizi wetu. Hata hivyo kuanguka kabisa huweza kutokea, na hutokea mara nyingi, Ebr. 6:6; 10:26-31. Mkristo aweza kujifanya moyo wake mgumu kiasi hiki asiweze kumrudia Mungu tena. Wajibu wetu ni wazi. Kuishi maisha yetu kwa ajili ya Mungu.
- D. Wakati wote ambao tunajaribu na kuendelea mbele zaidi, tusiogope. Roho hatatuacha; lakini mara moja akituacha, tutakuwa tumekufa kiroho milele. Yakobo aliyaeleza hayo kwa mfano wa kimwili, ili afundishe somo la kiroho. "Maana kama vile mwili pasipo roho umekufa, vivyo hivyo na imani pasipo matendo imekufa." Yak. 2:26.

## AZIMIO:

Kati ya faida na wajibu ambazo Mkristo anazifurahia, kipawa cha Roho Mtakatifu ndicho cha muhimu sana. Ille ahadi iliyotolewa na watu walioitiwa pumzi ya Mungu wakati wa mahubiri ya kwanza ya injili, yaonyesha jinsi Mungu aonavyo juu ya Roho akikaa ndani ya Mkristo. Mungu atusaidie tuweke hazina ya jambo hila ili tujitahidi kuishi maisha yetu kufuatana na hayo.

## **MAFUNDISHO JUU YA ROHO MTAKATIFU YASIYO SAWA**

INGIZO:

Sidhani kwamba fundisho lolote lingine la Biblia lilitumika ovyo kiasi hiki kama lile la Roho Mtakatifu. Hata ndani ya ushirika wetu wenyewe, ndugu zetu walikosea kuhusu "maongozi" na "masharti" kutoka kwa Roho Mtakatifu. Wapo wengi wanaolcosea kufahamu kwamba kazi ya Roho Mtakatifu ilikuwa "kumtukuza" Kristo, siyo kujitkuza mwenyewe! Yesu alisema, "Yeye atanitkuza mimi", Yn. 16:14. Hapo hutokea wasiwasi mwingL Jinsi mwanadamu aonavyo na asemavyo juu ya Roho Mtakatifu,hivyo ndivyo Roho Matkatifu alivyo muhimu katika maisha yake, akimfundisha na kumfikiria Yesu Kristo.

### **I. WENGINE WAKATAA KUMTAMBUA ROHO MTAKATIFU KUWA WA UNGU.**

#### **A. Fundisho la Mashahidi wa Jehovah.**

1. Yaonekana wazi kwamba Shetani amelianzisha lile "Fundisho la Utatu". Let God Be True, uk. 82.
2. Fundisho la "Utatu" halikukubaliwa na Yesu wala na Wakristo wale wa zamani. Kitabu kile kile, uk. 92.
3. Roho Mtakatifu ndiye nguvu ya Mwenyezi Mungu isiyonekana ikifanya kazi na kuwavuta watumishi wake wafanye mapenzi yake; kitabu kile kile, uk. 89.
4. Roho Mtakatifu siyo nafsi katika Uungu, wala Utatu - Studies in the Scriptures, uk. 169.
5. Hakuna Roho Mtakatifu binafsi aliyefunuliwa katika Maandiko. Studies in the Scriptures, uk. 210.

#### **B. Umormoni hueleza:**

1. Brigham Young alisema "Basi, kumbuka tangu sasa mpaka siku zijazo hata milele, kwamba Yesu Kristo hakuzaliwa na Roho Mtakatifu". Journal of Discourses, Kitabu I, uk. 51.
2. Joseph Fielding Smith, Mkuu wa Mitume Kumi na Wawili, alisema, "Watuambia ya kwamba Kitabu cha Mormoni chasema ya kuwa Yesu alizaliwa na Roho Mtakatifu. Mimi nalibisha neno hilo. Kitabu cha Mormoni hakilifundishi neno kama hilo! Wala Biblia hailifundishi." Doctrines of Salvation, Kitabu I, uk. 19.
3. Katika masomo juu ya Imani yaliyomo katika kupigwa chapa mara ya kwanza kwa Mafundisho na Maagano, mwaka 1835, imesemeka ya kwamba kuna nafsi wawili tu katika Uungu:  
"Swali: Kuna nafsi wangapi katika Uungu?"  
Jibu: Wawili, Baba na Mwana.  
"Swali: Wahakikishaje, kwamba kuna nafsi wawili katika Uungu?

"Jibu: Kwa Maandiko". Doctrine and Covenants, 1835, uk. 55.

4. Lakini sasa mstari ule uliotajwa hapo juu umeondolewa katika kupigwa chapa kingine, ikasemeka sasa "Roho Mtakatifu ndiye nafsi wa kiroho, ambaye ni nafsi wa tatu katika Uungu." The Restored Church, uk. 541, kupigwa chapa 1956.

C. Wabatisti huthibitisha, "Twaamini ya kuwa Maandiko yafundisha kwamba, ili mwanadamu aokolewe, lazima azaliwe upya, au azaliwe roara ya pili; kuzaliwa huko upya ndiko kupokea nia takatifu katika akili; huko ndiko kufanyikako na Roho Mtakatifu kwa jinsi ipitayo ufahamu wetu, kukiunganishwa na ukweli wa Uungu ... " The Standard Manual For Baptist Churches, Edward T. Hiscox, uk. 63.

Tena, "Twaamini kwamba toba na imani ni masharti matakatifu, yaani neema zisizoweza kutenganika, zilizochorwa katika nafsi zetu na Roho ya Mungu ituzaayo upya ... " Church Manual, Babtisti Churches, J. M. Pendleton, uk. 50.

D. Ulutheri husema, "Naamini ya kwamba kwa akili yangu mimi na kwa nguvu yangu mimi siwezi kumwamini Bwana wangu Yesu Kristo wala kumfikia, lakini Roho Mtakatifu ameniita, nilipousikia Utume mwema, akaniangaza aliponipa mapaji yake, akanitakasa na' kunilinda ili nishike imani ya kweli", Martin Luther, Katekismo, uk. 9.

E. Wamethodisti huamini, "Utakaso ni kule kuzaliwa upya kwa hali yetu iliyoanguka, kwa nguvu ya Roho Mtakatifu," Doctrines and Discipline of the Methodist Church, uk. 46.

F. Upresbyteri huhubiri, "Hata hivyo twaungama kwamba mwangaza wa ndani wa Roho ya Mungu unahitajika kwa ufahamu uokoao wa mambo hayo yaliyofunuliwa katika Neno:' (Kwa kweli hiyo ndiyo ambayo wale wengine wote wanifikiria vile vile kwa maneno yao - yaani tendo fulani ambalo latendeka na Roho Mtakatifu mara moja katika moyo wa kibinadamu, ambalo bila tendo hilo mtu hawezি kufahamu wala kulitii Neno la Mungu). The Confession of Faith of the Presbyterian Church, uk. 6.

G. Wanazarini husema - "Tena twaamini kwamba dhambi ya asili huendelea kuwako katika maisha mapya ya yule aliyezaliwa upya, mpaka itang'olewa kabisa na ubatizo pamoja na Roho Mtakatifu". Manual of the Church of the Nazarene, uk. 27.

H. Waadventisti wa Siku ya Saba husema, "Kanisa litakwenda nyuma likiwa bila kipawa cho chote, na kuwako kwa Kipawa cha Roho ya unabii kutakuwa alama moja itakayolitambulisha kanisa lile lililosalia". Church Manual of Seveth Day Adventists, Fungu 20, uk. 54.

Maangalizi:

Hatuna wakati wala nafasi ya kutaja wengine waliota mafundisho yasiyo sawa juu ya "Kuponya kwa Mungu, kusema kwa lugha, miito. maarifa ya mwujiza, kuongozwa na Roho Mtakatifu, kuona ishara, kusikia milio, Mungu akiusemea moyo wangu" n.k. Hayo yote ni mapotoe ya ukweli wa Mungu.

## AZIMIO:

Roho Mtakatifu ni wa Uungu. Ndiye sehemu ya Utatu, na ikiwa hivyo, alishirikiana kwa njia ya ajabu katika wokovu wa wanadamu. Maombezi yake ya kudumu mbele ya kitit cha enzi cha Mungu, hayo ndiyo kati ya faida zetu kuu, kama tukiwa Wakristo. Anakaa ndani yetu, tena ndiye mafariji wetu kutoka kwa Baba. Mungu atulinde tusimwaibishe atusaidie tuyakataze mafundisho yale ya uongo yaaminiwayo na kufundishwa sana katika ulimwengu wa dini.

## ASILI NA HALI YA MWANADAMU

INGIZO:

- A. Mwanadamu ndiye ambaye ni muhimu hasa. Kwa sababu bila mwanadamu, dunia ambayo tunakaa ndani yake, na ulimwengu tunaoujua, hazina maana wala kusudi lolote.
- B. Mwanadamu ambaye Mungu aliiumba kwa ajili yake nyota inayong'aa sana mbinguni. Mwanadamu ndiye aliyeuhuzunisha moyo wa Mwumbaji wake kwa dhambi alizozitenda tena na tena. Mwanadamu ndiye aliyemsulubisha Kondoo wa Mungu akiisababisha mauti vilevile.
- C. Mwanadamu ndiye wa pili chini ya Mungu na Kristo tu katika muumbo mzima wa, Mungu, Zab. 8. Na mwishowe, wakati hukumu na ahera ya milele zitakapotokea, mwana-damu atakuwa madhumuni yake.
- D. Uchunguzi juu ya mwanadamu utujulishe thamani yake machoni pa Mungu, na kutunyenyekeza vile vile tuone wajibu mkubwa mno tulio nao.

### I. ASILI YA MWANADAMU:

- A. Maono mawili juu ya asili ya mwanadamu.
  - 1. Asili kutoka Uungu, Mwa. 1,2,3.
  - 2. "Mapenzi ya kutokezea" (Evolution): Kitu cha kimwili ni cha milele; maisha yote hutoka kwa hali ya kutokuwa na maisha, na kila kitu ni tokeo la bahati.
- B. Mambo ambayo Biblia na Fafanusi la "Mapenzi ya kutokezea" zinakubaliana.
  - 1. Zote mbili zakubaliana kwamba kuna kipimo cha kupaa; wale wafuataao fafanusi la "Mageuzi ya kutokezea" hukataza "Kuanguka kwa mwanadamu".
  - 2. Zote mbili husema kwamba mwanadamu ana uwezo wa kuhojiana, kuwaza, kufahamu, na kujijua mwenyewe.
- C. Uwezo huo wa kuhojiana, kufikiri, na kuwaza watoka wapi?
  - 1. Sainsi haiwezi kutoa jibu.
  - 2. Biblia ndiyo itoayo jibu. Mwa. 1:26; Ayu. 32:8.
- D. Haiwezekani kueleza asili ya mwanadamu kwa ufahamivu, nje ya Mwa. 1.
  - 1. "Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu" Mwa. 1:26.
  - 2. "Akampulizia pumzi ya uhai (Ufasiri wa neno moja moja) .... mtu akawa nafsi hai", Mwa. 2:7 (neno lile lile latumika Mwa. 7:22. 1 Kor. 15:45).
- E. Maneno yatumikayo kwa nafsi, mwili, na roho: Nephesh, basar, ruach (James Orr, Msimamizi wa International Standard Bible ya mwili vile vile.) Roho hutumika kwa wale waliokwisha toka kwa mwili (1 Pet. 3:19). Kwa hiyo.
- F. Mwanadamu ni kwa hali mbili: Mwa. 2:7
  - 1. Mwili wa nyama ... kutoka kwa mavumbi ya ardhi.
  - 2. Roho ... nafsi ... pumzi ya uhai. Ayu. 32:8.
  - 3. Mwanadamu siyo kwa mfano wa kimwili wa Mungu.Mwa. 2:7; Lk. 24:39; Kwa hiyo lazima awe kwa mfano wa kiroho wa Mungu. Yn. 4:24.

## II. HALI MBILI ZA MWANADAMU HUONYESHA KWAMBA SISI TU MWILI NA ROHO:

A. Mwanadamu ana mwili, siyo kwamba ndiye mwili. Kuna mistari mingi katika Biblia itokezayo hali ya kidunia, yaani hali ya kimwili ya mwanadamu. Mara nyingi mistari hiyo hutumika (ikipotoshwa kudhihirisha kwamba hiyo ndiyo ambayo mwanadamu ndiye hasa. Lakini hii siyo kweli. Lazima Mkristo aifahamu mistari hiyo. Zab. 49:10-12; 90:9-10; 103:14-16; Mhu. 1:1-11; 3:19-20; 12:7; Ayu. 10:8; 14:1; 4:19; 34:15; Mwa. 18:227; 3:19; 1 Kor. 15:47; 15:45; 7:34; 2 Kor. 4:7; 5:1; Yak. 2:26; 1 Pet. 1:13-14; Mt. 26:41; Mk. 13:48.

B. Mwanadamu ana roho, siyo kwamba ndiye roho. Kuna wingi wa ushuhuda wazi wa Maandiko pia uonyeshao kwamba mwanadamu ana hali ya kiroho vile vile. Mistari mingi ihusikayo huonyesha hali zote mbili za mwanadamu katika aya ile ile. Bila kufahamu wazi ufunuo wa Mungu katika hali na tibia zote mbili za mwanadamu, twakosa sana uwezo wa kuyatambua mambo yale yaliyo tofauti. Mwa. 1:16, 17; 2:7; Kum. 4:29; 6:5; 11:13; 13:3; Mhu. 12:7; Mt. 26:41; 10:28; Mk. 13:48; Lk. 23:46; 12:20; (46-47; Zab. 2:26; 19:7; 34:22; 42:1; Mit. 11:30; 1 Kor. 2:11; 7:34; 1 Pet. 1:22; 2:11; 2 Pet. 2:8; Ebr. 4:12; 10:39; Flp. 1:27; Yak. 5:20; 1:21; Isa. 26:9.

C. Hali ya nafsi ya mwanadamu hudhihirishwa kwa jinsi nyingi za maelezo na usemi mbalimbali. Kila mojawapo husaidia kusafisha na kuendeleza ufahamu wetu wa ukweli huo wa ajabu.

1. Maisha ya kawaida ya mwili, Mt. 2:22; Lk. 12:22; Mdo. 20:10; Ufu. 8:8; 12:11; Law. 17:11; 2 Sam. 21:7; Est. 8: 11.
2. Sehemu ya mwanadamu isiyo ya kimwili wala isiyonekana, Mt. 10:28; Mdo. 2:27; 1 Fal. 17:21.
3. Kikao cha nafsi yake mwanadamu, Lk. 9:24-25; 1:46; Ebr. 6:19; 10:39.
4. Kitu cha pekee ndani ya mwanadamu, kilicho kama chombo cha kutambua, kufikiri, na kuona hamu. Mt. 11:29; Lk. 2:35; 1:46; Mdo. 14:2-22; Isa. 26:8.
5. Kikao cha mapenzi na nia ya mwanadamu, Mt. 22:37; Mdo. 4:32; Efe. 6:6; Flp. 1:27; Ebr. 12:3; Hes. 21:4
6. Kum. 11:13.
7. Watu fulani au watu wa binafsi, Mdo. 2:41-43; Rum. 2:9; Yak. 5:20; 1 Pet. 3:20; 2 Pet. 2:14 Mwa. 12:5; 14:21; Law. 4:2; Eze. 27:13; Hes. 6:6.
8. Viumbe vyenye uhai ... wa kibinadamu au wengine, 1 Kor. 15:45; Vfu. 16:3; Mwa. 1:24; 2:7-9. Mwili na nafsi ni sehemu ya lazima katika mwanadamu, Mt. 6:25; 10:28; Lk. 8:55; 1 Kor. 5:3; 7:34; Yak. 2:26.
9. Mahangaiko ya moyo yachangamanayo na nafsi, Mt. 26:38.
10. Mahangaiko ya moyo yachangamanayo na roho, Yu. 13:21.
11. Nafsi yamfurahia Mungu, Zab. 35:9.
12. Roho yamfurahia Mungu, Luk. 1:47.
13. Kikao cha njaa na kiu, Ufu. 18:14; Zab. 107:9; Mit. 6:30; Isa. 5:14; 29:8.

D. Roho hutumika kama:

1. Upepeo, Yn. 3:8; Ebr. 1:7; Amo. 4:13.
2. Pumzi, 2 The. 2:8; Ufu. 11:11; 13:15; Ayu. 12:10.

3. Sehemu ya mwanadamu isiyo ya kimwili wala isiyonekana, Lk. 8:55; Mdo. 7:59; 1 Kor. 5:5; Yak. 2:26; Mhu. 12:7.
  4. Sehemu ya mwanadamu inayomwezesha kuon-a. kufi· kiri, kuona moyoni, na kutamani, 1 Kor. 2: 11; Mt. 5:3; 26:41; Mk. 2:8; Lk. 1:47-80; Mdo. 17:16; 20:22; 1 Kor. 5:3-4; 14:4-15; 2 Kor. 7:1; Mwa. 26:35; Isa. 26:9; Eze. 13:3; Dan. 7:15.
- E. Kwa jinsi gani mwanadamu yu kwa mfano wa Mungu?
1. Mfano wa kiakili.
  2. Mfano wa kiadili (ana uwezo wa kupenda na kuchukia, pia ana kanuni ya mema na mabaya, n.k.)
  3. Mfano wa utawala.

### III. YAFUATANAYO NA HALI YA MWANADAMU

- A. Anaweza kujijua mwenyewe nia, hamu, na kusudi lake.
- B. Anaweza kujijua mwenyewe ikihsu kanuni: Sheria (Yak. 1:21-25).
- C. Ana uhuru wa kuchagua anayoyapenda ... ana uwezo wa kufikiria matokeo ya vitendo vyake.
- D. Ana uhusiano (wa asili) wa kumtegemea Mungu.
- E. Ana wajibu mbele ya Mungu ... kwa nguvu ya kuwa ameumbwa. Kuuvunja wajibu huo kutamtenga na Mungu. (Isa. 59:1, 2)

### IV. MWANADAMU - YA KALE NA MAPYA YA ONEKANAVYO KATIKA AGANO JIPYA.

- A. Mwanadamu wa kale na mwanadamu mpya. Rum. 6:6; Efe. 4:22-24; Efe. 2:15; pia Kol. 3:9-10. Huyo ndiye mwanadamu kabla ya Kristo na ukombozi. Hayo yote yamdhuru mwanadamu aliyeanguka, kabla ya wongofu wake.
- B. Mwanadamu wa nje, na mwanadamu wa ndani, 2 Kor. 4:16; Rum. 7:22; Efe. 3:16. Huo ndio mfano mwengine tena, uwekao wazi hali mbili za mwanadamu. ukidhihirisha kuzaliwa upya kwa mwanadamu wa ndani.
- C. Mwanadamu wa kimwili na mwanadamu wa kiroho, Rum. 18:1-14. Nia ya kimwili na nia ya kiroho hazikomi kugombana na kushindana. Ile moja ndiyo mwanadamu, ile nyingine ndiyo Mungu. Hiyo ndiyo rahisi sana, lakini yenye maana kubwa.
- D. Mwanadamu wa tabia ya asili na mwanadamu wa rohoni (kiroho), 1 Kor. 2:14-16. Kwa kweli mistari hiyo yatusaidia kuona ile tofauti kubwa mno kati ya Mungu na mwanadamu, kati ya njia yake na njia zetu. Kuna tofauti mashuhuri kati ya mambo yale sisi tunayoyafahamu na kuyaamini, na mambo yale Mungu anayotaka na kuyaamuru, tukiwa tuzaliwe upya kwa mfano wake. Avumilie kutusaidia! Nasi tuanze kubadilika zaidi na zaidi kila siku ipitayo.

### V. MAFUNDISHO YASIYO SAWA JUU YA ASILI NA HALI NA TUA YA MWANADAMU.

- A. Fafanusi la "Mageuzi ya kutokezea" (evolution) -"Mageuzi ya kutotkezea kamili hayamkulali Mwumbaji, wala mtengenezaji, wala mdumishaji-yafikiriwa

kwamba sheria zisizo na akili wala na nafsi hueleza asili na mi· enendo ya ulimwengu, ya maisha, na ya jamii." Golorious Challenge of Christ, na Warren Roward, uk. 80-81.

1. Mageuzi ya kutokezea ya Kiungu yashikwa na watu wengi wa dini. Mwamini Mungu, lakini wakataza taarifa ya Biblia juu ya muumbo, wakiona kwamba Mungu alimwumba mwanadamu lakini kwa njia ya mageuzi ya kutokezea tu.
2. Fafanusi la Mageuzi ya kutokezea hakuna wajibu wa mwanadamu mbe1e ya Mungu; waona kwamba mwanadamu ana wajibu mbe1e yake mwenyewe, na kwa ajili yake mwenyewe tu; G. G. Simpson, his View of Life, uk. 25.
3. Wafuatao Mageuzi ya kutokezea hufundisha mafafanusi yao kama yangekuwa mambo ya hakika, "Mapigano yamefaulu;" "mabishano na watu wenye akili yamekwisha mwaka 1925"; "Mjinga tu huzungumza juu ya jambo kama 'Mageuzi ya kutokezea kinyume cha Dini'," Science Ponders Religion, Harley Shipley.
4. Watu waaminio hivyo hawaangalii mambo ya ukweli wakinena kwa sauti kubwa - vitu vya kimwili na vya mile1e; uhai hutoka kwa kutokuwa na uhai, na hayo yote ni matokeo ya bahati. Warren Howard, ambaye ni mwenye World Wide Christian Publications, ni Mkristo mwenye akili, akifanya kazi nyingi, mtu amwogopaye Mungu. Napendekeza sana vitabu vyake vifuatavyo :

*The Glorious Challenge of Christ. Jesus Christ and Modern Science.  
The Bible and The Theory of Evolution.*

*Anwani: 398 Grant Ave. Beverly, New Jersey, 08010, U. S. A.*

B. Umormoni - Brigham Young alisema: "Sasa sikieni, wellyeji wa dunia, Wayahudi na mataifa, Watakatifu na wenye dhambi! Wakati baba yetu Adamu alipoingia bustani ya Edeni, aliingia mwenye mwili wa kimbilguni, akimetia Hawa ambaye ni mmojawao wa wake, pamoja naye. Alisaidia kuumba na kutengeneza ulimwengu huu. Yeye ndiye Mikaeli, yule malaika mkuu, Mzee wa Siku! ambaye watu watakatifu wameandika na kusema juu yake yeye ndiye baba yetu na Mungu wetu, Mungu wa pekee ambaye sisi twahusiana naye. Lazima kila mtu wa duniani, Wakristo waaminifu na wasio waaminifu, wote waisikie, na baada ya muda mfupi au mrefu watajua", Journal of Discourses, Kit. 1, uk. 50. C. Tena, Umormoni wasema juu ya hali ya mwanadamu baada ya kufa, "Joseph Smith ... alilikubali fundisho la Kiroma-Kikatoliki kwamba kuna hali ya kati au ya kuandaa kati ya mauti na Hukumu ya mwisho." Mormonism --- Shadow or Reality. J. Sanders Turner, uk. 385. Tena: Herber C. Kimball asema yafuatayo, "Hii ndiyo kuwapenda waovu, yaani kuwapeleka jehanum wachomwe moto mpaka watasafishwa. Kweli, watakwendia pale, watakaa pale, watachomwa, kama kiko kizee kinukacho kwa utumiaji mrefu na uchafu, mpaka watachomwa moto kabisa, na roho zao ziokolewe siku ya Mungu Mwenyezi." Journal of Discourses, Kitabu 4, uk. 223.

D. Ukatoliki - Kanuni juu ya Ahera ya kutakasia (Purgatory). "Kanisa la Kikatoliki limedhihirisha kuwako kwa Ahera ya kutakasia, katika Azimio la Umoja lililopangwa kwenye Mkutano Mkuu wa Firenze, mwaka 1439, na tena kwenye Mkutano Mkuu wa Trento, likisema: "Kanisa la Kikatoliki, likiongozwa na Roho Mtakatifu, likifuata Maandiko Matakatifu na mafundisho ya zamani ya Baba zetu, limefundisha katika Mikutano Mitukufu, na juzi tu katika ule Mkutano Mkuu wa ulimwengu wote kwamba kuna Ahera ya kutakasia, na kwamba zile roho ambazo zimefungwa ndani yake husaidiwa na mavumilivu ya waaminifu, lakini zaidi has a husaidiwa na ile dhabihu ya kupendeza ya madhababu."

"Mkutano Mkuu ule ule ulifundisha (ling. Kikao, XIV, Kan. 12), kufuatana na Maandiko (Res. XX 12:2; 2 FaI. XII. 13, 14) kwamba Mungu haondoi kila mara adhabu zote za mnda kwa sababuya dhambi zilizosamehewa. Maandiko yafundisha kwamba hakuna machafu yo yote yawezayo kuingia mbinguni (Hek. VII. 25; Isa. XXv. 8; Hab. 1:13; Ufu. XXI. 7), na kwamba Wakristo mara nyingi wanakufa wenye dhambi zinazoweza kusamehewa, au wenye adhabu za rouda za dhambi zao ambazo hazijalipiwa bado, kwa hiyo lazima wazilipie kwenye Ahera ya kutakasia." The Question Box, uk. 393-394.

E. Mashahidi wa Jehovah pia wafundisha: "Mwanadamu asiye mkamilifu hamtesi hata mbwa aliyerukwa na akili, bali humwua; hata hivyo wahudumu wa kanisa wamhesabia Mungu aliye upendo (1 Yoh. 4:16), jinai ile mbaya ya kuwatesa viumbe vyatya kibinadamu kwa sababu hii tu kwamba wana bahati mbaya ya kuwa wenye dhambi tangu kuzaliwa kwao." Let God Be True, uk. 79.

F. Tena, "Fundisho lile la jehanum yenyе mota ambapo waovu huteswa milele baada ya kufa kwao, 'haliwezi kuwa la kweli, has a kwa sababu nne: (1) Kwa kuwa ni kinyume kabisa cha Maandiko; (2) Kwa kuwa ni okinyume cha akili; (3) Kwa kuwa ni kinyume cha upendo wa Mungu; na (4) Kwa kuwa ni kinyume cha haki" (Kitabu kile, uk. 80).

G. Na mwishowe, "Mateso ya milele hukosa kanuni ya upendo; Mungu ni upendo; Mwumbaji ambaye angetesa viumbwe vyake milele, angekuwa yule Adui mbaya, lakini asingekuwa Mungu wa upendo." (World Distress, na J. F. Rutherford, uk. 40).

AZIMIO:

Mwanadamu ndiye kiumbe cha juu kabisa katika muumbo wa Mungu. Lakini katika viumbe vyote vya Mungu, ndiye mwanadamu awezaye kujaribu kumwondo mwumbaji wake na kuwa Mungu mwenyewe. Wakati huu wa kiwiliwili ambao sisi twaishi ndani yake, kila mara hujaribu kumfanya mwanadamu, na vitu vya kimwili, na mambo ya dunia hii, kuwa kama Mungu. Tuungame siku zote utegemeo wetu kwa Mungu, uhafifu wa nguvu yetu, udhaifu wa ujuzi wetu, na kutokuweza kwetu kwa kupiga hatua zetu wenyewe. Kila mara na tupige magoti yetu, na tunyenyekeze mioyo yetu, na tuungame makosa yetu, na tumtegemee Mungu wetu aliyeko, aliyekuwako, na atakayekuwako milele! AMIN

## HALI YA SHERIA

INGIZO:

A. Elezo: Sheria ndiyo utawala au mamlaka ya mtu mwenye akili akiwa na nguvu juu ya mtu mwingine mwenye akili.

B. Kuna mambo ya asili matatu katika sheria:

1. Tamani, tumaini, au matakya mtu mmoja mwenye akili, kwamba mwingine afanye kitendo fulani, au aone kwa jinsi fulani.
2. Nguvu ya mtu mmoja ya kulazimisha au kuadhibisha, kama sheria haitiiwi. Kama hakuna adhabu, hakuna sheri a vile vile.
3. Maneno ya kuidhihirisha sheria. Lazima sheria ifahamike.

C. Kuna aina mbili za sheria: Sheria ya Asili na Sheria ya Kiroho.

1. Sheria ya asili: (Sheri a ihusuyo mambo ya ulimwengu huu).
  - a. Sheria ya asili siyo ndani ya elezo lililoandikwa hapo juu.
  - b. Kwa nini wanadamu waiamini Sheria ya Asili? Kwa sababu waamini kwamba mambo ya asili hupatana tamani na matakwa ya mtoa sheria.
  - c. Wanadamu wanapoanza kutokumwamini Mto Sherla, ndiyo wanaanza kusema kwamba mambo ya asili hutokea kwa bahati (ling. A. E. Taylor, Does God Exist? C. S. Lewis, Miracles. ling. Fafanusi la Mageuzi la kutokezea)
2. Sheria ya Kiroho: (Kifungo kifuatacho.)

I. SHERIA YA KIROHO: SHERIA ZINAZOTOLEWA KWA WATU WENYE AKILI NDIZO ZENYE MASHARTI NA ADHABU ZA KISERIKALI, ZA KIJAMII, NA ZA KIDINI.

- A. Sheria za kwanza zilizotolewa kwa watu wenye akili, 2 Pet. 2:4-8, 11; Yud. 1:6; Ebr. 1:7, 13.
  1. Sheria kwa malaika .... hatujui walikuwa nani, wala walipewa sheria lini.
  2. Waliadhibiwa .... na viumbe vingine vyenye akili.
  3. Maneno ya sheria yalikuwemo.
- B. Dibaji kwa sheria walizopewa wanadamu.
  1. Sheria ya milele ya pekee ni hali ya Mungu: Kwa hiyo sheria waliyopewa wanadamu siyo ya milele, ni sheria ya kunenwa.
  2. Hali ya Mungu haibadiliki. Yak. 1:17; Ebr. 1:10-12; Mal. 3:6.
  3. Sheria za Mungu hubadilika kufuatana na maendeleo na kurudi nyuma kwa hali ya mwanadamu (Mungu hutoa sheria mbalimbali nyakati mbalimbali).
  4. Hakuna sheria iliyopewa mwanadamu, iliyotolewa kabla ya Mwa. 1.
  5. Nyakati fulani Mungu alimtolea mwanadamu ridhaa kwa ajili ya ugumu wa miyo ya wanadamu, Mdo. 17:30-21, pia Mt. 19:1-12.
- C. Sheria zilizotolewa kwa wanadamu katika Agano la Kale.
  1. Sheria za kwanza: Mwa. 1-3.
    - a. Zilikuwa zipi:
      - 1) Zaeni mkaongezeke.

- 2) Mkaitiishe nchi.
- 3) Ule matunda yo yote, lakini usile matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya.
- b. Adhabu kwa mwanadamu: "siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika."
- c. Je, walikufa kwa maana ipi?
- 1) Kiroho ... wametengwa na Mungu, Isa. 59:1-2.
  - 2) Kimwili ... wamekuwa wanadamu yawapasayo kufa (tafs. "Ukifa, utakufa"). Wametengwa na mti wa uhai, Isa. 2:26.
  - 3) Swali: Ilikuwa imetajwa adhabu nyingine ila hiyo?  
Ndiyo, (a) Mauti, (b) Kazi, (c) Utungu katika kuzaa watoto.
2. Sheria ya sadaka: kwa Kaini na Habilii. Bila shaka ilikuwa sheria, Ebr. 11:4; Rum. 10:17; Mwa. 4:4, 5, 7, adhabu haitajwi.
3. Sheria ya kukataza kuua, 1 Yoh. 3:11-15; Mwa. 4:8-11.
- a. Labda Kaini na Habilii walipewa sheria hii na Mungu hasa au na wazazi wao, Ebr. 1:1.
  - b. Adhabu: Ardhi haitatoa wingi wa mazao yake na Kaini alikuwa amekuwa mtoro na mtu asiye na kikao.
  - c. Kaini: "Kila anionaye ataniua."

*Maanganizi: Baada ya Mwa. 6 katika maandiko yote ya A. K., kisasi mikononi mwa wale ambao Mungu aliwaagiza kulipiza kisasi.*

*Swali: Kama Wakristo wakiruhusiwa leo kuua, je kwa jinsi gani upendo wetu kwa maadui wetu ni tofauti na upendo wa maadui wetu katika A. K.?*

4. Wanadamu tangu Adamu mpaka Musa walikuwa chini ya sheria zipi?  
Rum. 5:13.
  - a. Kulikuwa na dhambi tangu Adamu mpaka Musa. Gharika, Mwa. 6-7.
  - b. Dhambi fulani hazikuhesabiwa mpaka Musa.
  - c. Dhambi zao hazikufanana na makosa ya. Adamu.
    - 1) Je, kwa maana ipi zilikuwa tofauti  
Dhambi ilikuwapo, lakinui hakukuwa na makatazo hasa, Rum. 7:9.
    - 2) Adhabu haikutangazwa.
  - d. Hata hivyo Mauti alikuwa akitawala juu yao, jinsi aliviyotawala juu ya Adamu.
5. Sheria ambazo matatifa walikuwa chini yao tangu Musa mpaka Kristo, Rum. 2:12-16; Rum. 7. Je, leo mataifa wapo chini ya sheria wanayoifahamu tu? Mk. 16:15-16. Tazama kwamba katika Rum. 7 Paulo aiangalia dhambi kama mtu aishiye kwa muda wa kame nyingi.
6. Sheria ya Musa.
  - a. Makusudi:
  - b. Kuufunua utakatifu wa Mungu, 2 Kar. 3; Ebr. 12.

- c. Kuifunua hali ya dhambi ya mwanadamu, Rum. 7:15.
  - d. Kumtengeneza mwanadamu upya (kadiri iwezekanavyo) kwa ushirika wa Mungu. Law. 17; Kut. 19.
  - e. Kuwaongoza wanadamu kwa Kristo. Gal. 3:24.
7. Haki ya aina gani ilikuwa imeunganishwa na sheri a ya Musa?
- a. "Haki yangu mwenyewe" Flp. 3:9; Rum. 10:2; Rum. 3:20. "Haki ya Mungu inadhihirishwa ndani ya Injili." Rum. 1: 17. "Krista kwa Wayahudi ni kikwazo" ... alifundisha juu ya hali ya dhambi ya wanadamu, 1 Kor. 1 :22.
  - b. Yatambulikana kwamba hakuna neema katika A. K. (Lakini siya kwamba hakuna neema ya yote, Zek. 12:10). Hakuna neema ya kutasha kwa kuhesabiwa haki, Rum. 3:20; 1 Kor. 10:13. Soma pia Ebr. 11:39; 12:1-4.
8. Kusudi la sheria ya Musa lafunua ya kwamba ndiya ya muda tu, Gal. 2:19.
9. Ilihusika kwa kirefu na kumsafisha mwanadamu wa nje. Ebr. 9:9-13. Ilikuwa na maana ya pekee: Mungu alitengeneza matokeo ya kiraho ya A. J. kushindana na matokea kimwili ya A. K. Ebr. 9:23-25.
10. Hapa zamani sheria ilisemwa na manabii kwa wale baba, Ebr. 1:1.
11. Sheria ile ya A.K. ilikuwa imetimizwa. Mt. 5:17-19; Lk. 24:46-47; pia Efe. 2; Kol. 2:14-17.
- D. Sheria zilizotolewa kwa wanadamu katika Agano Jipy.
1. Sheria ya Kristo. Ebr. 1:1; Gal. 6:23, 19; ilikuwa hiyo ambayo mitume waliifundisha kuwa sehemu ya sheria ya Krista: Ndiyo Yn. 16:12-13. Kuwa chini ya sheria ya Krista katika A. J., kufuatana na Rum. 7 ni sawa na kusema kwamba tumealewa na kutawaliwa na Kristo; Rum. 7:1-4.
  2. Sheria ya Raha wa Uzima, Rum. 8:2.
    - a. Ni kinyume cha sheria ya Musa na cha sheria ya dhambi na mauti vile vile.
    - b. Kutawala kwa dhambi katika miili yetu. Rum. 7:12, 13, 21-24.
  3. Sheria ya Imani, Rum. 3:27.
    - a. Imani (Yud. 1:3), kwamba ile jamii ya ukweli huianzisha imani (Rum. 10:17; Rum. 11:7), huitawala imani (2 The. 3:14), na huidumisha imani (1 Tim. 4:6).
    - b. Sheria ya imani ndiyo imani yenye.
    - c. Sheria ya imani ina makusudi hayo:
      - 1) Humfanya mwanadamu aamini. Rum. 10:17.
      - 2) Humwambia mwanadamu yampasayo kuyaamini, huamuru na kuahidi, Mdo. 2:38-39.
      - 3) Humwambia mwanadamu juu ya adhabu, kama asipoamini, Yn. 8:29; Lk. 13:3-5; 1 Pet. 3:21.
    - d. Imani hutengeneza sheria: Twalitengeneza kusudi lile hasa ambalo sheria ilitalewa kwa ajili yake. Gal. 3:17-24. Twaiweka katika cheo chake cha kiungu. Gal. 3:27-31.
  4. Sheria ya Uhuru, Zab. 119:45.
    - a. Hakuna ye yate aliye huru na sheri a, isipokuwa Mungu.

- b. Wengine wate wapa chini ya sheria.
  - 1) Uhuru sio upatavu wa sheria.
  - 2) Kizuio cha upotavu wa sheri a siya usheria wa kupita kiasi.
- c. Huitwa sheri a ya uhuru, kwa sababu huleta uhuru, Gal. 5:1; Yn. 8:32; Rum. 8:1-2.
- d. Yaitwa sheria kamilifu ya uhuru (Yak. 1:25), sababu sheria ni kamilifu na uhuru ni mkamilifu vile vile.

## II. MAFUNDISHO JUU YA SHERIA ZA MUNGU YASIYO SAWA.

A. Waadventisti wa Siku ya Saba. "Kanuni ya Mungu ya maadili isiyowezekana kubadilika iliandikwa na kile kidole cha kiungu. Ilitolewa na Mungu kwa utu wa vizazi vyote, na haikufutwa wala haikuondolewa wakati wo wote" (Mwandishi wa maneno hayo ameyaandika maneno hayo chini ya ukurasa mmoja wenye Amri Kumi.) Uk. 364, God Speaks to Modern Man.

Tena, "Sheria za Mungu na hali yake hazitengeki. Hakubadilika wala hatabadilika hata kidogo," uk. 372, kit. kile kile.

"Kwanza na juu ya yote, kuna sheri a ya maadili ya Amri Kumi zilizoandikwa na Mungu katika bamba za mawe", Kit. kile, uk. 375.

"Wakati wote Mungu anaishi, sheria yake inaishi pia. Hakuna njia ya kuzitangua zile Amri Kumi." Kit. kile, uk. 398.

B. Sayansi ya Kikristo (Christian Science). Mary Baker Eddy, mwanzishaji wa chama hicho asema kwamba mwanadamu hawesi kuzivunja sheria za Mungu, wala hakuna yo yote kama dhambi, mwenye dhambi, wala haja ya kuwapatanisha na Mungu. Science and Health, uk. 491; Unity of Good, uk. 74, 64. Akaua mauti na hukumu, jinsi Biblia inavyozifunua wazi, Misc. Writtings, uk. 42, 65. Science and Health: 469:21; 450:19. Kwa hiyo akana sheri a za msingi wa Mungu hasa!

C. Umormoni. Wangerudisha tena sheria zile za sadaka zilizokuwa zikitia sharti chini ya sheria ya kale, lakini ziliondolewa wakati wa kufa kwake Kristo; Joseph Fielding Smith, "Sasa katika halii ya vitu, lazima sheria ya sadaka irudishwe tena ... Sadaka ya kumwaga damu ilianzishwa wakati wa Adamu, na kwa sharti lazima

irudishwe tena." Doctrines of Salvation, Kit. cha 3, uk. 94.

D. Ndugu Zetu (Our Brethren). Nia ya E. C. Fuqua kuhusu sheria za Mungu za ndoa. Asema kwamba sheri a hizo haziwezi kutumika kwa watu wa nje ya Kristo. Angalia, "watu wakikaa duniani hawawezi kuwa na wala kuwa bila cho chote kilichoandikwa na kuwa asili ya yo yote, wakiona kwamba hawapo chini ya sheria ya Kikristo, bali chini ya sheri a ya Kiserikali peke yake" - Pia, "Sheria yake yote na utoaji wake wa sheri a hutumika katika kanisa, na kati ya washarika wake peke yake; kwa hiyo ulimwengu sio chini ya sheria ya Kristo hata kidogo." Tena, "wala sioni ambapo wale wa ulimweriguni wapewapo na Mungu sheria yo

yote juu ya jambo lo lote. Mataifa na wale wengine wasioamini hawana sheria ya kumwelekea Mungu;" The Warren Fuqua Debate, uk. 10-11.

Ndugu Pat. Harrell ayafundisha yale yale hasa, akisema, "Ingawa wapagani hawakuwa na wajibu kwa maadili ya Kikristo, hata hivyo hawakuwa huru na mwongozi wala wajibu wa kiadili ... msingi wa maadili ya mataifa ni ule ule wa ufunuo wa asili ..... Mtu angeweza kuwa na wake wengi au wake mbalimbali wa kufuatana, hata hivyo asingezi kwa hali ya asili. Kwa sababu msingi, jinsi wajibu wa mataifa ulivyoelezwa, ni ule wa ufunuo wa asili ambao maadili ya Kikristo ya ndoa hayamo ndani yake, kwa hiyo siyo kwa bahati bali kwa kusudi kwamba Agano Jipyä halisemi lolote kuhusu hali ya ndoa ya 'Naongofu.' uk. 131, 132, 133-134. Divorce and Remarriage in the Early Church.

Sam. F. Meyers alisema, "Na ile kanuni juu ya 'kuishi katika uzinzi' ikifahamika hivyo, ni wazo ambalo ni nje kabisa ya Biblia. Yaani kama kanuni hiyo haiwezekani wakati ile sherehe haipo, basi bila shaka haiwezekani katika jamii za Biblia vile vile. Kwa kweli tumedaiwa sherehe (au sakramenti) hiyo na Papa Pius IV." Tena, "Kitu ambacho kimenikirihisha kila mara mpaka ugagazi, kikihu swali hila ni kwamba watu hawataki kuyasamehe yale ambayo Mungu amekwisha samehe. Yaani talaka kabla ya kugeuka kuwa Mkristo, upande wao ina maana kwamba yampasa Mkristo kumkataa mume (au mke) wa pili na kumrudia yule wa kwanza, hata ingawa mara nyingi haiwezekani kufanya la haki katika mambo kama hayo. Huu ndio mfano mwengine wa madaraja ya Kanisa yasiyo rasmi, lakini hutumika sana mionganoni mwa watu wadhaniwao kuwa huru." uk. 12, 18-19, Marriage Adultery and Remarriage, na Sam. F. Meyers.

(Nadhani kwamba labda Mungu atashikwa na ugagazi vile vile, kama wanadamu wakijibishana hivi na kukosa sana kueleza mistari ambayo ni sehemu ya maana katika Injili (Sheri a) ya Kristo ambayo yapasa kuhubiriwa kwa kila kiumbe duniani, Mk. 16:15-16. Na kwa Injili hiyo watu wote watahukumiwa, Yn. 12:48-50, binafsi, 2 Kor. 5:10-11, Siku ile Kuu ya Mwisho, Mt. 25:31-46. A. M. C.)

Hoja rahisi yenye sehemu tatu yaonyesha makosa katika mawazo ya Ndugu Zetu (Our Brethren):

1. Hoja kuu: Watu wote waivunjao sheria ya Kristo, ndio watu walio chini ya sheria ya Kristo. Soma Rum. 4:15.
2. Hoja ndogo: Watu wa duniani ndio watu ambao wameivunja Sheria ya Kristo. Soma Mdo. 17:23-31; Mdo. 2:38-41; n.k.
3. Azimio: Watu wa duniani ndio watu walio chini ya sheria ya Kristo. Soma Mk. 16:15-16. Jinsi Ndugu N. B. Hardeman alivyozoea kusema, "hili haliwezi kushindwa!"

AZIMIO:

Sheria za Mungu ni za ajabu kuangaliwa. Zilitolewa kwa ajili ya wanadamu kwa mwenendo wa miuda yote. Maisha yetu yatasitawishwa nazo, kama tukizitii. Hali za maisha yetu zimetiwu muhuri nazo, kama tusipozitii. Kama tukizipokea na kupendezwa nazo, tutajaziwa wingi wa heri kwa milele yote!

## ASILI NA HALI YA DHAMBI

INGIZO:

Dhambi ndiyo fumbo la mwanadamu, siyo la Mungu. Kwa sababu Mungu hana giza lo lote likaalondani yake. Ufahamu wetu wa dhambi tulio nao ni wa kadiri ile ile has a kama nia yetu kwa Kristo. Wachache sana husikitishwa na kuutambua uharibifu wa dhambi, sababu busara zetuzimekuwa pumbavu na akili zetu zimeingiwa na giza, ling. Ebr. 5:11-14. Juhudi yetuni ya maisha yetu yote, kwa sababu Shetani ni "Mdanganyifu wa ulimwengu wote", na hakomi kusonga mashambulio yake mbele. Kila mara aujua udhaifu wetu, akitenda kufuatana na huo. HIVYO NDIVYO ITUPASAVYO HATA SISI!! Mungu atusaidie!

### I. ASILI

- A. Dhambi ya Adamu na Hawa, na matokeo yake kwao.
  1. Iliivunja sheria ya Mungu, Mwa. 3:1-8.
  2. Adhabu: "Siku mtakapokula, mtakufa hakika." Mwa. 3:3 (Eze. 18:20).
  3. Mauti za aina mbilizilikuja kwa sababu ya dhambi.
    - a. Kimwili ... Wamekuwa hali ya kufa ... walitengwa na mti wa uhai.
    - b. Kiroho ... Isa. 59:1-2 .. walitengwa na Mungu.
- B. Matokeo ya dhambi ya Adamu kwetu.
  1. Dhambi iliingia ulimwengu kwa Adamu, na mauti kwa dhambi. Rum. 5:12.
    - a. Dhambi ya kwanza. Dhambi iliingia kwa mtu mmoja, 1 Kor. 15:21-22.
    - b. Hii ilikuwa mvunjo mkubwa, wa Mwa. 3:3.
    - c. Je, kwa maana ipi dhambi yote ilileta mauti juu ya wote? Kwa jinsi ya Adamu aliyekichwa cha 'maungamoya wanadamu wote. Rum. 5:12-13 (Je, hii ni kweli??? Ebr. 7)
  2. Mauti ya kimwili ilikuja kama tokeo la dhambi ya Adamu, Rum. 5:12-13. Mwanadamu ametengwa na mti wa uhai. Amekuwa mwanadamu impasayo kufa.
  3. Mwanamume alikuwa amefanyika kuwa juu ya mwanamke. Mwa. 3:16; Kwa nini? 1 Tim. 2:12-14.
    - a. Mwanamume aliumbwaa kama wa kwanza.
    - b. Mwanamke alidanganywa. (Nani aliyekuwa na dhambi kubwa zaidi?)

### II. HALI YA DHAMBI

- A. Dhambi ni Uasi. 1 Yoh. 3:4 ('Anomia' ... maana yake ni ama kupita, au kutokutii, kukosa .. kutokukuwa na sheria.)
  1. Yak. 2:9 ... "Kuhukumiwa na sheria kuwa wakosaji" (Neno hila ni 'parabatia' ... maana yake, kuwa bila idhini ya sheria ... Kum. 1:17).
  2. Kum. 9:7 ... "Mmekuwa na uasi juu ya Bwana" (Kuwa bila sheria .. kuyafuata mapenzi ya mwenyewe, kutokuwa na sheria).

3. 1 Tim. 2:12 ... "Mwanamke alikuwa katika hali ya makosa" (Katika hali ya kuvunja sheria .... uasi) ANOMIA.

- a. 1 Kor. 4:6 ... "Kuivunja sheria" (ANOMIA ... uasi).
- b. 1 Kor. 9:21 ... "wasio na sheri a" (ANOMOS).
- c. Rum. 2:12 ... "Waliokosa pasipo sheria" ... (ANOMOS).
- d. 1 Tim. 1:9 .... Waasi na wasiotii.

4. Kosa .... (PARABASIS).

- a. Rum. 4:15 (PARABASIS) .... kosa.
- b. Rum. 5:14 ... "Kosa la Adamu".
- c. Col. 3:19 ... "Iliingizwa kwa sababu ya makosa".
- d. Ebr. 2:2 ... "kosa".

e. Ebr. 9:15 ... "Makosa yaliyokuwa chini ya agano la kwanza".

B. Dhambi ni kutokuwa na haki, 1 Y oh. 5: 17 ... (ADIKIA .... kutokuwa na haki, upotovu" makosa, kuvunja haki.)

- 1. Zab. 119:172 ... "Maagizo yako yote ni ya haki."
- 2. Zab. 119:138 ... Shuhuda kwa haki.
- 3. Zab. 119:75 ... Kama mtu azitii shuhuda za Mungu, ndiye mwenye haki; kama mtu asipozitii shuhuda za Mungu, siye mwenye haki.
- 4. Rum. 6:13-14 ... msiitoe miili yenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi, Gal. 1:7. Kuigeuza injili (kugeuza ni neno lingine tu) kama kitendo cha kutokuwa na haki.
- 5. Yn. 7:18 ... ye ye anayetafuta utukufu wake mwenyewe, hana haki.
- 6. Rum. 3:5 ... Ikiwa udhalimu mmoja waithibitisha haki ya Mungu.
- 7. Rum. 1:18 ... na uasi wote wa wanadamu waipingao kweli kwa uovu. Pia Rum. 1:29, udhalimu wa kila namna.
- 8. Kulitii lisilo la haki (1 Yoh. 5:17).
- 9. 2 Thes. 2: 10, 12 ... madanganyo yote ya udhalimu.
- 10. 1 Yoh. 1: 9 ... Kutusafisha na udhalimu wote.
- 11. 2 Pet. 2:13-15 ... Kutenda mabaya.
- 12. Ebr. 8:12 ... Kuwasamehe maovu yao.

C. Dhambi huzaliwa na tamaa iliyodanganywa. Yak. 1:13-15.

- 1. Jinsi mwanadamu atendavyo dhambi, Yak. 1:13-15.
  - a. Tamaa.....hamu, maelekeo, baja.
  - b. Kuvutwa.....kudanganywa.
  - c. Kitendo au dhambi.
  - d. Mauti ... tokeo
- 2. Tamaa .. 'epithumia' (Taft. haja na kitu ambacho kimekataliwa, tamaa, haja).
  - a. Mk. 4:19 ... Tamaa za mambo mengine ziliizua lile neno.
  - b. Yn. 8:44 ... Baba na tamaa za baba yenu ndizo mtakazozitenda.
  - c. Rum. 6:12 ... Dbambi hutawala ... mkazitii tamaa zake.
  - d. Rum. 1:24 ... Mungu aliwaacha ... katika tamaa za mioyo yao.
  - e. Rum. 7:7 ... Singalijua kutamani, kama torati isingalisema "Usitamani."
  - f. Rum. 13:14 ... Msiuangalie mwiili, hata kuwasha tamaa zake.

- g. Gal. 5:24 ... Walio wa Kristo wanieusulubisha mwili pamoja an mawazo yake mabaya na tamaa zake.
- h. Gal. 5:16 ... Enendeni kwa Roho ... wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili.
- i. Efe. 2:3 ... Mazungumzo ... Tamaa za miili yetu . . . tulipoyatimiza mapenzi ya mwili.
- j. Efe. 4:22 .....Kuzifuata tamaa zenye kudanganya.
- k. 1 Tim. 6:9 .....Walio na mali nyingi huanguka ... na tamaa nyingi zisizo na maana, zenye kudhuru, ziwaso zanadamu.
- l. 2 Tim. 2:22 ... Zikimbie tamaa za ujanani; lakini ifuate haki.
- m. 2 Tim. 3:6 ... Waongoze ... wanawake wajinga wenyewe mizigo ya dhambi, waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi.
- n. 2 Tim. 4:3 ... walimu wanaojipatia tamaa zao wenyewe.
- o. Tit. 2:12 ... kukataa ubaya na tamaa za kidunia, tupate kuishi kwa kiasi.
- p. Tit. 3:3 ... tulikuwa waasi, tukitumikia tamaa za namna nyingi ..
- q. 1 Pet. 1:14 ... msijifananishenatamaa zenu za kwanza, za ujinga wenu.
- r. 1 Pet. 2:11 ... Ziepukeni tamaa za mwili zipiganazo na roho.
- s. 1 Pet. 4:2 ... Msiendelee kuishi ... katika tamaa za wanadamu.
- t. 1 Pet. 4:3 ... Tulipokwenda katika ujisadi. Tamaa, ulevi wa divai.
- u. 2 Pet. 1:4 ... Kuokolewana uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa.
- v. 2 Pet. 2:18 ... Wavutwa na tamaa za mwili.
- w. 2 Pet. 2:10 .. Kuufuata mwilikatika tamaa ya mambo machafu.
- x. 2 Pet. 3:3 ... Wenyewe kudhahiki wafuatao tamaa zao wenyewe.
- y. 1 Yoh. 2:16 ... Tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima.
- z. 1 Yoh. 2:17 ... Dunia inapita, pamoja na tamaa zake.
- aa. Yud. 1:16... Wenyewe kulalamika, waendao kwa tamaa zao - tamaa mbaya.
- bb. Mt. 5:27-28 ... Mtu atazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha zini.

D. Dhambi ya Kutokuamini, Ebr. 3:12-13 .. ('Apistias') .

1. Ebr. 3:12-13 ... moyo mbovu wa kutokuamini.

2. Yn. 16:9 ... ya dhambi, kwa sababu hawaniamini mimi.

E. Lisilotoka katika imani ni dhambi. Rum. 14:23. Mstari huu mara nyingi hutumika vibaya na ndugu zangu wenyewe. Mstari huu wahusika na mtu aivunjaye dhamiri yao - siyo mapenzi ya Mungu yaliyofunuliwa. Hii yaonyesha jinsi ilivyo vibaya nino kuvunja dhamiri yetu! Yawezekana kwamba twakosa, kama twayatenda yale ambayo dhamiri yetu yafiikiria kuwa sawa, kwa sababu dhamiri yetu labda imefundishwa vibaya. Lakini twalaumiwa kila mara, kama twaivunja dhamiri yetu bila kufikiria kwamba dhamiri yetu ni ya haki au siyo!

1. Yo yote ambayo mtu ayafanya, lazima aiamini haki ya hayo. (Lazima tushike dhamiri njema, yo yote tunayofanya, mema au mabaya.)

2. Kabla hajageuka kuwa Mkristo, Paulo aliamini ya kwamba kuwaua Wakristo ni haki. Lakini kama Paulo angalikataa kuwaua Wakristo, akiamini kwamba ni haki kuwaua, basi angalitenda dhambi! Hiyo ndiyo ya ajabu, lakini ni kweli!
3. Orodha:

Dhambi ya kuivunja dhamiri, Rum. 14:23. Mhubiri aamini kuwa ni haki kuhubiri kwamba mwanadamu aweza kuokolewa bila ubatizo.	Dhambi ya kutokuhubiri kwamba ni sharti kubatizwa. Biblia yasema kwamba ubatizo ni lazima kwa wokovu. Mk. 16:16.
Kama mhubiri huyu akisema kwamba ni lazima mtu abatizwe ili aokolewe, basi aivunje dhamiri yake, na kwa hiyo atenda dhambi.	Kama mhubiri huyu akihubiri kwamba mtu aweza kuokolewa bila ubatizo basi atenda dhambi, (aikosea Mk. 16:16 hasa, akiivunja dhamiri yake asiivunje.
Kama akiyahubiri yale aliyo na hakika nayo, havunji dhamiri yake wala hatendi dhambi ya kukosea Rum. 14:23, lakini aivunja Mk. 16:16.	Kama mhubiri huyu akihubiri kwamba ni lazima kubatizwa, lakini haiamini, basi haikosei Mk. 16:16, lakini aivunja Rum. 14:23.

Kwa hiyo lazima mtu aishi katika nuru ya dhamiri yake, lakini mara nyingine yapasa dhamiri yake ifundishwe tena. Hiyo ndiyo iwapasayo Wakristo vile vile.

- F. Ajuaye kutenda merna, wa1a hayatendi, kwake huyo ill dhambi. Yak. 4:17.
1. Jinsi dhambi itendewavyo hasa. Mt. 25:31-46. Ni wachache sana mionganoni mwetu tusiohukumiwa na dhamiri yetu wenye kuhusu kweli hizo kuu?!
  2. "Usipotenda vyema dhambi iko, inakuotea mlangoni," Mwa. 4:7.
- ANGALIA: Je. mtoto mchanga aweza kuwa mwenye dhambi, isipokuwa aivunja yo yote ya aina hizo za dhambi?

### III. TABIA ZA DHAMBI:

- A. Dhambi ndiyo yenyewe udanganyifu. Ebr. 3:13.
1. Efe. 4:22 .....Tamaa zenyewe kudanganya.
  2. Kol. 2:8 .....Madanganyo matupu.
  3. Mwa. 30:13 .....Nyoka alimdanganya Hawa.
  4. Rum. 7:11.....Dhambi ilinidanganya, na kwa hiyo ikaniua.
  5. Mt. 13:22 ... Udhanganyifu wa mali hulisonga lile neno.
  6. 2 The. 2:10 .....Madangayo ya udhalimu.
  7. 1 Kor. 15:33 .....Msidanganyike; Mazungumzo mabaya huharibu tabia njema.
- B. Dhambi ni ya kujifurahishia ... (APOLAISIS ... Imejaa anasa) Ebr. 11 :25.
1. HEDONE ... (Anasa) Lk. 8:14; Tit. 3:3; 2 Pet. 2:13.
  2. SPATALOSA ... Kwa Kiyunani (kutokujiuzia nafsi yake ... kujifurahisha mwenyewe) 1 Tim. 5:6.

- C. Dhambi ni ya kuenea pote (Rum. 3:23) ndani ya kanisa na nje yake.
- D. Dhambi hushirikianishwa kwa urahisi, kwa sababu ya wenzetu. 1 Kor. 15:33.
- E. Dhambi ni ya kujificha. Mwa. 3:8; Yn. 3:19 ... Waangalia po pote, isipokuwa juu.

#### VI. SABABU ZA DHAMBI:

- A. Chini ya mvuto wa viongozi wenyewe busara, (1 Fal. 15:30). Upendo wa mambo ya kisasa au wa kujitenga. chini ya mvuto wa viongozi wake .... Upande wa kanisa, viongozi dhaifu ni sawa na usharika dhaifu. Viongozi wema watatokea kwa usharika imara. Shirika lo lote ni kama kivuli kirefu cha viongozi wake tu. Hayo nayathibitisha bila kusita!
  - 1. Wazo la Hitler kuhusu taifa lililo bora kuliko mataifa yote mengine, liliwafanya watu kuyaacha mawazo yao wenye na kuvichagua vimeo vyta taifa; hata hivyo ni watu waliomfanya Hitler kuwa na utawala.
  - 2. Hume na Spinoza waliiwafanya watu kuweka mbele dini ya kiakili isiyo na kumcha Mungu ye yote.
  - 3. Ndugu aweza kukosea na kuwaongoza wengi katika upotevu kwa sababu ya mvuto alio nao juu yao, 20:29-31. Wazee wabaya na wahubiri waovu, kuliko kundi lo lote lingine kanisani, huwapoteza watu wengi.
- B. Kukawisha kwa Adhabu (Mpango wa kununua anasa ya kimwili) Mhu. 8:11.
  - 1. Uongo wa Anania (Mdo. 5) uliadhibishwa mara moja. Hofu kubwa ikalipata kanisa.
  - 2. Lakini, dhambi nydingine zatupata mapema! 1 Tim. 5:24.
- C. Tamaa ya kujifurahisha katika dhambi. Ebr. 11:25, soma Isa. 1:13-15.
- D. Kujijenga mwenye (Kol. 2:20 kinyume cha 2 Pet. 1 :6). Katika kiini cha dhambi kuna kule kujifanya yeye mwenye. Wazee waonywa kipekee, 1 Pet. 5:3.
- E. Kiburi huleta dhambi, 1 Yoh. 2:15-17. Kiburi kimetupata wengi wetu, kiasi cha kutisha!
- F. Tamaa huleta Dhambi. Yak. 1:13-15; Yos. 7:21; 1 Yoh. 2:17, 18. Ndugu waogopa kwa ajili ya wahubiri wasipatwe na tamaa fulani, yaani waona kwamba wana makosa, sababu mara nydingi wana makosa kweli!

#### V. MATOKEO YA DHAMBI:

- A. Mauti ya kiroho. Eze. 18:20; Rum. 6:23.
- B. Mauti ya kimwili. Rum. 5:12-14.
- C. Mateso ya ulimwengu, kufanya kazi kwa ajili ya riziki, uchungu katika kuzaa watoto. Mwa. 3:16, 17, 19.
- D. Huzuni, maisha yenye uzito, dhamiri iliyochukizwa, Mwa.3:7-11.
- E. Urafiki na unyumba zilizovunjika, n.k. Efe. 5:6; Kol. 3; Mit. 16:28.
- F. Dhamiri zimeuawa, kama tukiendelea katika dhambi, 1 Tim. 4:2.

#### VI. MIFANO YA MATOKEO YA DHAMBI:

- A. Adamu na Hawa. Mwa. 3.
  - 1. Wamekuwa wamdnigia hali ya kufa wakiwekwa chini ya nguvu ya mauti.

2. Walikufa kiroho, Isa. 59:1.
3. Walipoteza Edeni. Mwa. 3:23.
4. Dhamiri itambuayo makosa. Mwa. 3:7.
5. Walifukuzwa k.utoka katika kuwako kwa Mungu, Mwa. 3:24.

B. Kaini, Mwa. 4.

1. Hofu, Mwa. 4:14.
2. Amekuwa mtoro, Mwa. 4:12, na mtu asiyeye na kikao.
3. Ardhi haikumpa mazao yake. Mwa. 4:12.

C. Esau ... mtu asiyemcha Mungu, Mwa. 25:33-34; Ebr. 12:16.

D. Akani, Yos. 1:21.

1. Moyo wa Yoshua uliyeyuka. Yos. 7:6.
2. Wayahudi thelathini na sita waliuawa Ai. Yos. 7:5.
3. Jeshi la Waisraeli liliaibishwa.
4. Akani na jamaa zake waliuawa kwa kupigwa mawe, Yos. 7:25.

E. Daudi

1. Uriya aliuawa. 2 Sam. 11:15.
2. Mwana wa Daudi aliyezalia Bathsheba, alikufa, 2 Sam. 12:14.
3. Upanga hakuondoka nyumbani mwa Daudi. 2 Sam. 12:10.
4. Wanaume wengine waliwatwaa wake wa Daudi. Mwa. 12:11, 12.

F. Herode katika Mdo. 12:23.

G. Anania na Safira. Mdo. 5:1-11.

H. Sodoma na Goroma, Yud. 1:6-7.

Je, mifano mingapi ya kutishainahitajika, mpaka tutapiga magoti katika toba na sala, tukiamua kwa nguvu kuyaacha mabaya na kuyatenda merna siku zote za maisha yetu?

VII. THA WABU YA MWENYE HAKI:

- A. Habili, Ebr. 11:4.
- B. Henoko, Ebr. 11:5.
- C. Ibrahimu, Ebr. 11:8-10.
- D. Musa, Ebr. 11:24-29.
- E. Paulo, 2 Tim. 4:6-8.
- F. Yesu Kristo, Ebr. 12:1-4.

VIII. MAFUNDISHO YASIYO SAWA JUU YA DHAMBI, HALI YAKE NA ADHABU:

A. Ukatoliki wa Kiroma.

1. Kanuni ya Dhambi ya Asili na Hatia ya Kurithiwa. Augustino alikuwa mtambulishi mkuu wa kanuni hiyo akijadili kwamba ubatizo wa watoto wachanga usingekuwa na maana, kama kanuni hiyo isingekuwa ya kweli. Alijadili kwamba dhambi ya asili ni halii fulani iende leayo kwa njia ya kuzaliwa kwa kimwili tangu Adam mpaka vizazi vyote. Mwishowe hii imekuwa sababu hasa kwamba vyama vingine vyta dini vililipokea na kulikubali kosa Iile Iile. Kanuni hiyo yashikwa na waandishi maalum wa madhehebu mengi ya Kiprotestanti. Waamini kwamba hatia, na matokeo

vilevile, ya dhambi ya Adamu yamepashwa kwa wanadamu wote. Mara nyingi wataja Rum. 5:12 ili waihakikishe. Upande mwingine hiyo ndiyo iwafanyayo kulikubali wazo lile kwamba Iazima Mungu awaguse mioyo yao hasa kwa Roho Mtakatifu kabla hawajaweza kulikubali neno la Mungu na kuIiamini. Hayo yote yalianzishwa katika UkatoIiki, na yote hayo siyo ya kweli hata kidogo.

2. Kanuni ya dhambi za mauIisho na za kusameheka. "Luther alifundisha ya kwamba dhambi zote ni za uovu ule ule, na kwamba ni mubali kutofautisha kati ya dhambi za maulisho (zisizosamehewa) na dhambi za kusameheka, sababu alifikiri kwa ukosefu kwamba hata dhambi iliyo ndogo ina sumu ya shauku ya mauIisho ... Mafundisho yake yaIilaumiwa na Mkutano Mkuu wa Trento ... Tena ni kinyume cha akili na cha Maandiko Matakatifu. AkiIi hueleza wazi kwamba kuna tofauti dhahiri kati ya hasiraya ghafula ya chuki kwa sababu ya tabia nyepesi ya kushtusha (dhambi ya kusameheka) na dhambi ile yenye kusudi hasa la kuua au kuzini (dhambi ya maulisho)". uk 275, The Question Box, Bertrand L. Conway, C. S. P. The Paulist Press (andiko rasmi la Kikatoliki).

3. Sakramenti ya Toba "upande wa padre - ondoleo dhambi: 'Nakuondolea dhambi katika jina la Baba na Ia Mwana na la Roho Mtakatifu!' Upande wa yule atubuye majuto, m.y. huzuni ya moyo, na kuichukia dhambi ile iliyofanyika, na kuamua kutokutenda dhambi tena; ungamo; m.y. taarifa juu ya dhambi kwa padre ili kupata msamaha; kipatanisho; m.y. malipo ya adhabu ile ya muda kwa sababu ya dhambi zilizosamehewa." Kit. kile kile, uk. 280.

4. Ungamo la sikio la dhambi. "Ungamo la sikio halitajwi po pote katika Biblia, lakini Kristo mwenyewe aliliamuru kiungu, akiwapa Mitume wake uwezo wa kufungua na kufunga dhambi ... Kwa kifupi, mwenye dhambi Iazima aiweke wazi nafsi yake mbele ya padre ili aweze kujua hali ya dhamiri yake na, akisadikishwa na huzuni yake, amwagize malipo ya toba yaliyo sawa na kumfaa." Kit. kile, uk. 287.

5. Huruma ya kuachia. "Huruma ya kuachia haiihusu dhambi hata kidogo, wala zile za zamani, wala za sasa, wala zile zijazo. Ni kwa sababu ya dhambi.zilizosamehewa, kuipunguza kabisa au kisehemu adhabu ile ya muda, ikijaliwa na Papa na Maaskofu kutoka kwa hazina ya kiroho ya kanisa iliyojumlishwa kwa zile fadhiIi za Yesu Kristo zisizo na mwisho zenye msamaha, na zile fadhiIi nyingi za Watakatifu. Ni zaidi ya Iile ondoleo Ia kazi za kikanuni za toba tu, yaani yapunguza kweli kabisa au kisehemu adhabu ile mwenye dhambi aliyoipata na Mungu, ama hapa ama mahali pa Ahera ya kutakasia ... Kuanzia Kame ya nane, adhabu zile za kutubisha za Kanisa la zamani zimebadilishwa kuwa sala, kufunga chakula, kupiga mijoledi, haji za kwenda Roma na mahali patakatifu pengine kama Mt. Albano thuko Uingereza ria Mt. Y ohana huko Campostella kule Spania, kutoa zaka kwa makanisa na mahospitali, kupiga vita vitakatifu, na kuweka mwaka wa makumbusho ya Huruma ya kuachia." uk. 294, 295, kitabu kile.

6. Ahera ya kutakasia (purgatory) - "Kanisa la Kikatoliki limedhihirisha kuwako kwa Ahera ya kutakasia, katika Azimio la Umoja lililopangwa kwenye Mkutano Mkuu wa Firenze, mwaka 1439, na tena kwenye Mkutano Mkuu wa Trento, likisema, 'Kanisa la Kikatoliki, likiongozwa na Roho Mtakatifu, likifuata Maandiko Matakatifu na mafundisho ya zamani ya Baba zetu, limefundisha katika Mikutano Mitukufu, na juzi tu katika ule Mkutano Mkuu. wa ulimwengu wote kwamba kuna Ahera ya kutakasia, na kwamba zi1e rohoambazo zimefungwa ndani yake husaidiwa na mavumilivu ya waaminifu, lakini zaidi has a husaidiwa na ile dhabihu ya kupendeza ya madhabahu' .... kwa hiyo, wote wanaokufa wenye dhambi za kusamehewa au wenye adhabu ile ya muda ya dhambi zao isiyolipiwa bado, lazima wazipatanishe katika Ahera ya kutakasia." uk. 393, 394, The Question Box na Bertrand L. Conway, C. S. P.

B. Mashahidi wa Jehovah.

1. Dhambi ya Kurithiwa. "Mwanadamu aliumbwaa kwa mfano wa Jehovah, lakini alitenda dhambi kwa kusudi, kwa hiyo wanadamu wote tangu kuzaliwa kwao ni wenye dhambi, tena ndio 'wa ulimwengu'. uk. 29. Jehovah of the Watch Tower, Martin na Klamm.

2. Dhambi na adhabu yake. "Nafsi ya mwanadamu siyo ya milele, lakini ni chini ya nguvu ya mauti, yaweza kufa. Wanyama wanazo nafsi vile vile, ingawa mwanadamu ana cheo kikubwa zaidi kwa muumbo wa pekee ... Jehanum, ambayo maana yake ni mahali penye 'mateso ya moto' ambapo wenye dhambi wanakaa baada ya kufa mpaka wakati wa ufufuko. Hiyo ndiyo kanuni ya 'Dini iliyosimamika', siyo ya Biblia. Jehanum ndiyo kaburi la kawaida la utu, tafsiri yake hasa ni sheol (Kiebrania), 'mahali pa raha katika tumaini ambapo wale waliofariki wamelala mpaka wata-fufuliwa na Jehovah Mungu ... Adhabli ya milele ndiyo adhabu au rada ambayo haina mwisho. Maana yake siyo 'mateso ya milele' kwa nafsi zilizo hai. Maangamizo kamili, kufa mara ya pili, ndiyo ajali ya wote wamkataao Jehovah Mungu, na hiyo ndiyo ya milele." uk. 29, 30. Kitabu kile kile.

C. Wengine wa ndugu zetu. Kuna wale kanisani waaminio kwamba mataifa hawahesabiwi dhambi zao za kuivunja sheri a ya Kristo. Wafundisha hasa kwamba mataifa ni bado kama sheria kwao wenyewe wasimjibu Mungu kadiri sheri a ya Kristo yahusika, kwa sababu hawakuwa na nafasi ya kuisikia injili. (Labda hiyo sababu kwamba wengine hawashughuliki na kazi ya kuitangaza injili ulimwenguni mwote!)

1. E. C. Fuqua, katika kukizungumzia kitabu cha Thomas B. Warren juu ya ndoa, kinachoitwa 'Divorce and Remarriage, ataja Rum. 2:14, akisema kwamba mataifa hawakutenda dhambi kinyume cha sheria yo yote, bali kinyume cha dhamiri yao, kisha ataja Rum. 5:13. Alisema wazi kwamba ulimwengu (nje ya Kristo) hawawezi kutenda dhambi kinyume cha sheria ya Mungu, kwa sababu hakuwapa sheria! Ndugu Fuqua amaliza akisema kwamba mataifa "hawana sheri a ya kuandikwa ya aina yo yote". uk. 86, 88, WarrenFuqua Debate. K wa hiyo aamini kwamba wale walio nje ya kanisa leo, wanafanya dhambi wakati wanaivunja dhamiri yao (au sheri a

ya kiserikali); kwa sababu hii, injili haiwezi kuhubiriwa "kwa kila kiumbe".

2. Pat. Harrell katika kitabu chake "Divorce and Remarriage in The Early Church" ameandika, "Kama mataifa ambao hawana ile sheria, wakifanya kwa asili yale ambayo sheria inaanrisha, basi ndio kama sheria kwao wenyewe, ingawa hawana sheria. Waonyesha kwamba yale sheria inayaamrisha yameandikwa katika miyo yao, dhamiri yao ikiusikia ushuhuda, na fikara zao zishindanazo zikiwashtaki au labda kuwardhisha, siku ile ambayo, kufuatana na injili yangu, Mungu atahukumu siri za wanadamu kwa Yesu Kristo. Wazo hilo la ufunuo wa kiasili likitumika na Paulo katika kuwajongelea mataifa, hiyo ndiyo ionekanayo katika hotuba yake kwenye Areopago .... Ufananaji wa hiyo na waraka kwa Warumi ni wazi sana. Tena ni kufuatana na wazo hila Paulo alitajalo akisema kwamba tabia za asili hufundisha juu ya urefu wa nywele za mtu. Uzinzi wakataliwa na fikira ile ya Kirabbi juu ya agano la Nuhu, na vile vile na wazo lile la Paulo juu ya sheria ya ndani .... Mwanamume angeweza kuwa na wake wengi au na wake mbalimbali wafuatanaao, na hayo yasingekuwa uzinzi kwa asili. K wa sababu msingi ambao wajibu wa mataifa huelezwa ndani yake, ni ule wa ufunuo wa kiasili ambao maadili ya Kikristo ya ndoa hayamo ndani yake, basi siyo kwa bahati bali kwa kusudi, kama Agano Jipya halisemi lolote juu ya hali ya ndoa za wale waliogeuka kuwa Wakristo." uk. 132, 133, 134.

Maangalizi:

Matokeo mabaya ya mawazo hayo madanganyifu ni wazi mara moja. Dhambi siyo tena kitu ambacho kitakuwa wazi juu ya msingi wa maelezo ya injili ya Kristo, bali kila mtu amekuwa akiwa sheria yake mwenyewe! Mafundisho kama hayo yanaivunja vile vile fikara ile ya Paulo katika Rum. 2, sababu hapo Paulo alikuwa ameeleza hali ya mataifa kabla ya kuja kwa injili ya Kristo! Sheri a ya Kristo imemelekezwa kwa watu wote, watu wa Athene wakiwa ndani yao!, Mdo. 17:30-31. Wayahudi na mataifa, Waamerika na Waafrika, wote huhifadhi uhusiano ule ule na injili ya Kristo. Hakuna mtu awezaye kuokolewa bila yake. Bila yake hao wote na wengine wote pia wamepotea!

Wayahudi na mataifa, Wazungu, Waasia na Waafrika, wote huhifadhi uhusiano ule ule na injili ya Kristo. Hakuna mtu awezaye kuokolewa bila yake. Bila yake hao wote na wengine wote pia wamepotea!

Maana yake ndiyo kwamba kila mpagani kutoka Texas mpaka Timbuktu (Ulimwengu Huu. H.S.), yambidi kuwa na wajibu mbele ya Mungu, akiwa amepotea katika dhambi, Rum. 3:26 na Rum. 6:23. Tena maana yake ndiyo kwamba injili ya Kristo ni tumaini lake la kwanza, la mwisho, na la pekee aliO nalo kwa wokovu wake, Rum. 1:16, kwa hiyo heri tumjie kabla hatujachelewa sisi au yeye! Mk. 16:15-16.

### AZIMIO:

Dhambi kila mara siyo jambo la kupendeza wala la kusomea wala la kuzungumzia. Lakini kwa sababu ni kitu kikubwa katika maisha yetu na katika maisha ya kila mtu, na kwa sababu Biblia yasema mengi juu yake, lazima tuiangalie na kupiga hila na nguvu yake, "nguvu ya dhambi ni torati. Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo." Paulo, 1 Kor. 15:56-57. Amina!

## HALI YA YALE MAAGANO MAWILI

INGIZO:

- A. Maelezo: Agano ndilo mapatano, wosia, hitiari.
- B. Fikira hiyo ya agano hukubali pasipo uthibitisho kwamba kuna Washiriki wawili.
  - 1. Katika Agano la Kale.
    - a. Mungu
    - b. Waisraeli.
  - 2. Katika Agano Jipya.
    - a. Mungu.
    - b. Ye yote atakayeyapokea masharti.
- C. Hukubali pasipo uthibitisho kwamba kuna hali za aina mbili: ile ya Mungu na ile ya mwanadamu.
- D. Hukubali pasipo uthibitisho kwamba kuna sababu fulani ya agano au wakati fulani ambao limetolewa.
- E. Hukubali pasipo uthibitisho yale ambayo yamo ndani yake.

### I. AGANO LA KWANZA. Ebr. 9:13; 8:13.

- A. Maelezo ya kihistoria; Ahadi ile katika Mwa. 3:15 iliyakusudia machache tu.
  - 1. Mwa. 3:11
    - a. Jinsi dhambi ilivyoingia. Mwa. 3. Adhabu yake. Mwa. 3:15. - yaeleza kwa kiasi kwamba Mungu atafanya kitu juu yake.
    - b. Uovu wa wanadamu uliendelea kuongezeka mpaka ulikuwa umevunjika na ile gharika. Mwa. 6.
    - c. Wakati walipoanza tena kuzivunja amri za Mungu, kulitokea na mchanganyiko wa lugha. Mwa. 11.
  - 2. Mwa. 12:1-3, Mdo. 7:2-3.
    - a. Wito wa kwanza huko Uri. Mdo. 7:2-3.
    - b. Wito wa pili huko Harani. Mwa. 12:1-3.
    - c. Ahadi ilielekea jamaa moja tu. Mwa. 12:3.
  - 3. Mwa. 12:7 - Nchi ya pekee iliahidiwa kwa Ibrahimu.
  - 4. Mwa. 17: 1-3 - Agano la tohara.
    - a. Kwa mwili - siyo kwa akili wala kwa moyo, Flp. 3:3.
    - b. Agano la kutengwa.
      - 1) Mwa. 17:14 - jamaa ya Ibrahimu ... ni hawa tu waliotahiriwa.
      - 2) Mwa. 21: 12 - Iliuelekea uzao wa Ibrahimu tu kwa njia ya Isaka.
      - 3) Mwa. 28:14 - Ilimwelekea Yakobo tu.
      - 4) Mwa. 49:10 - Ilimwelekea Yuda tu.
  - 5. Ilitokea kwa taifa la pekee - yaani kwa taifa hilo tu na ndani yake tu. Kut. 2:23-25.
- B. Agano lililotolewa na Mungu kwenye mlima wa Sinai, Gal. 3:16-17; Kut. 24:41.

1. Wakati wa Sheria (soma ili ulinganishe) Mwa. 15:13; Mdo. 7:6; Gal. 3:17.
2. Mapatano. Kut. 19:10-11; Kum. 33:31; ling. Ebr. 8:7-9; Kum. 5:1-3; Gal. 4:24; Kum. 5:22; Kut. 19:8.
3. Nani aliye lililofanyika pamoja naye. Kut. 19:1-8; Kum. 5:1-3, 22; Mal. 4:4.
4. Zile mbao mbili za sheria.
  - a. Kum. 5:22- Mbao za mawe ... hakuongeza nena.
  - b. Kut. 25:16 - Tia ndani ya sanduku huo ushuhuda.
  - c. Kut. 31:18 - Alimpa Musa mbao mbili za ushuhuda - Mbao za mawe zilizoandikwa kwa chanda cha Mungu.
  - d. Ebr. 9:4 - Sanduku la agano lenye mbao za agano ndani yake.
  - e. Kut. 34:27-28 - Nimefanya agano nawe, na pamoja Israeli, kwa mujibu wa maneno haya - huko siku arobaini - akaandika katika hiza mbao, hayo maneno ya maagano, hizo amri kumi. (Hizo zili-kuwa mbao mbili za pili - Kut. 34:1).
  - f. Kum. 4:12-14 - Akasema kutoka kati ya moto; akawahubiri agano lake, alilowaamuru kulitenda, yaani, zife amri kumi: akaziandika juu ya mbao mbili za mawe ... akaniamuru niwafundishe maagizo na hukumu, mpate kuzitenda katika nchi ile mtakcryoivukia ili kuimiliki.
  - g. Kum. 31:24-26 - Chuo cha torati kiliwekwa kando ya sanduku la agano.
  - h. 1 Fal. 8:9 - Hamkuwa na kitu ndani ya sanduku, ila zile mbao mbili za mawe.
  - i. Kum. 29:1 n.k. - Kulikuwa na maongezeko ya sheria zilizotolewa mlimani Sinai.
  - j. Kut. 20:23 - Yote yameandikwa katika chuo cha torati, Kut. 24:3, 4, 7, 8.
5. Jinsi kilivyowekwa wakf. Ebr. 9:18-22. Kwa damu. Kut. 24:5-8.
6. Damu ambayo agano lilitiwa muhuri kwake, ilionyesha tabia ya agano ilivyo.
  - a. Torati haikuweza kutakasa. Ebr. 10:1-4 - Torati ndiyo Mt. 26:28. Ilikuwa ya muda tu - haikuwa kwa milele.
  - b. Ilitengenezwa katika mwili. Mwa. 17:12-14. Iliwekwa wakf kwa damu ya mafahali na mbuzi. Kut. 24:7-8; Ebr. 9:12; 10:4.
  - c. Ile hema ya ibada ilionyesha kwamba ilikuwa muda tu: iliweza kuhamishwa, ilikuwa imetengenezwa kwa vifaa vilivyo chakaa, jinsi ya ibada yenyewe. Ebr. 9:8-10.
7. Udhifu wa Agano la Kwanza. (Angalia: Kama twasema juu ya udhaifu wa Sheria, usiishtaki nguvu ya yule mtoa-sheria; ilikuwa imetolewa kwa kusudi lake lenyewe Hi Iionyeshe udhaifu wake wenyewe.). Rum. 8:3.
  - a. Hali yake ya kuwa minghairi. Kum. 4:20; 5:1-5; 7:6; 26:18-19; Kut. 19:4-6; Zab. 105:4-6.
  - b. Agano hilo ilikuwa limevunjika kutoka mwanzo.

- 1) Waisraeli walilivunja kabla halijaandikwa, Kut. 32:1-30; 1 Kor. 10:7.
  - 2) Halitoi baraka kama limevunjika, Law. 26:14-16.
  - 3) "Wameziasi sheria - wamelivunja agano la milele" Isa. 24:5.
  - 4) "Ameyavunja maagano .... " Isa. 33:8.
  - 5) "Wameyarudia maovu ya baba zao ... nyumba ya Israeli na nyumba ya Yuda wameyavunja maagano yangu" Yer. 11:10.
  - 6) "Wameyavunja maagano yangu ... " Eze. 44:6-7.
- c. Lilifanya kazi upande wa nje tu.
- 1) Waliyaandika juu ya miimo ya nyumba. Hes. 15:38-40; Kum. 6:8-9.
  - 2) Lilikuwa na utakaso wa kimwili tu. Hes. 19.
  - 3) Lilikuwa na adhabu thelathini na tano za kufa, Ebr. 10:28.
  - 4) Lilikuwa na sheria za jinsi ya mwili tu likaamriwa mpaka wa matengenezo mapya, Ebr. 9:1-10.
- d. Kulikuwa na mstari wa kudumu wa adhabu za kufa chini ya sheria. Kum. 27:14; Rum. 4:14-15.
- 1) Kum. 27:14 - laana mbali mbali.
  - 2) Rum. 4:14-Haiwezekani kurithi kwa sheria ...
  - 3) Rum. 4:15 - Sheria ndiyo iliyofanya hasira.
  - 4) Kut. 32:1-28 - Watu elfu tatu waliuawa mwanzoni.
  - 5) 2 Kor. 3:7 - Huduma ya mauti.
  - 6) Rum. 3:19 - Torati ilitolewa ili watu wote wahukuiniwe wenye hatia mbele ya Mungu.
- e. Halikuwa na Kristo ndani yake. 1 Pet. 1:19-20; Yn. 14:1-8; Yn. 1:18.
- f. Halikuwa na Roho Mtakatifu ndani yake. Rum. 8:26-27; Gal. 3:1-5.
- g. Halikuwa na msuluhishi aliye hai mbele ya Mungu - makuhani walikuwa wadhaifu wenye dhambi vile vile.
- 1) Musa alikuwa amemwoa mwanamke Mkushi (Hes. 12:1)
  - 2) Haruni aliwaongoza watu wafanye ibada ya sanamu. Kut. 32.
  - 3) Makuhani wa sheria walikuwa makuhani wenye udhaifu. Ebr. 5:1-6; 7:27-28.
- h. Halikuweza kuondoa dhambi.
- 1) Law. 16:1-34 - upande wa nje tu.
  - 2) Ebr. 9:22 - Hata kutakaswa kwa kisherehe kwa kimwili, kwa sharti kulikuwa na damu.
  - 3) Ebr. 10:4 -- Damu ya mbuzi na ndama wa ng'ombe haikuweza kuondoa dhambi.
  - 4) Ebr. 9:15 - Kwa hiyo Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zilizokuwa chini ya agano la kwanza.

- i. Lile agano la kale halikuweza kuhesabia haki.
    - 1) Mdo. 13:37-39 - Kila aaminiye huhesabiwa haki katika mambo yaleyote asiyoweza kuhesabiwa haki kwa torati ya Musa.
    - 2) Mdo. 10:43 - Kila aaminiye atapata ondoleo la dhambi.
    - 3) Rum. 3:20 - Hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki kwa matendo ya sheria.
    - 4) Gal. 2:15-16 - Haiwezekani kuhesabiwa haki kwa matendo ya sheria.
  - j. Halikuweza kuhuisha. Gal. 3:21.
  - k. Halikuweza kutoa Haki.
    - 1) Gal. 2:21 - Kama sheria ingaliweza kutoa haki, yakini haki ingalipatikana kwa sheria.
    - 2) Flp. 3:9 - Haki ile ipatik~nayo kwa sheria, ni haki yangu mwenyewe· yakibinadamu tu.
    - 3) Rum. 10:3-5 - Wakitaka kuithibitisha haki yao wenyewe ... Kristo ni mwisho wa sheria kwa kila mtu aaminiye.
    - 4) Rum. 3:21 - Haki ya Mungu imedhihirika pasipo sheria ... hata haki ya Munru ilio kwa njia ya imani.
  - l. Halikuweza kumkamilisha mtu. Ebr. 7:19.
  - m. Halikuweza kuiletea dhamiri amani.
    - 1) Ebr. 9:9 - Haikuwezekana kumkamilisha mtu yule aliyeabudu ... kuhusu dhamiri yake.
    - 2) Ebr. 10:1-2 - Wasingejiona tena katika dhamiri yao kuwa na dhambi.
    - 3) Ebr. 9:14 - Damu yake Kristo itawasafisha dhamiri zenu na matendo mafu, mpate kuabudu.
    - 4) Ebr. 10:22 - Tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya.
  - n. Ahadi za Agano la Kale zilikuwa za ulimwengu huu, Kum. 11:13-17; 28:1-8.
  - o. Mungu aliona kwamba liIikuwa na ukosefu. Ebr. 8:6-8.
  - p. Watoto waliozaliwa chini yake walikuwa wakiwa watumwa wake. Gal. 4:24-25.
  - q. Hakuna urithi wa ahadi chini ya sheria. Gal. 3: 18; 4:30.
8. Kuondolewa kwa Agano la Kwanza.
- a. Yer. 31:31-34; Ebr. 8:6-13; 19:9 - Agano Jipyä litakuja.
    - 1) Agano lile la kwanza litaondolewa ili la pili litengenezwe.
    - 2)Lile la kwanza limekuwa la kuchakaa na la kutoweka. Ebr. 8:13.
  - b. Baraka za wakatihuu ni mbaIi na sheria. Gal. 3:1-7.
  - c. Kukombolewa na Kristo kutoka kwa laana ya sheria. Gal. 3:8-13.

d. Ahadi ile aliyopewa Ibrahimu haikubatiliwa na sheria ... Gal. 3:15-21.

- 1) Sheria ilikuwa ya muda tu. Gal. 3:19-24.
- 2) Baraka zilikuja kwa njia ya Kristo, Gal. 3:16.
- 3) Sheria iliingizwa mpaka mzao kitakuja, Gal. 3:19.
- 4) Sheria haikuwa sehemu katika agano la ahadi, Gal. 3:17-19.
- 5) Sheria iliingizwa kwa sababu ya dhambi za makosa. Gal. 3:19.

e. Sheria ilikuwa. kiongozi kutuleta kwa Kristo, Gal. 3:24.

- 1) Sheria ilikuwa imetuleta kwa Kristo. Gal. 3:24.
- 2) Imani ilipokuja, kazi ya kiongozi kile iliondo-lewa, Gal. 3:25.
- 3) Kuhesabiwa haki kwa imani - siyo kwa sheria. Gal. 3:26-27.
- 4) Hamna Myahudi wala Myunani tena - lakini sheria ilikuwa imeweka mpaka kati ya Wayahudi na Wayunani. Gal. 3:28-29.
- 5) Wote wamekuwa mmoja katika Kristo. Gal. 3:29.

f. Sheria ilikuwa kama wakili juu ya Wayahudi mpaka utimilifu wa wakati, Gal. 4:1-7.

- 1) Sheria ilikuwa juu yao mpaka utimilifu wa wakati. Gal. 4:1-3.
- 2) Kukombolewa kutoka kwa sheria, ulipowadia utimilifu wa wakati. Gal. 4:4-5.
- 3) Tumepokea hali ya kuwa wana - siyo watumwa tena - bali wana na warithi, Gal. 4:6-7.

g. Mjakazi alikuwa amefukuzwa: Mfano wa Sheria na Injili, Gal. 4:21-31.

- 1) Hawa ndio kama maagano mawili, 4:24.
- 2) Yerusalem ulio ni mwungwana, ndiye mama yetu, 4:26.
- 3) Watoto wengi zaidi wa yule aliyeachwa (mataifa), Isa. 54:1-8.
- 4) Kumfukuza mjakazi, Mwa. 21:10, 12.
- 5) Sisi si watoto wa mjakazi sheria. Gal. 4:31.

h. Kuwa hurukutbka kwa sheria. Gal. 5:1-12.

- 1) Kufanywa huru katika Kristo, 5:1.
- 2) Ye yote airudiaye sheria ameanguka kutoka katika hali ya neema, 5:4.

i. Kuifia sheria. Rum. 7:1-6.

- 1) Mume wa kwanza alikuwa sheria, mume wa pili ni Kristo.
- 2) Kuolewa na wawili wakati ule ule - huitwa uzinzi.

- 3) K wa sababu ya kuifia sheria kwa mwili wa Kristo, Kol. 2:14; Efe. 2:14-15; na kuolewa aliyefufuka kutoka kwa wafu. Rum. 7:5.
- j. Kutofautisha zile sheria mbili. 2 Kor. 3:1-18.
- 1) Barua zisizoandikwa katika vibao vya mawe ila katika vibao ambavyo ni mioyo ya nyama .... 2 Kor. 3:3.
  - 2) Andiko huua - bali roho huhuisha. 2 Kor. 3:6; Ebr. 8:6-13; Rum. 7:9-10.
  - 3) Wahudumu wa Agano Jipy - siyo wa andiko, bali wa roho, 2 Kor. 3:5.
  - 4) Utukufu wa yale ya Kale hubatilika (3:7) lakini mapya huzidi, 2 Kor. 3:9-10.
- k. Kukibomoa kile kiambaza cha kati kilichotenga na kuwafanya wale wawili kuwa mmoja. Efe. 2:11-22.
- l. Alizifuta zile hati zilizotushitaki na kuzigongomea msalabani. Kol. 2:14-19.
- m. Kama ule ukuhani ukibadilika, hamna budi sheria nayo ibadilike. Ebr. 7: 11-25.
- 1) Kama ule ukuhani ukibadilika, hamna budi sheria nayo ibadilike. Ebr. 7: 12.
  - 2) Kristo alitoka katika Yuda. Ebr. 7:14.
  - 3) Kuhani kufuatana na mithili ya Melkizedeki, Ebr. 7:15.
  - 4) Hakuwa kuhani kwa sheria ya amri iliyo ya jinsi ya mwili, bali kwa nguvu za uzima usio na ukomo .... Ebr. 7:16.
  - 5) Alifanywa kuwa kuhani pamoja na kiapo, Ebr. 7:20-21.
- n. Kulifanya lile agano lililo jipy. Ebr. 8:6-13.
- 1) Mjumbe wa agano lililo bora. Ebr. 8:6.
  - 2) Agano la kwanza lilikuwa na upungufu, 8:7.
  - 3) Agano la kwanza lilitolewa wakati "nilipowashika mikono yao .... " 8:9 ..
  - 4) Agano jipy liIikuwa likija, 8:8-12, Yer. 31:31-34.
  - 5) Agano la kwanza lilikuwa likitoweka. 8:13.
- o. Tofauti kati ya lile la kwanza na lile la Kristo. Patakatifu makuhani, na dhabihu. Ebr. 9:6-8.
- 1) Patakatifu, palipo pakubwa zaidi, 9:9.
  - 2) Sheria ilikuwa kwa jinsi ya kusafisha kimwili, 9:10.
  - 3) Dhamiri haikusafishwa, 9:9, 10:1-4, 9:14.
  - 4) Agano lilikuwa na nguvu palipotukia kufa kwa mtu. 9:16-17.
  - 5) Agano lile jipy liIiwekwa wakf kwa damu ya wanyama, 9:18-22.
  - 6) Agano lile jipy likiwa na dhabihu iliyo bora zaidi. 9:23-24.
  - 7) Kristo alitolewa sadaka mara moja tu, 9:25-28.

p. Tumaini letu halitoki katika agano lile la zamani, bali katika lile jipya, Ebr. 10:1-25.

1) Dhabihu wakati wa agano la kwanza. Agano hila halikuweza kuondoa dhambi, 10:4.

2) Damu ya Kristo ilimwagika ifanye hivyo, 10:19.

3) Katika Kristo kuna njiampya iliyo hai, 10:20.

4) Kuhani Mkuu aliye wa maana, 10:21.

5) Tumenyunyiziwa mioyo tuache dhamiri mbaya, tukaoshwa miili kwa maji safi. 10:22.

q. Musa alisema, lakini Mimi nasema; Mt. 5, Lk. 10, Mk. 6.

r. Mungu nyakati hizi asema katika Mwanawe. Ebr. 1:1; Mt. 17:1-8.

s. Kumsikia nabii katika mambo yote, kama ilivyokuwa na Musa. Kum. 18:15-18; Mdo. 3:22-26.

t. Kwa nini kuweka kongwa juu ya shingo za mataifa, ambalo baba zetu wala sisi hatukuweza kulichukua? Mdo. 15:10.

Kumbukumbu la pekee: Namshukuru sana Bw. Clinton D. Hamilton kwa hapo juu. Maelezo hayo yalichukuliwa kutoka kwa masomo yaliyofundishwa naye, wakati mwendishi wa kitabu hiki alipokuwa katika Chuo Kikuu (H.S.).

Maangalizi: Agano lile jipya hutofautishwa na lile la zamani kwa kila jinsi iwezekanavyo, lile jipya likionekana kuwa 1a juu zaidi katika kila jambo. Ye yote atafutaye leo kuishi chini ya lile la kwanza au akijaribu kuliweka juu ya ye yote mwingine, "ameanguka kutoka katika hali va neema" na pia "ametengwa na Kristo", Gal. 5:4.

## II. MAFUNDISHO JUU YA YALE MAAGANO MA WILI YASIYO SAWA!

A. Waadventisti wa Siku ya Saba. "Yaonekana kwa wote kwamba lazima kuna zaidi ya aina au jinsi moja ya sheria katika Biblia. Twajua kwamba zile amri kumi zilizo sheria nyadilifu ya Mungu, hazikubatilika msalabani.

Hayo ndiyo ambayo tumekwisha jifunza. Ni vibaya kwa kila mtu leo vile vile kuiba, kuua, kuzini au kuvunja yo yote ya zile Amri Kumi, jinsi ilivyokuwa vibaya zamani kufanya hivyo", uk. 375, God Speaks to Modern Man, na Arthur E. Lickey.

B. Umormoni: Umormoni hufundisha kwamba ule ukuhani wa Melkizedeki wa agano 1a zamani una mamlaka juu ya wote waaminio, hata leo. "Ukuhani huu wenye mamlaka hukusudia kuwasaidia watu katika jitahada zote za maisha, zile za muda na zile za kiroho vile vile. Kufuatana na wajibu za pekee zifaazo kwa mahitaji hasa.

"Nabii Joseph Smith alisema wakati fulani kwamba kila ukuhani ni wa Melkizedeki. Hii ndiyo kusema kwamba ukuhani wa Melkizedeki hushinda hitima zote na wote wenye mamlaka katika ukuhani. Rayo yanenwa wazi katika

kitabu kiiwacho "Doctrine and Covenants", ml. 107, mst. 5: 'mamlaka yote mengine au hitima katika kanisa zimewekwa baada ya ukuhani huo tu.'

"Kuna ukuhani wa aina mbili zielezwazo katika maandiko; yaani ule wa Melkizedeki na ule wa Haruni au wa Walawi. Rata kama kuna ukuhani wa aina mbili, ukuhani wa Haruni au wa Walawi umo ndani ya ukuhani wa Melkizedeki, ambao kama kichwa kikuu unayashika mamlaka ya juu yahusianayo na ukuhani, ukishika funguo za ufalme wa Mungu vile vile nyakati zote za ulimwengu kwa ajili ya fanaka za siku hizi duniani; ndio kama mlango ambao maarifa yote, na mafundisho, na mpango wa wokovu, na kila jambo lenye maana zafunuliwa kwake, zikipitishwa kutoka mbinguni." uk. 65-66. The Maize of Mormonism, na Walter R. Martin.

C. Waprotestanti walio wengi: Kama ukifutu mathubutu kwa ajili ya muziki za vyombo mbali mbali, ya kuishika siku ya sabato, au ya kutoa sheria ya zaka, wateteaji wote wa mambo kama hayo hulitumia lile agano la kale kwa uthibitisho wa vi tendo vyao. Agano lile la kale likikataliwa kwa maneno, ndilo msingi hasa wa vitendo vingi mno katka mambo ya dini leo.

#### AZIMIO:

Mungu alikuwa mtungaji na mdumishaji wa Agano la Kale. Sheria zake na maadili yake zimeyatimiliza yote Mungu aliyoyakusudia na kuyapanga. Ndiyo historia iliyoadikwa na masomo yavutayo sana, hata hivyo Mkristo leo huishi chini ya sheri a mpya iliyo bora zaidi ambayo atahukumiwa kwake.

## **HALI YA INJILI**

**INGIZO:**

- A. Injili ya Yesu Kristo ndiyo habari bora kabisa ambazo ulimwengu ulizisikia wakati wo wote. Si shani kwamba hata malaika walitangaza kufika kwake duniani! Lk. 2:8-14.
- B. Ujumbe huu mtukufu ulikuwa na yote ndani yake ambayo Yesu aliyafundisha akikaa duniani na kwa njia ya upuzio baadaye alipokuwa amepaa kumrudia Baba.
- C. Majina mengi hutumika kutaja ujumbe huo mtukufu wa ukombozi : "Injili ya utukufu", 2 Kor. 4:4; "Injili ya amani", Efe. 6:15; "Injili ya neema ya Mungu", "Injili ya Mungu", Rum: 1:1.

### **I. MAANDALIO YA INJILI KWA KUSUDI LA MILELE:**

- A. Kwa kusudi la milele la Mungu, Efe. 1:3-14. Mungu-mjenzi wa juu na jicho la maji wa baraka zote. mst. 3-6.
1. "Baraka zote za rohoni," Efe. 1:3, 2:6, 3:10-11.
  2. "Ametuchagua," Kum. 14:2.
  3. "Kuwekwa msingi ulimwengu", Yn. 17:24; I Pet. 1:20.
  4. "Ametutia mikono yake", Mdo. 4:28; 1 Kor. 2:7; Rum. 8:29-30.
  5. "Kuchaguliwa kuwa wana", Rum. 8:14; Gal. 4:5.
  6. "Kukombolewa," Ebr. 9:15, 22, 10:4.
  7. "Siri", Gal. 4:4, Mk. 1:14-15. (Ufunuo wa kusudi la Mungu kuwaokoa Wayahudi na mattaifa vile vile katika Kristo.)
  8. "Kusudi" Rum. 8:28. Mungu alikusudia kufanya hayo kabla ulimwengu haujakuwako! Tazama nguvu na utukufu na hekima ya Mungu wetu!
- B. Kwa Kristo kusudi la milele liliikuwa limetimizwa.
1. Kristo ndiye njia ya kuzipitisha baraka, Efe 1:7-12.
  2. Kristo ndiye ufunuo wa Mungu, Yn. 1:18.
  3. Kristo ndiye hazina za Mungu, Kol. 2:3.
  4. Kristo ndiye Mungu, Yn. 1:1-2.
  5. Kristo ndiye ukamilifu wa Mungu, Efe. 1:23; Kol. 1:19.
  6. Kristo ndiye aliyetangulia kuwa na sifa zote, Kol. 1:15-18.
  7. Kristo ndiye hekima na nguvu ya Mungu, Kol. 2:3, 1 Kor. 1:24; 1 Kor. 2:1-13.
  8. Kristo ndiye utimilifu wa Mungu, Kol. 2:9, Efe 1:10.

### **II. MAANDALIO YA INJILI KATIKA UNABII:**

- A. Ahadi zile mbili alizopewa Ibrahimu, Mwa. 12:1-3.
1. Taifa - ambayo ilikuwa ahadi ya nchi, mst. 1-2, 7.
  2. Ahadi ya kiroho - "kwa uzao wako" jamaa zote za dunia watabarikiwa, mst. 3.
- B. Mungu aliitimiza ile ahadi ya nchi.

1. Nchi - ambayo Mungu a1imwahidi Ibrahimu, Mwa. 12:1-3. Aliahidi upya kwa Isaka, Mwa. 21:12, 26:4, a1iiahidi ten a katika Mwa. 22:18, na kwa Yuda, Mwa. 49:11.
2. Ilikuwa yenyenye masharti, Kum. 29:1, 9, 22-28; Kum. 28, 30:1-10, Yer. 18:1-10.
3. Masharti yalikuwa yamevunjwa, 1aana iliingia, 2 Nya. 36:20-23.
4. Ahadi ya nchi ilikuwa imetimizwa. Chini ya Yoshua, Mungu aliitoa nchi yote a1iyoiahidi kwa mababa, Yos. 21:43-45, 23:15-16. Sulemani aliitawa1a hiyo yote 1 Fal. 4:21. Ahadi i1ikuwa imetimizwa, Neh. 9:7-8.
5. Mungu aliokoa yale "mabaki", Isa. 1:9, 10:20-26; 11:11; utumwa wa muda wa miaka sabini, Yer. 25:8-12, 29:10-14; 2 Nya. 36:17-25.
6. Ndiyo yaliyorudi tena, Ezr. 1; 9:13-15; Neh. 1:3-11; Hag. 1:12,1:14, 2:3.

**Maangalizi:** Hakuna cho chote ki1ichokosekana katika ahadi za Mungu. Anayeingojea nchi kutoka kwa Mungu leo, anangoja bure!

- C. Ahadi ya kiroho imetimizwa, Mwa. 13:3, kwa "mataifa yote", 22:18.
1. Katika unabii, Isa. 7:14, 9:6-17, 22:22, 11:1-11. Soma pia Isa. 2:1-4, 28:11-16, 66:8, Dan. 2:44, 9:24-27; 7:24-27; Mal. 3:1.
  2. Katika maandalio, Mt. 3:3; Mk. 1:1-3; Mt. 3:16-17; Mk. 14; Lk. 1:16-17; Mt. 10:2-4, 10:5-7; Mt. 12:28; Lk. 17:20; 24:14-20.
  3. Katika ukamilifu, Lk. 1:26-33; Mdo. 2:22-37 (2 Sam. 7:11-14); Gal. 3:6-29.

**MaangaIizi:** Katika Yesu Kristo kila neno la unabii lihusulu injili, hali, ufalme, shughuli zake, na ahadi zake, limetimizwa. Anayeyangojea mengine, anangoja bure!

### III. HALI YA INJILI KATIKA UKAMILIFU:

- A. Injili iwaelekeayo watu wote wa nyakati zote na wa mataifa yote.
1. Mamlaka yake, Mt. 28:18-20; Yn. 12:48-50.
  2. Hali yake yahusuyo maisha, Mt. 5:48; 1 Pet. 1:15-17; 1 Yoh. 3:3.
  3. Hali yake ya kutumika, Lk. 24:47, Rum. 3:23.
- B. Injili itoayo amri, Ebr. 5:8-9.
1. Masharti yake yahusuyo wokovu, Yn. 8:24; Lk. 13:3-5; Rum. 10:9-10; Mdo. 2:38; Mk. 16:15-16; Mdo. 22:16.
  2. Masharti yake yahusuyo maisha, Mt. 5:48; 1 Pet. 1:15-17; 1 Yoh. 3:3.
  3. Masharti yake yahusuyo ibada, Yn. 4:24, Flp. 3:3; Yn. 17:17, 6:63; Efe. 5:19, Kol. 3:16; Mdo. 20:7, Mt. 26:28; 1 Kor. 16:1-2; 1 Kor. 8:1-5; 2 Kor. 8:9; Flp. 4:4-7.
  4. Masharti yake yahusuyo huduma, Mt. 7:12, 22:39; Yak. 1:27; Gal. 6:10; Rum. 12:10, 12:14-21; Yak. 2:14-26.
- C. Injili ya Upendo.
1. Kumpenda Mungu, Mt. 22:34-37.
  2. Kuwapenda waliopoteza, Rum. 10:1-3 .
  3. Kuwapenda wasiopendeza, Rum. 5:6-8.

4. Kuwapenda ndugu, 1 Pet. 1:22; Yn. 13:34.

D. Injili tamaa, Ebr. 1:1-2, 1:3; Gal. 1:23; Rum. 1:7. (badala ya mara nyingi)  
Ebr. 9:26-28; 10:2.

1. "Imani", Yud. 1:3.

2. "Mara moja", 9:26-28, 10:2.

3. "Kuihubiri", Gal. 1:11, 2 Pet. 1:21.

4. "Watakatifu", 1 Yoh. 3:1; Kol. 3:16.

Maangalizi: Injili imefunuliwa katika ukamiJifu wake. Hatuingojei nyingine! Injili ipo; Hakuna haja ya kuisaisha, wala ya kuiandika upya, wala ya kuiongeza; Ilikuwa imetolewa na mamlaka ya mbinguni na wadhamini wake wamesimikwa. Wale wanaongojea cho chote kingine, wanangoja bure!

#### IV. MAFUNDISHO YASIYO SAWA JUU YA INJILI NA HALI YAKE:

A. Mafundisho ya Umormoni hukana kweli za msingi za Injili:

1. Kuzaliwa na mwanamwali, "Wakati mwanamwali Mariamu alipompata mimba yule mtoto Yesu, baba alikuwa amemzaa kwa mfano wake mwenyewe. Hakuzaliwa na Roho Mtakatifu. Na baba alikuwa nani?

Alikuwa wa kwanza wa jamaa ya kibinadamu .... Yesu, kaka yetu, amezaliwa katika mwili na nafsi yule yule aliyekuwako katika bustani ya Edeni ambaye rii baba yetu huko mbinguni ... Wakati baba yetu Adamu alipoingia bustani ya Edeni, alilingia mwcnye mwili wa kimbingu, akimleta Hawa ambaye ni mmoja wao wa wake, wake wa kimbungu, pamoja naye ... yeye ndiye baba yetu na Mungu wetu, Mungu wa pekee ambaye sisi twahusiana naye." uk. 96, The Maze of Mormonism, na Walter R. Martin.

2. Damu ya Kristo, "Hakuna mwanamume wala mwanamke ambao wakiyavunja maagano yaliyofanyika na Mungu wao, hawatashitakiwa kuilipa adhabu ya mauti. Damu ya Kristo haitayamwaga hayo hata kidogo. Lazima damu yako mwenyewe iyalipie hayo . . . ." Kit. kile, uk. 11 1.

3. Kufa kwake Kristo mara ya pili, "Wakikuamini kuja kwake Yesu mara ya pili hasa, Wamormoni hufundisha kwamba wakati Yesu atakaporudi tena, Wayahudi wa.takuwa wamekusanyika katika nchi ya Palestina, na Wamormoni watakusanyika kwa jinsi ya ajabu katika jimbo la Missouri, hukumu ya Bwana itakapotolewa mahali pote pa duniani isipokuwa katika Yerusalem ule wa zamani na ule Yerusalem mpya. (Taz., Doctrine and Covenants, fungu 29, mst. 9-11.) uk. 118, kit. kile. (Hayo ni mbali mbali kidogo tu na mafundisho ya Waprotestanti wote wauaminio ufalme wa Yesu udumuo duniani kwa muda wa miaka elfu moja. Biblia haifundishi hivyo; taz. 2 Pet. 3:1-15. A. M. C.)

B. Mafundisho ya Maashahidi wa Yehovah hukana.

1. Injili ya Kristo, "Katika mpango wao, injili yashika nafasi ya pili tu baada ya utetesi ule wa miaka elfu moja ujao ... Hiyo yaeleza wazi, kwa nini nyumba zao za kukutanikia haziitwi makanisa, bali Majumba ya Ufalme." uk. 9, The Bible, The Christian and Jehovah's Witness, na Gordon R. Lewis.

2. Uungu wa Kristo katika injili, "Ndilo jambo la hakika kwamba Biblia haifundishi po pote usawa wa Mwana wa Baba, bali hufundisha kinyume cha hayo hasa; huonyesha kwamba Mwana yu katika hali ya kuwa chini ya Baba, kwa hiyo ndiye mdogo kuliko Baba," uk. 12, kit. kile.

AZIMIO:

Injili ya Yesu Kristo ndiyo habari bora mno ambazo ulimwengu umezifahamu wakati wo wote. Ndiyo ujumbe wa wokovu kwa nafsi ye yote azitiyiye amri zake na kuzipokea ahadi zake. Ndiyo "habari njema" kwa kila mtu. Mungu atusaidie tuipokee kwa furaha na kwa shukrani.

## HALI YA IMANI

### I. INGIZO:

- A. Maelezo ya Imani.
1. Ebr. 11:1.
    - a. Katitka utafsiri wa Kiingereza uitwao King James Version twapata zaidi maelezo ya namna ya imani kuliko ya imani yenye.
    - b. Utafsiri mwingine uitwao American Standard Version (A. S. V.) husema - Imani ndiyo hakika ya mambo yatumainiwayo, thibitisho la mambo yasiyoonekana.
  2. Imani ndiyo matumaini. 2 Kor. 5:1.
  3. Imani ndiyo kujua. 2 Kor. 5:6.
  4. Kwa imani twafahamu. Ebr. 11:3.

Angalia: Katika matumizi hayo yote kuna msingi fulani wa imani yetu.

- B. Kwa hiyo ushuhuda uliopokelewa ndio sawa na imani pamoja na utii ili mambo yale yatazamiwayo na yale yasiyoonekana yapatikane.

### II. NGUVU ZA IMANI:

- A. Imani hutuunganisha na mambo ya milele, yaani na mambo yasiyoonekana, 2 Kor. 4:18.
- B. Imani hutupa ujuzi na ufahamu.
1. Ubora wa ufahamu huo, Zab. 119:98-100.
    - a. Hutupa ufahamu zaidi ku<sup>l</sup>iko adui zetu.
    - b. Hutupa ufahamu zaidi kuliko wazee wa zamani waliokuwa nao.
    - c. Hutupa ufahamu zaidi ku<sup>l</sup>iko wa<sup>l</sup>imu wetu.
  2. Mtu asiyefundishwa akiwa bila elimu lakini akiwa mtu aiaminiye Biblia hujua zaidi juu ya mambo yale yenye maana, kuliko mtu mwenye cheo cha juu cha Chuo Kikuu ajua juu ya mambo hayo kwa bahati ya elimu aliyo nayo.
  3. Mambo ambayo twayafahamu kwa imani.
    - a. Kwa imani twafahamu asili yetu. Ebr. 11:3; Kol. 1:16-19; 2:3.
    - b. Kwa imani twafahamu kusudi letu. Mhu. 2:3; 12:13, 14.
    - c. Kwa imani twafahamu madhumuni yetu. Rum. 2:5-11.
- C. Nguvu ilio kuu ya imani ndiyo kuwaokoa wanadamu, Rum. 5:1.
1. Mtu awezaje kuhesabiwa haki mbele ya Mwumba wake?
  2. Imani yamwekea Kristo mzigo wa dhambi zetu.
- D. Nguvu ya kuenenda kwa imani. 2 Kol. 5:7; Gal. 2:20, 21.
- E. Nguvu ya kustahimiIi. Ebr. 11:27, 35, 37; 1 Pet. 1:7; Ufu. 2:10.
- F. Nguvu ya kushinda. 1 Yoh. 5:4; Ebr. 11:33; Ufu. 3:21.

### III. IMANI IOKOAYO NI NINI?

- A. Wengine husema ni nini?
1. Imani ndiyo kiumbe kilicho juu.

2. Imani kwa mmoja aliye juu, yaani Mungu, Yn. 14: 1.
3. Bayana ya kwamba Yesu ndiye Mwana wa Mungu, Mt. 8:29.

Mashetani wafanyayo hasa:

- a. Wamwamini Mungu mmoja - watetemeka. Yak. 2:19.
- b. Wamwamini Kristo - kwamba ana nguvu ya kutesa - kwamba amekwisha panga wakati wa mateso hayo, kwamba amekuja kuwatesa wao wenyewe kabla ya wakati wao.
- c. Walimwungama Kristo.

4. Kumontaja Yesu kuwa Bwana wao binafsi, na kujinena kufanya mambo kwa jina lake. Mt. 7:21-23; Lk. 6:46.

B. Imani iokoayo ndiyo kumpokea Yesu Kristo kama Bwana na kumtegemea kwa kutosha ili tufanye jinsi alivyosema.

C. Maelezo ya Thayer: Onyesha katika orodha.

1. Bayana ya kwamba Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu.
2. Kumtegemea yeeye kama Bwana. kuungana naye.
3. Kuzitii amri zake.

#### IV. JINSI IMANI IOKOAYO IPATANISHAVYO:

A. Jinsi wengine wasemavyo: Kwa kipawa cha moja kwa moja kutoka kwa Mungu.

1. Wakatoliki huipata yao kutoka kwa Papa asiyeweza kukosea. naye kutoka kwa Roho Mtakatifu
2. Wamormoni huipata imani moja kwa moja kutoka kwa Mungu.
3. Wabatisti husema kwamba ndiyo kipawa kutoka kwa Mungu. Angalia jinsi wote wajikanavyo na kuyataa mafundisho yao wenyewe.

Swali: Je, Mungu aitoa imani kwa njia hizo tofauti? Hakuna mstari hata mmoja katika Biblia usemao kwamba imani ndiyo kipawa cha moja kwa moja kutoka kwa Mungu.

B. Biblia isemayo juu ya jinsi imani ijavyo.

1. Petro. Mdo. 15:7. "Mataifa husikia ... huamini".
2. Yesu. Yn. 17:20 "... Watakaoniamini kwa sababu ya neno lao."
3. Wakorintho. Mdo. 18:8 "waliposikia, waliamini, wakabatizwa."
4. Yohana. Yn. 20:30, 31 "hizi zimeandikwa .... ili mpate kuamini."
5. Paulo. Rum. 10:13-17 "iman. chanzo chake ni kusikia. "

C. Mpango wa Mungu wa imani ndio huo:

MUNGU	ANGALIA: Kama wale walio-
KRISTO (Yn. 14:8)	tajwa juu wakisema kweli, basi
MITUME (Roho	ni kosa la nani kama mtu fulani
Mtakatifu	haipati imani? Basi ni kosa la
Yn.14:26; 16:7-13)	Mungu! Kama hii.ni kweli, basi, kwa nini kuhubiri? Kweli
NENO	ndiyo - Rum. 10:14-17.

## V. JINSI IMANI HIYO IPASAVYO KUWA NAYO ILI TUOKOLEWE KWAKE :

A. Jinsi isivyo :' Fungu Ia tisa la Malezi ya Kimethodisti imani peke yake.  
Kama kuokolewa kukiwa kwa imani tu.

1. Kuokolewa kabla ya kumjia Mungu. Ebr. 11:6; Yn. 14:6.
2. Kuokolewa bila nguvu ya Mungu. Rum. 1:16; Yn. 1:11-12.
3. Kuokolewa kwa imani iliyokufa, Yak. 2:17, 29.
4. Mashetani wataokolewa, Yak. 2:19; Mt. 8:29.
5. Kuokolewa bila maungano, na wakati ule ule kuzipenda zaidi sifa za wanadamu klilikio sifa za Mungu. Yn. 12:42, 43, kuelekeza na Mt. 10:32, 33.

B. Jinsi ilivyo:

1. Lazima kufanya kazi kwa upendo, Gal. 5:1-6.
2. Yak. 2:19-26 Kaza maneno yote yenye maana. Imani na utii, auimani na matendo yaweza kupatanishwa tu na Yak. 2:22.

Angalia: Tazama mmoja wa Mungu akimbariki mtu ye yote kwa sababu. ya imani yake. kama imani hii imejidhihirisha kwa kitendo fulani. Ebr. 11.

## VI. IMANI LAZIMA ITII LINI?

A. Lazima imani itii kama hakuna sababu ya utii ionekanayo duniani, isipokuwa yale Mungu aliyoyasema.

1. Nuhu hakuwa na sababu ya kuamini kwamba gharika yaja, isipokuwa kwa asili ya neno la Mungu, Mwa. 6:22.
2. Wengi husema, "Sioni, kwa nini yanilazimu kulifanya .... " Sababu ndiyo kwamba Mungu alisema, 'Fanya hivyo'.

B. Lazima imani itiikama jambo lile liagizwalo laonekana kuwa kinyume cha kila fundisho lililotangulia.

1. Ibrahimu akimtolea lsaka kuwa sadaka, alikuwa akimtolea mmoja aliyekuwa mtoto wa ahadi.
2. Jinsi ya imani Ibrahimu aliyokuwa nayo, Ebr. 11:19; Rum. 4:18-22.
3. Kufuatana na wengine, hii ingekuwa kuivunja "sheria moja ya maadili ya milele."

C. Lazima imani itii, kama akili ya binadamu haiwezi kuona wiano kati ya baraka zitamanikazo na njia ziagizwazo kuufikia mwisho huo.

1. Yule Naamani mwenye ukoma aliyejosha katika Mto wa Yordani.
2. Yule kipofu aliyenawishwa katika birika ya Siloamu, Yn.9.
  - a. Nini walilolitaka zaidi kuliko lo lote lingine?
  - b. Mungu alitumia kuponya kwa kimwili ili kuonyesha masharti ya kuponya. kwa kiroho. Yer. 8:22.
  - c. Je, akili ya binadamu yaweza kuona uhusiano wo wote kati ya kule kujiona mara saba katika Mto wa Yordani na kule kutakaswa. kwa ukoma, au ya kule kunawa huko Siloamu na kule kuponywa kwa kipofu?
3. Wakati mwisho ufikiwapo, je, njia za kuufikia au yeye aliyeleza jinsi ya kuufikia, hupata utukufu?
  - a. Naamani alimtukuza Mungu. 2 Fal. 5:14-15.

- b. Kipofu, Yn. 9:30, 32, 33.
  - c. Ubatizo wetu. Mdo. 10:47, 48.
4. Nguvu haikuwamo katika mto wa Y ordani, bali katika yeye aliyesema, 'Jioshe'.
  5. Nguvu haikuwamo, katika birika ya Siloamu, bali katika yeye aliyesema, 'Nawa'.
  6. Nguvu haikuwamo (haimo) katika maji, bali katika yeye aliyesema, 'Wabatizwe'.

AZIMIO:

Kwa hiyo, ubatizo kwa ondoleo la dhambi ni kuhesabiwa haki kwa imani.

## HALI YA UTII

### I. KATIKA AGANO LA KALE:

#### A. Maangalizi ya kutangulia:

1. Hali ya utii hutokana na Hali ya Mungu, Hali ya Mwanadamu, Hali ya Sheria, na Hali ya Dhambi.

2. Wakati wa peke yake amba mwanadamu aweza kusema kwamba ana uhusiano na Mungu ufaao, ndio wakati atiipo.

#### B. Utii huonyesha uhusiano ufaao kati ya Mungu na mwanadamu.

1. Shauri lile la Sauli, 1 Sam. 15:22, 23.

a. Sadaka ya kuteketezwa      kinyume cha Kutii

b. Kutii                                kinyume cha Dhabihu

c. Kutii                                kinyume cha Mafuta ya

beberu

d. Kuasi                                kinyume cha Dhambi ya uchawi

e. Ukaidi                                kinyume cha Dhambi ya ukafiri.

2. Mungu hutaka utii. Yer. 11:7, 8.

3. Mungu alimbariki Ibrahimu kwa sababu ya utii wake, Mwa. 22:18; 22:12.

4. Isaka alibarikiwa na kuipokea ahadi kwa sababu ya utii wake Ibrahimu, Mwa. 26:3-5.

5. Uhusiano uliofaa kati ya Mungu na Waisraeli ulidumishwa kwa njia ya utii wao.

a. Tiini sauti yangu.

b. Shikeni agano langu.

Tunu ya thamani kwangu

Mtakuwa - Ufalme wa makuhani

Taifa takatifu.

6. Mistari mingine mbali mbali juu ya jambo hilo.

a. Kum. 11:27, 28 - Mtakaposikiza, baraka ni hapo - msiposikiza, laana ni hapo, 30:1.

b. Yer. 11:1-8 - Itiini sauti yangu, mkafanye sawa sawa na yote (niwaagizayo ninyi) .... ndivyo mtakavyokuwa watu wangu, nami nitakuwa Mungu wenu.

c. 1 Sam. 12:14-15 - Mkimeha Bwana na kuisikia sauti yake, itakuwa vema kwenu, Mwa. 22:12; Ebr. 10:31; Mt. 10:28.

d. Isa. 1:19, 20 - Kama mkitii, mtakula merna ya nehi - kama mkikataa, mtaangamizwa kwa upanga.

e. Zek. 6:15 - Kama mkijitahidi kuitii sauti ya Bwana, baraka zitakuja juu yenu.

#### C. Kutoikutii kutaadhibika kwa ukali.

1. Kum. 11:28 - Kama msiposikiza - laana ni hapo.

2. Kum. 13:1-5 - Kama nabii wa uongo akikufanya uiabudu miungu mingine, atauawa.

3. Kum. 28:26 - Nanyi mtasalia waehaehe kwa hesabu, kwa kuwa hamkuisikiza sauti ya Mungu.
4. Law. 26:14-33 - Adhabu mbali mbali hutishwa juu ya Waisraeli, kama wakitenda dhambi.
5. Yer. 9:13-16 - Kuwaangamiza Waisraeli, kwa sababu ya kutokuwa na utii.
6. Yer. 18:10-12 - Mabaya juu ya Waisraeli, kama wasipoaeha uovu wao.
7. Isa. 65:12 - Mtainama ili kuehinja, kwa sababu hamkuitika.
8. Yer. 12:15-17; 3:12, 13 - Kama hawataki kusikia, watalaaniwa.

## II. AGANO JIPY A HUDHIHIRISHA TENA NA ZAIDI MASHARTI YA AGANO LA KALE JUU YA UTII NA ADHABU ZA KUTOKUTII:

A. Utii ndio sababu na sharti la wokovu kadiri mwanadamu akihusika.

(Hakika)

Ushuhuda katika A. J. - Imani (Tegemeo) huelekea -  
Utii uletao - (Baraka) (Furaha)

## III. HALI YA UTII KATIKA AGANO JIPYA:

A. Paulo.

1. Neema na utume iLi mataifa yote wapate kujitiisha kwa imani. Rum. 1:5.
2. Injili ijulikane na mataifa yote, ili waitii imani, Rum. 16:26.
3. Jami kubwa ya makuhani wakaitii iLe Imani, Mdo. 6:7.
4. Kwa imani Ibrahimu alipoitwa alitika, Ebr. 11:8.
5. Kwa hiyo, utii ni sehemu ya imani ya kweli, na vivi hivi tumeokolewa kwa imani.

B. Kristo na mtu binafsi, Ebr. 5:8, 9.

Kristo Mwokozi

1. Kaeni mkiwa mmeokolewa kwa utii, 1 Pet. 1: 14.

UTII

2. Hata mkapata kutii na kunyunyiziwa damu ya Yesu, 1 Pet. 1 :2.

Mtu Kuokolewa

C. Kristo na Mitume. Yn. 14:15, 23. Kum. 5:10.

1. Mkinipenda, mtazishika amri zangu. (Baba atampenda), Yn. 14:15.
2. Mtu akinipenda, atalishika neno (nasi tutakuja kwake) langu. Yn. 14:23.
3. Imani itendayo kazi kwa upendo, (Na kufanya makao kwake), Gal. 5:6.

D. Kristo na mawazo ya mtu binafsi: "Tukiangusha mawazo, kila fikira ipate kumtii Kristo." 2 Kor. 10:5, 6.

E. Kristo huonyesha uhusiano kamili na Mungu, Flp. 2:5-8; Ebr. 5:2, 9; Yn. 4:34, Rum. 5:19.

Maangalizi: Kuna kuitazamia hukumu ya kutisha kwa wale wasiotii. Ebr. 10:26-31; Rum. 12:19-21; 2 The. 1:7-9; 1 Pet. 4: 17. HaLi ya kutokutii hutajwa katika mistari kama hiyo, Efe. 2:1-3; 5:6; Kol. 3:6.

#### IV. YATOKANAYO NA HAYO NA AZIMIO:

##### A. Imani huunganishwa na utii.

1. Imani itendayo kazi kwa upande yafaa. Gal. 5:6.
  2. Imani hukamilishwa kwa matendo. Yak. 2:14-26.
  3. Wale ambao wanazifuata nyayo za imani yake Ibrahimu. aliyokuwa nayo kabla hajatahiriwa. Rum. 4:12.
  4. Kwa imani Ibrahimu aliiitika. Ebr. 11:8.
- B. Kujitakasa roho kwa kuitii kweli, 1 Pet. 1:22; Yn. 8:32; 17:17; 14:6; Ebr. 5:8, 9; 1 Pet. 1:2.
- C. Kila atakayeliitia Jina Ia Bwana ataokoka, Rum. 10:13; Mdo. 2:21; 22:16; 2:38.

Kuita - Kuokolewa  
Kuamini  
Kusikia  
Kuhubiri  
Kutuma

D. Ibrahimu hakusita kwa kutokuamini ... kama mtu akikoma kuamini, akoma kutii vile vile. Rum. 4:16-25; Ebr. 3:12,13; Ebr. 10:32-39. Na tena, kama mtu akikoma kutii, ndiyo kwa sababu ya kutokuamini.

## HALI YA WOKOVU

### I. INGIZO:

- A. Jinsi mazungumzo mengine katika masomo hayo yalivyoeleza kwamba:  
Wokovu hutanguliwa na mathibitisho hayo:
1. Mwokozi - Kristo.
  2. Kuokolewa - Wale wakubalio.
  3. Upande wa mwanadamu, haja na wokovu-kuanguka, mtu amepotea.
  4. Kuvunja amri - dhambi.
- B. Maangalizi: Kutoka mwanzo wa A. K. mpaka A. J. maana izidiyo ya jambo hilo la Wokovu huendelea kuelezwaza zaidi na zaidi.

### II. YALIYOMO KATIKA WAZO HILO LA WOKOVU:

- A. Ondoleo la dhambi zi1izopita.
1. Je, ondo1eo la dhambi hutokea duniani au mbinguni?
    - a. Mbinguni, yaani moyoni mwa Mungu. Ebr. 8:7-13; Yer. 31:31-34. "Dhambi yao sitaikumbuka tena."
    - b. Lifuatalo nalo: Kwa hiyo mtu angeweza kubna kwamba amesamehewa kweli.
  2. Je, mtu ajuaje jinsi apatavyo ondoleo??
    - a. Lazima Mungu aifunue.
    - b. Lazima tushawishiwe kwamba tumepotea.
    - c. Lazima tuamini kwamba atasamehe kama sisi tukiyakubali masharti ya msamaha.
  3. Je, twajuaje kwamba tumesamehewa?
    - a. Kwa ushuhuda ule ule utuelezao tufanyeje, 1 Kor. 2:10,11; Rum. 8:16.
    - b. Kuomba ushuhuda mwingine zaidi kwamba neno 1a Mungu hulidhania neno la Mungu.
- B. Mabadiliko ya uhusiano.
1. Mtoto anapozaliwa katika ulimwengu, roho yake hutoka kwa Mungu .... ikiwa bila dhambi. Upotofu kamili hauwezekani. Ezk. 18:19; Mt. 18:3-6.
  2. Tumekuwaje kuwa watoto wa Shetani?
    - a. Tukiyaruhusu maovu yatutawale. Yn. 8:16; 8:23. 34.38,42.44-41; Rum. 6:16.17.
    - b. Tukiufuata mwenendo wa ulimwengu huu. Efe. 2:1-3.
    - c. Tukichukuliwa na Shetani kuwa watumwa wake. 2 Tim. 2:26; Yn. 8:44.
  3. Je. uhusiano huo wa kuwa mtoto wa Shetani utakubalika?
    - a. Lazima utawala wa Shetani uvunjike - kwa Neno. 2 Kor. 10:3-5.
    - b. Lazima mtu autegemeze uhusiano na Mungu, Kristo" na Roho Mtakatifu, ambao hakuutegemeza kabla yake.
    - c. Lazima mtu afanywe mwana au azaliwe ndani ya ukoo wa Baba.
      - 1) Kukombo1ewa. Kol. 1:13.14.
      - 2) Kuzaliwa. Yn. 3:5 - Gal. 3:26.27.
      - 3) Kufanywa wana, Rum. 8:14-16.

4. Mambo yahitajikayo kwa uhusiano uliobadilika.

a. Upatanisho: Mabadiliko ya shauku.

- 1) Haikuwezekana kubadilisha uhusiano kabla hasira haijaondolewa. Kol. 1:20-22; - 1sa. 59:1,2; Yak. 4:4 n.k.
- 2) Haikuwezekana kupasha upatanisho kwa njia ya adhabu. Rum. 12:19-21.
- 3) Mungu alitumia kitendo cha upande. Alimweka Mwanawe pekee adhabu, ili aipate shauku yetu. 1sa. 53:4-6; 2 Kor. 5:18-21; 1 Yoh. 4:9,10; Rum. 5:6-11.
- 4) Kisha, miyo yetu imebadilika kwa upendo wa Mungu.

b. Kuzaliwa upya: Mtoto mchanga, 1 Pet. 2:1, 2; Tit. 3:8.

1) Maelezo ya upya huo:

- a) Kiumbe kipyta, 2 Kor. 5:17.
- b) Upya wa uzima. Rum. 6:4.
- c) Watoto wachanga. 1 Pet. 1:21, 22; 2:1,2.

2) Uhusiano mpya: Wana wa kiume na wa kike, Gal. 3:26, 27; 2 Kor. 6:18-21.

3) Jamii mpya ya ushirikiano, Efe. 5: 11; katika nuru: 1 Yoh. 1:6.

4) Ufahamu mpya: Masharti ya maisha ndani ya Kristo, Mt. 6:33.

5) Kiumbe kipyta kilicho safi, Tit. 3:8.

- a) Kuzaliwa upya kuletwako na Roho Matkatifu. 1 Pet. 1:22, 23.
- b) Kuzaliwa kwa maji na kwa Roho, Yn. 3:5; Tit. 3:8.
- c) Kuza1iwa kutoka katika wafu, Kol. 1:18; Efe. 2:1; Rum. 6:3-6.

C. Kuhesabiwa haki. Eleza kwa mifano: Kuurudia mpango wa kutokuwa na dhambi mwanadamu aliokuwa nao kab1a ya kuanguka.

1. Jinsi mtu asivyo hesabiwa haki.

- a. Siyo kwa matendo ya sheria, Rum. 3:20.
- b. Siyo kwa hekima yake mwenyewe, 1 Kor. 1:21 (Hawezi hata kumjua Mungu).

2. Jinsi mtu ahesiwiwavyo haki.

- a. Kama Mungu akimwinua mtu, sababu zake ni nini? Rum. 3:24-26.
- b. Kwa njia ya imani, Mdo. 13:39.

D. Wongofu. (Kugeuka tena) Mara nyingine "toba" hutumika badala yake. (Mdo. 11:18; 17:30, 31; 11:21).

E. Ukombozi (Kununua tena; fidia) Mara nyingine maana yake ndiyo:

1. Kazi ya Kristo. Efe. 1:7; Kol. 1:14. Mara nyingine maana yake ndiyo:
2. Ukombozi wetu binafsi, kwa damu ya Kristo, 1 Pet. 1:18, 19.
  - a. Kristo aliilipa bei yake.
  - b. Bei yatumika kwa ajili yetu, kama tukitii, 1 Pet. 1:21, 22.
  - c. Kukombolewa kutoka kwa sheria.

d. Tumekombolewa kutoka katika mazoeo yetu yasiyofaa. 1 Pet. 1: 18.

F. Utakaso (Sijo kazi ya pili ya Neema, bali kuwekwa mbali kwa ajili ya Kristo).

1. 1 Kor. 6:11; Mdo. 13:39 hueleza fundisho hila wazi.

a. Tumepata utakaso kwa k~tolewa mwili wa Yesu Kristo mara moja tu. Ebr. 10:10, 14.

b. Watu wa binafsi hutakaswa wakati wa toba, 1 Kor. 6:11.

c. Wakristo watakaswa, 1 The. 4:3.

d. Utakaso hutokea wakati wa kuwekwa mbali na ulimwengu - wakati tulivyoitwa kwa injili, Kol. 1:13; 2 Thes. 2:14.

AZIMIO:

Wokovu hutokea katika nia ya Mungu. Matokeo yake hayaonekani kabla hatujatii amri zake. Kama tukiyapokea Mungu asemayo na tukiyafundisha aagizayo, basi hatupo chini ya hukumu. Kama tukikosa kufanya hivyo, tupo chini ya hukumu tukapotea. Mungu atusaidie tuwe na upendo na utii siku zote, halafu wokovu utakuwa wetu.